15 MEI, 2023

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Ishirini na Tano – Tarehe 15 Mei, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali.

Tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 317

### Kuitambua Shule ya Mkalapa kuwa ya Mchezo wa Mpira wa Wavu

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA** aliuliza:-

Je, ni lini Shule ya Sekondari Mkalapa itatambuliwa kuwa shule ya vipaji vya michezo ya mpira wa wavu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Deo Ndejembi majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kuboresha miundombinu ya michezo katika shule teule 56 nchini ikiwa ni wastani wa shule mbili kwa kila Mkoa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapokea ombi la Mheshimiwa Mbunge la kutambua shule ya Sekondari Mkalapa kuwa shule ya vipaji vya mchezo wa wavu.

Nielekeze wataalam wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kutembelea shule hiyo ili kuona miundombinu iliyopo na namna shughuli za michezo zinazofanyika shuleni hapo ili kuona kama inakidhi vigezo vinavyotakiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anastazia Wambura swali la nyongeza.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninapenda kujua sasa ni lini Serikali itaanza kuimarisha miundombinu ya shule hizo 56 lakini niombe na miundombinu ya Shule ya Mkalapa pia iboreshwe?

Swali la pili, ninapenda pia nijue Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba shule zote zinapata walimu wa michezo ili kusudi vijana wetu waweze kushiriki katika michezo kikamilifu? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali itaboresha miundombinu ya shule hizi 56 ikiwemo kama nilivyosema tathmini inafanyika katika Shule ya Sekondari Mkalapa ambayo imefanya vizuri sana katika michezo ya UMISETA lakini vile vile michezo ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo Serikali inafanya tathmini na itaijumlisha na yenyewe Shule ya Mkalapa na tutatafuta fedha na kwenda kujenga miundombinu kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la walimu wa michezo. Katika ajira ambazo Serikali imetangaza hizi 21,000 ambapo 13,390 hizi ni ajira za walimu. Tutaangalia ni namna gani nayo tuna-*accommodate* walimu wa michezo, walimu wa kilimo, walimu wa ufundi ili kuweza kuboresha elimu yetu hapa nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jeremiah Amsabi Mrimi swali la nyongeza.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Shule ya Sekondari Ngoreme Wilayani Serengeti kumekuwepo na jitihada nyingi za wananchi na wadau mbalimbali za kujenga miundombinu kwa lengo la kuifanya kuwa shule ya Kidato cha Tano na cha Sita. Yamekuwepo maombi yangu mbalimbali mara kadhaa kwa TAMISEMI.

Je, ni lini sasa TAMISEMI mtaipandisha hadhi shule hii kuwa ya Kidato cha Tano na cha Sita?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Amsabi Mrimi kwa jitihada zake za kuhakikisha shule hii ya Ngoreme inapandishwa hadhi. Kwa sasa walikuwa wanamalizia ujenzi wa mabweni ili kuweza kuhakikisha kwamba shule hii inakidhi vigezo vya kuwa *A level* na baada ya hapo Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Wizara ya Elimu zitafanya jitihada za kuhakikisha shule hii inasajiliwa kuwa na mkondo wa Kidato cha Tano na Sita.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini sasa aulize swali lake, kwa niaba yake Mheshimiwa Regina Qwaray.

Washa kwanza kisemeo.

Na. 318

**Kukamilisha ujenzi wa maabara za shule za sekondari**

**MHE. REGINA N. QWARAY K.n.y. MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa maabara za sayansi katika shule za sekondari utakamilika kama ilivyokusudiwa katika bajeti ya 2022/2023?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali ilitoa kiasi cha shilingi milioni 180 kwa ajili ya ukamilishaji wa maabara Sita Halmashauri ya Mji wa Mbulu na tayari mabara hizo zinatumika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri ilitenga na kutoa shilingi milioni 30 kupitia mapato ya ndani ili kukamilisha ujenzi wa vyumba viwili vya maabara na ujenzi huo upo katika hatua ya umaliziaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga na kupeleka fedha kwa ajili ya umalizaji wa maabara 11 ambazo hazijakamilika kadri ya bajeti itakavyoruhusu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Regina Qwaray swali la nyongeza.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Swali la kwanza; je, kwa shule ambazo

zimekwishakukamilisha maabara, Serikali ina mkakati gani wa kupeleka wataalam wale *lab technician* ili waweze kutoa huduma katika maabara hizo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mkakati gani kwa maabara ambazo zimekwishakukamilika kupeleka vifaa ili wanafunzi waanze kujifunza kwa vitendo zaidi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kwenye swali lake la kwanza la nyongeza lini shule hizi ambazo maabara zimekamilika zitapelekewa wataalam. Serikali imetangaza ajira 21,000 kwa sekta ya elimu na afya na katika walimu tutaajiri jumla ya walimu karibia 13,390 ambapo wengi watakuwa ni walimu wa sayansi ili kwenda kukidhi hitaji hili la maabara katika shule hizi ambazo Serikali ilipeleka fedha kumalizia maabara.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la vifaa. Serikali itapeleka vifaa hivi kadri ya upatikanaji wa fedha lakini ni *priority* ya Serikali kuhakikisha wataalam wanapofika katika maabara hizi vilevile na vifaa vinakuwepo vya kufundishia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga Mbunge wa Vwawa sasa aulize swali lake.

Na. 319

**Barabara ya Iyula – Ipyana – Idunda**

**MHE. JAPHET N. HASUNGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kutoka Iyula – Ipyana hadi Idunda – Vwawa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Jimbo la Vwawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2021/2022, Serikali ilitenga shilingi milioni 250 kwa ajili ya kufanya matengenezo ya barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 10 kwa kiwango cha changarawe. Katika mwaka wa fedha wa 2022/2023, Serikali imechonga kipande cha barabara hiyo chenye urefu wa kilometa 3.5 kilichobakia kutoka Idunda kwenda Kitongoji cha Itete kilichopo mpakani mwa Wilaya ya Songwe na Mbeya kwa shilingi milioni 10.5.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuweka mipango ya matengenezo ya barabara hii kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Japhet Hasunga swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nashukuru sana kwa Serikali kutoa hizo fedha ambazo zimetumika katika hilo eneo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kipande cha Idunda – Soga kuelekea katika eneo la Mbeya Vijijini, Serikali imelima tu lakini haikuweza kuweka changarawe na kujenga kidaraja kidogo katika lile eneo. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba inakamilisha hilo eneo ili liwe linapitika wakati wote wa mwaka?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa ili wananchi wa Idunda, Ipyana waweze kusafiri hadi Iyula hadi kuelekea Makao Makuu ya Jimbo la Vwawa ni lazima kipande cha

Iyula – Hatete – Mbewe kikamilike ambacho mpaka sasa hivi bado hakijakamilika.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba inakamilisha kipande hicho ili kuwasaidia wananchi hao waweze kusafiri kiurahisi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu swali lake la kwanza la kipande cha Idunda – Soga ili kiweze kujengwa kuwa changarawe na kuna daraja ambalo Mheshimiwa Hasunga amelitaja lina changamoto. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 *TARURA* katika Wilaya ya Songwe, Halmashauri ya *Songwe DC* ilikuwa imetengewa shilingi milioni 650 tu, lakini katika mwaka wa fedha 2021/2022 na huu tunaokwenda wametengewa zaidi ya shilingi bilioni 2.8 kwa ajili ya utekelezaji wa barabara. Hivyo basi, nichukue nafasi hii kumuelekeza Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Songwe kuhakikisha wanafika kwenye barabara hii na kuona changamoto ambayo ipo ili waweze kutengeneza daraja hili ambalo amelitaja Mheshimiwa Hasunga la kuunganisha wananchi kati ya Songwe na Mbeya.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la wananchi wa Igana kupita barabara ya Iyula - Katete na Mbewe. Nirejee tena yale maelekezo ambayo nilikuwa nimeyatoa kwenye swali lake la kwanza, Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Songwe anapotembelea barabara hii ya Idunda – Soga ahakikishe anaangalia nini kimekwamisha barabara hii ambayo nimetoka kuitaja hivi sasa na kuweka mikakati ya kuweka changarawe na kuimalizia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe sasa aulize swali lake.

Na. 320

**Kutofanya kazi Mamlaka ya Mji Mdogo Nansio**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza:-

Je, kwa nini Mamlaka ya Mji Mdogo wa Nansio haifanyi kazi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Jimbo la Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tathmini iliyofanyika inaonesha kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo Nansio bado haijakidhi vigezo vya kupandishwa hadhi na kuwa Halmashauri ya Mji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mamlaka nyingi zilizoanzishwa bado zina upungufu wa miundombinu mbalimbali yakiwemo majengo ya utawala na huduma za kijamii, kwa sasa Serikali imeweka kipaumbele katika uboreshaji wa miundombinu katika maeneo ya utawala yaliyopo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mkundi swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukukru. Kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa, Sheria Na. 07 ya mwaka 1982 Kifungu cha 16 na 17, tarehe 01 Oktoba, 2007, Mji wa Nansio ulipewa hadhi ya kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo na ikaanza kufanya kazi. Sasa swali langu lilikuwa ni kwa nini kwa sasa haifanyi kazi na kutoa huduma kwa wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa kwa tathmini iliyofanyika wakati huo ilionekana haijakidhi vigezo kupandishwa hadhi kuwa Halmashauri ya Mji. Ni kwa nini sasa Serikali isifanye mapitio ya sifa zilizopo sasa ili mamlaka hii iweze kupewa hadhi ya Halmashauri ya Mji Mdogo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu maswali mawili ya nyongeza...

*(Hapa Saa 3.22 asubuhi umeme ulikatika)*

*(Saa 3.27 asubuhi umeme ulirudi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kimei swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba niulize; je, Serikali ina mkakati gani wa kuweka taa kwenye Mji mdogo wa Himo hasa eneo la barabara ambayo ni barabara kuu inayoenda nchi jirani na pia kwenye mji huko mpakani?

**SPIKA:** Swali la msingi linahusu miji midogo. Mheshimiwa Oran Manase Njeza swali la nyongeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa vile Mamlaka ya Mji mdogo wa Mbalizi kwa muda mrefu sasa imeshakua, na ina uchumi mkubwa, ni lini Serikali itaipandisha hadhi kuwa Halmashauri ya Mji wa Mbalizi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kuhusu kupandisha hadhi Mamlaka ya Mji

Mdogo Mbalizi kuwa Halmashauri ya Mji, kwa sasa Serikali inamalizia kwanza majengo ya kiutawala na huduma za kijamii katika mamlaka ambazo zipo tayari. Baada ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu katika mamlaka hizi, tutaanza sasa kuangalia ni wapi panahitaji napo kupandishwa hadhi na kuwa mamlaka ya mji kama vile kule Mbalizi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mamlaka ya Mji Mdogo Namanyere, tumeshafanyiwa tathmini na tumekidhi vigezo: Ni lini sasa tutapandishwa hadhi kuwa mamlaka ya Mji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mji Namanyere kupandishwa hadhi itakuwa ni baada ya Serikali kumalizia ujenzi wa miundombinu katika Halmashauri, Mamlaka za Miji na Majiji ambayo yamehama katika maeneo yao ya kiutawala, na sasa Serikali inapeleka fedha nyingi kumalizia maeneo hayo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Afya, Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 321

**Kukabiliana na ongezeko la wagonjwa wa kansa ya kizazi**

**MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kukabiliana na ongezeko la Wagonjwa wa Kansa ya Kizazi?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali katika kukabiliana na ongezeko la wagonjwa wa kansa ya kizazi, kwa kufanya yafuatayo:-

Moja, kutoa elimu kwa umma kuhusu kujikinga na ugonjwa wa saratani kupitia vipindi vya redio, televisheni, machapisho na magazeti, mitandao ya jamii kama facebook, *Instagram* na pia televisheni za sehemu za kusubiria wagonjwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Pili, Serikali inatoa chanjo kwa wasichana ili kuwakinga na kirusi kinachosababisha saratani ya mlango wa kizazi.

Tatu, kuanzisha huduma za awali za uchunguzi na matibabu ya saratani ya mlango wa kizazi kuanzia ngazi ya zahanati hadi hospitali za Taifa.

Nne, Serikali imeimarisha huduma za kibingwa za uchunguzi na matibabu kwa kuhakikisha uwepo wa wataalamu na vifaa tiba kwa ajili ya kukabiliana na Saratani.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Taasisi ya Kansa ya *Ocean Road Dar es Salaam* imekuwa na ongezeko kubwa la wagonjwa siku hadi siku na idadi kubwa ya wagonjwa ambayo inaongezeka hapo ni akina mama wenye matatizo ya kansa ya kizazi: Je, Serikali haioni haja sasa kuwasaidia akina mama hawa kufungua vituo vya kansa katika hospitali za kanda na mikoa ili kupunguza gharama za usafiri kwa akina mama hao na mahitaji muhimu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Serikali imeonesha kwamba kuna huduma za awali za uchunguzi wa kansa katika hospitali mbalimbali: Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kuziunganisha huduma za uchunguzi wa awali za kansa katika kliniki zetu za mama na mtoto ili mama apate huduma hiyo kabla na baada ya uzazi? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya ya kufuatilia eneo hili la afya ya akina mama. Nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake la kwanza kwamba Serikali yetu imejipanga, ndiyo maana mmetusikia hapa tukisema Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa kwa mwaka huu tu shilingi bilioni 290.9 kwa ajili ya kuleta vifaa tiba. Kwa hiyo, kwenye hospitali zetu za kanda na mikoa, vifaa vile vitasaidia kuchunguza, lakini kwenye kanda wanatibiwa kabisa. Kwa hiyo, hiyo huduma imepelekwa, kanda watatoa, mikoa watatoa. Tuliona juzi madaktari waliokuwepo hapa, kazi yao mojawapo ni kwenda kuhakikisha wanatambua mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwenye maana ya kufika kule wilayani, labda nikwambie tu, tunalichukua, tunaliongezea nguvu lakini wenzetu waliokuja hapa pia mojawapo ya kazi yao ni kukutana na akina mama mpaka kwenye vituo vyetu na zahanati, wakiendelea kuhakikisha kwamba mojawapo ya jambo la kuzingatia ni kuangalia hiyo saratani ya kizazi, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali ya nyongeza yawe mafupi. Mhehsimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kumekuwa na Waganga wa Jadi na wa Asili ambao wamekuwa wakibaini kwamba wao wanatibu kansa mbalimbali: Nini kauli ya Serikali kuhusiana na waganga hao ambao wamekuwa wakiwapa wagonjwa taarifa ambazo siyo sahihi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kauli yetu ni moja tu kwamba, yeyote atakayeibuka akiwa na jambo hilo, moja, tunatuma watu wetu wa Mkemia Mkuu, lakini taasisi ya tiba asili kuhakikisha na kukiangalia kile anachokisema kama ni kweli. Tunapogundua siyo tiba, tunamzuia kufanya hivyo na tunamtia moyo wa kuendelea kufanya utafiti na kufikiria namna ya kutatua kwa pamoja kwa kushirikiana na sisi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, swali la nyongeza.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii nami niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa swali la msingi linaongelea ugonjwa wa kansa, lakini mimi naongelea ugonjwa wa Malaria, ambapo utafiti uliofanyika 2017/2018 Mkoa wa Tabora tulikuwa na asilimia

11.7, lakini utafiti wa 2022 tuna asilimia 23.4. Nini mkakati wa Serikali wa kutuondolea janga hili kubwa la Malaria ambalo linasababisha vifo vingi zaidi? Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Naibu Waziri atapata nafasi ya kulijibu hilo swali kama swali la msingi. Mheshimiwa Neema Lugangira, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa. Kwa kuwa swali la msingi linauliza kuhusu ongezeko la kansa, mimi nilitaka kufahamu: Je, Serikali imefikia wapi katika kufanya tafiti kwenye mikoa ya kanda ya ziwa na suala zima la ongezeko kubwa la magonjwa ya kansa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, hatua tuliyoifikia tayari tumeshachukua *sample* kwa watu mbalimbali zaidi ya 700, na sasa ziko kwenye maabara kwa ajili ya kuchambua kwenye *level* ya *genetics* ili kuona hasa ni nini tatizo linalosababisha hali hiyo kule kanda ya ziwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy John Sabu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 322

**Kuanzisha huduma za *dialysis* kwa wagonjwa wenye kipato cha chini**

**MHE. LUCY J. SABU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha huduma za *dialysis* kwa Wagonjwa wenye kipato cha chini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy John Sabu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitoa huduma za matibabu ikiwemo huduma ya kusafisha figo *(dialysis)* kwa wagonjwa wote bila kujali kipato cha mgonjwa husika. Huduma hizi kwa sasa zinatolewa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali za Rufaa za Kanda, Mikoa na Hospitali Maalum, ikiwemo Hospitali ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa wito kwa wananchi wenye kipato kidogo kufuata taratibu zinazopelekea wao kupata misamaha ya huduma ikiwemo huduma hii ya usafishaji wa figo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy John Sabu, swali la nyongeza.

**MHE. LUCY J. SABU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Je, Serikali imejipangaje katika kupunguza gharama za huduma hii ya *dialyisis,* kwani kwa sasa ni shilingi 200,000 hadi shilingi 350,000 kwa mgonjwa anapoenda kuhudumiwa kwa mara moja?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kutokana na majibu ya Serikali, napenda kufahamu, ni utaratibu upi mgonjwa ambaye ana kipato kidogo afuate ili aweze kupata msamaha wa huduma hii ya usafishaji wa figo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge, lakini niseme, moja ni kwamba kwenye bajeti hii ambayo tunaiwasilisha sasa, mpaka jana tulikuwa tunakaa kuangalia maeneo mawili. Waziri wetu ameangalia kwenye eneo la mama na mtoto na eneo hili, na tumegundua kuna uwezekano badala ya tiba hii kuwa shilingi 350,000, inawezekana kabisa mtu akatibiwa kwa shilingi 90,000 hadi shilingi 150,000. Kwa hiyo, tuna mpango huo wa kushusha gharama hizi.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ni kwamba, mtu afuate utaratibu gani? Moja, akishakuwa na barua ya Mtendaji wake wa Kata, hiyo inatosha kumfanya aweze kupewa *exemption,* ndivyo utaratibu unavyosema.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sebastian Kapufi, swali la nyongeza.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Je, ni lini Serikali itaanzisha huduma hii ya usafishaji figo katika Mkoa wetu wa Katavi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwenye hospitali yao mpya ya Mkoa wa Katavi tayari vifaa vimenunuliwa, sasa hivi wako kwenye *finishing* ya aneo ambalo linatakiwa hivyo vifaa visimikwe halafu huduma hii itaanza mara moja kwenye mkoa wenu wa Katavi. Hata *CT-Scan* ambayo Rais wetu ameinunua imeshafika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kabula Enock Shitobelo, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Furaha Matondo.

Na. 323

**Upungufu wa wauguzi Hospitali ya Bugando**

**MHE. FURAHA N. MATONDO K.n.y. MHE. KABULA E. SHITOBELO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaongeza wauguzi katika Hospitali ya Bugando kwani kwa sasa ina upungufu wa wauguzi 1,200?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Bugando ina watumishi jumla 1,930, wauguzi wakiwa 667. Katika watumishi hawa wote, Serikali inawalipa mishahara watumishi 1,120. Hopsitali ya Bugando kwa mapato yake ya ndani inawalipa watumishi 2,205 mishahara kamili pia inawalipa watumishi 605 nusu mshahara.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Furaha Matondo, swali la nyongeza.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Bugando ni Hospitali ya Kanda, kutokuwa na watumishi wa kutosha kunaathiri utendaji kazi na hivyo kusababisha vifo vingi sana; na kwa kuwa Bugando inahudumia mikoa ya Kanda ya Kati, mikoa ya Kanda ya Magharibi na mikoa ya Kanda ya Ziwa: Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kulipa umuhimu suala hili ili kuweza kupata watumishi wa kutosha na kuweza kuondokana na tatizo lililopo la vifo vingi vya wananchi wetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza tunapokea maombi yake, na tutaenda kuyachakata kwa sababu Hospitali ya Bugando kwa siku inapata wagonjwa 1,200 mpaka 1,500 na unaona idadi ya watumishi hapa ni 1,930. Sasa tutaenda kuchakata tuone tutakachoweza kufanya, lakini mwaka 2022 walipewa watumishi 367. Kwa hiyo, tutaendelea. Kwa kuimarisha Hospitali ya Kanda ya Chato na kuimarisha hospitali yetu ya mkoa iliyopo pale na hospitali za wilaya, foleni itapungua kwenye eneo la Bugando na itawezekana sasa kumaliza hili tatizo la watumishi na msongamano uliopo pale.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara inayofuata. Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Juduth Salvio Kapinga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 324

**Kuimarisha ukusanyaji mapato biashara za mtandaoni**

**MHE. JUDITH S. KAPINGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha ukusanyaji mapato kwa biashara zinazofanyika mtandaoni?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa

Judith Salvio Kapinga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato, Serikali kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2022 ilifanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura Na. 332 na Sheria ya Ongezeko la Thamani, Sura Na. 148 ili kuwezesha kutoza kodi kwenye biashara zinazofanyika kwa njia ya mtandao. Aidha, Mamlaka ya Mapato Tanzania imeanzisha kitengo maalum kinachosimamia biashara za mtandao, ikiwa ni pamoja na kubuni na kuboresha mifumo ya usimamizi wa biashara za mtandao ili kuwezesha utambuzi, usajili na ukusanyaji wa kodi stahiki.

Mheshimiwa Spika, mikakati mingine ni pamoja na kuwajengea uwezo Maafisa wa Kodi juu ya namna ya kutathmini na kukusanya mapato ya kodi yanayotokana na biashara za mtandao, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Judith Kapinga, swali la nyongeza.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa majibu mazuri, ila nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tayari Serikali ina kitengo maalum na tayari inafanya utambuzi na ukusanyaji wa kodi hizi: Je, tangu jitihada hizi zifanyike, mapato yanayotokana na biashara hizi yameongezeka kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Pamoja na mikakati mizuri ambayo Serikali inafanya, bado biashara nyingi za kimtandao hazijafanyiwa utambuzi na hazifanyiwi ukusanyaji ikiwemo biashara ya *D & D;* Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha mikakati hii ili biashara hizi ziweze kufanyiwa utambuzi wa ukusanyaji mapema ili kuongeza mapato? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Judith, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza ni kiasi gani, naomba hili nijibu kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, Serikali imeendelea kulipa *VAT* na kwa taratibu zote na imechukua suala hilo na inaendelea kulifanyia kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea, Mbunge wa Korogwe Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 325

**Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde ya mpunga Korogwe Mji**

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde ya mpunga ya Mahenge, Goo na Kwamngumi - Korogwe Mjini.

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea, Mbunge wa Korogwe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mabonde ya umwagiliaji ya Mahenge, Goo na Kwamngumi ni miongoni mwa maeneo ya uzalishaji wa mpunga katika Halmashauri ya Mji Korogwe. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilitenga fedha kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde hayo. Mwezi Aprili, 2023 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilisaini mkataba wenye jumla ya Shilingi bilioni 1.85 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa miundombinu katika Bonde la Mahenge na Bonde la Goo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji katika Mpango na Bajeti ya mwaka 2023/2024 imepanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili kupata gharama halisi ya kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji katika Bonde la Kwamngumi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimea, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza naipongeza na kuishukuru Serikali kwa kutupatia fedha kwa ajili ya bonde hili moja. Tunaiomba Serikali itupatie fedha kwa mwaka unaofuata kwa ajili ya Bonde la Kwamngumi pamoja na Bonde la Kwamsisi kwenye Halmashauri yetu ya Korogwe Mjini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, Dkt. Alfred James Kimea kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumepokea maombi yake na kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi, tayari Kwamngumi tumeshaingiza katika Mpango wa mwaka 2023/2024 kwa ajili ya upembuzi yakinifu. Hivyo nimwondoe

hofu, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba inawekeza katika miundombinu ya umwagiliaji. Tutapitia tena na maeneo mengine ambayo ameyataja hasa katika eneo la Kwamsisi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Martha Mariki, swali la nyongeza.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa. Je, ni lini mradi wa umwagiliaji wa Mwamapuli uliopo Halmashauri ya Mpimbwe utaanza kujengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ukisoma katika kitabu chetu cha kwenye bajeti kiambatisho Na. 6, kimeelezea skimu ambazo tunakwenda kuzifanyia kazi kwa maana ya ujenzi kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, skimu ya Mwamapuli yenye hekta 12,000 Wilaya ya Mpimbwe ni sehemu ya utekelezaji wa ujenzi wa katika mwaka wa fedha unaokuja. Nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge skimu hiyo inakwenda kutekelezwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba tu kujua Serikali itaenda lini kuangalia skimu ya umwagiliaji ya Kisango na skimu ya umwagiliaji ya Mariwanda ili kuifanyia kazi. Lini mtaenda kuangalia skimu hizo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha skimu zote zinafanyakazi ili tuongeze eneo la kilimo cha umwagiliaji. Nataka nimuhaidi Mheshimiwa Mbunge, kwamba nitawaelekeza watalamu wangu kwenda kupitia maeneo ambayo ameyataja ili tuweze kupata picha halisi na tuingize kwenye mpango. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Leah Komanya, swali la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Je, ni lini Serikali itaendeleza Ujenzi wa skimu ya Kijiji cha Mwagrila baada ya kutumia shilingi bilioni 1.2 na haikuwa kwenye mpango wa Serikali? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tulituma watalamu kupitia skimu zote nchi nzima, zile ambazo zilikwama na zile ambazo zinahitaji marekebisho tumeishatengeneza picha nzuri ya kuzijua zote pamoja na hiyo ambayo ameitaja nataka nimtoe hofu ya kwamba ipo ndani ya mipango ya Serikali tutaitekeleza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza je, ni lini mradi wa Mgambalenga katika kata ya Ruaha Mbuyuni utakamilika, kwa sababu toka mwaka 2014 umeanza kujengwa lakini haupatiwi pesa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika skimu 42 ambazo zilifanyiwa upembuzi yanikifu na usanifu wa kina katika mwaka wa fedha 2022/2023 ni pamoja na skimu ya Mgambalenga. Hivyo katika Mwaka 2023/2024 skimu hii itaendelea kufanyiwa ukarabati wa miundombinu na kazi itafanyika kwa uharaka zaidi ili wakulima waweze kupata fursa ya kufanya kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani Mbunge wa Ushetu sasa aulize swali lake.

Na. 326

**Ujenzi wa nyumba za watumishi nchini**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa nyumba za Watumishi nchini hasa katika Halmashauri mpya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Geofrey Pinda majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi napenda kujibu

swali la Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Ushetu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2012 hadi 2014, Serikali kupitia Shirika la Nyumba la Taifa ilijenga nyumba za gharama nafuu 1,189 katika halmashauri 31 kwa ajili ya kuziuza kwa watumishi waliopo katika Halmashauri hizo. Aidha, kuanzia mwaka 2013 hadi sasa, jumla ya nyumba 983 zimejengwa na taasisi ya *Watumishi Housing Company* katika mikoa 19 na kuuzwa kwa watumishi wa umma na wanachama wa mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Serikali kupitia taasisi zake ikiwemo Shirika la Nyumba la Taifa na Watumishi *Housing* itaendelea kujenga nyumba bora kwa ajili ya watumishi wa umma ili kuwaongezea tija katika utendaji kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa shirika hili limekuwa linajenga nyumba katika halmashauri mpya zilizoko mjini. Je, ni lini sasa shirika hili litaanza kujenga nyumba za watumishi katika halmashauri zilizoko vijijini hasa katika Halmashauri ya Ushetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kwa kuwa Serikali inakuwa inapeleka fedha nyingi za ujenzi wa madarasa, zahanati na hospitalini lakini watumishi hawana nyumba kabisa. Ni lini mkakati wa Serikali kuwajengea nyumba watumishi hawa hasa walioko vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumba la Taifa *(National Housing)* limeendelea kujenga nyumba katika maeneo mbalimbali. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge wa Ushetu kwa kuwasemea watumishi wetu walioko

katika maeneo na hasa Ushetu huko, kitu kikubwa kabisa ambacho tunaweza tukaahidi ni kwamba tunaendelea katika hatua mbalimbali za ujenzi na katika muda wowote ule tutafika huko Ushetu.

Mheshimiwa Spika, ombi letu sisi kama Wizara nikuomba halmashauri zote kutenga maeneo ambayo wangependekeza kujenga nyumba hizi zinazosimamiwa na mashirika kama hiyo *National Housing* na Watumishi *Housing*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili; fedha nyingi zimepelekwa katika hizi mamlaka zetu za halmashauri kupitia TAMISEMI, na nimeona kwa sehemu kubwa sana fedha zinazopelekwa zinakuwa na kiambata cha nyumba za watumishi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swali la msingi kwa kupitia mashirika yetu haya taasisi zinazojenga nyumba zetu za watumishi. Sisi kama Wizara ya Ardhi tutaendelea kusimamia ujenzi wa nyumba hizo lakini niwahimize tu vilevile kwenye halmashauri wanapopata fedha zinazotoka Serikali kuu basi katika ile matumizi wajibane waweze kuweka na nyumba kiasi za watumishi wao katika maeneo wanapo pokea fedha zao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aloyce Kamamba, swali la nyongeza.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Kakonko na halmashauri yake ni mpya na hivi watumishi hawana nyumba za kuishi je lini Serikali sasa itajenga nyumba kwa ajili ya watumishi waliyoko katika Wilaya ya Kakonko? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kakonko na maeneo yote ambayo ni halmashauri mpya niwaombe kama nilivyosema kwenye swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Ushetu kwamba tutenge maeneo. Kwa sababu wakati mwingine mkienda kwenye maeneo hayo unakuta hakuna hata maeneo yaliyotengwa na halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za taasisi kama *National Housing* na *Watumishi Housing.*

Mheshimiwa Spika, hata hizi nyumba zilizopo bahati mbaya sana inatokea watumishi wengi hawaendi kukaa kwenye hizi nyumba na badala yake mashirika haya yamekuwa sasa yakipangishwa watu wa kawaida na hiyo ni mifano ipo hata hapa Dodoma tunazo nyumba nyingi pale Iyumbu lakini watumishi hawaendi pale kwa ajili ya kuzitumia. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 327

**Kuruhusu uraia pacha kwa Watanzania wenye uraia wa nchi nyingine**

**MHE. AGNESTA L. KAIZA** aliuliza: -

Je, Serikali ipo tayari kuruhusu uraia pacha kwa Watanzania wenye uraia wa nchi nyingine?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Masauni, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimwa Agnesta Lambert Kaiza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, uraia wa Tanzania unaongozwa na Sheria ya Uraia ya Tanzania Sura ya 357 Rejeo la mwaka 2002. Sheria hii inabainisha aina tatu za uraia wa Tanzania ambazo ni uraia wa kuzaliwa, uraia wa kurithi na uraia wa tajnisi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Uraia tajwa hapo juu, Serikali hairuhusu uraia pacha kwa watu wazima isipokuwa kwa watoto wenye umri chini ya miaka kumi na nane ambao wanakuwa na uraia wa Tanzania na uraia wa nchi nyingine.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, swali la nyongeza.

**MHE. AGNESTA. LAMBERT KAIZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa sheria zetu siyo amri ya Mungu na kwa kuwa ndani ya Bunge hili tumekwisha rekebisha sheria mbalimbali. Je, Serikali inapata kigugumizi gani kuleta Muswada wa Marekebisho ya Sheria hii ya Uraia Pacha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kwa kuwa Katiba yetu ya nchi inakataza ubaguzi wa aina yoyote ile. Je, Serikali haioni kuwa kama raia wake ambao wamepata urai nchi nyingine kwamba huu nao ni ubaguzi kwao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili kwa pamoja ya

nyongeza ya Mheshimiwa Agnesta Lambert, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli sheria siyo msahafu na sheria hizi zinatungwa kwa maslahi ya watu, lakini pia zinatungwa kwa matakwa ya watu. Bado Serikali haijajiridhisha kwamba uraia pacha ni takwa la wananchi walio wengi na ndiyo maana hata ukiangalia katika mchakato wa Katiba uliyokwama ambao ulihusisha maoni ya wananchi mbalimbali Serikali ilipendekeza hadhi maalum na siyo uraia pacha. Kwa sababu halikuwa takwa la wananchi waliyo wengi lakini ikitokezea haja hiyo Serikali italiangalia.

Mheshimiwa Spika, sheria hii na hili haina maana kwamba Serikali ina ubaguzi na ndiyo maana tupo katika hatua za mwisho mwisho kuanzisha utaratibu wa kuwa na hadhi maalum kwa ndugu zetu hawa ambao wananchi nje ambao utaweza kuwapa fursa mbalimbali, wataweza kupata fursa nyingi ambazo wenyewe wamependekeza kulingana na maoni waliyotoa. Kuna fursa kama kumi ambazo utaratibu huu utakapokamilika zitaweza kutolewa kwa ndugu zetu hawa Watanzania waliochukua uraia wa nchi nyingine.

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mwakamo, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa diplomasia ya kiuchumi inafanya watanzania wengi kwenda nchi mbalimbali duniani kutafuta mazingira ya kiuchumi na ili wasibaguliwe kule na wanataka kufaidika na huduma hiyo…

**SPIKA:** Mheshimiwa swali lako.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka wa kufanya marekebisho ya sheria hizo ili

watanzania hao waweze kufaidika na uchumi wa dunia? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika majibu yangu ya swali la msingi la Mheshimiwa Agnesta, kwamba Serikali imeona juu ya umuhimu wa waliokuwa watanzania hawa waliochukua uraia wa nchi nyingine kuweza kufaidika na fursa mbalimbali hapa nchini. Lakini siyo tu kwa wao kufaidika, hata kutoa michango yao katika uchumi wa nchi yetu na maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nimeeleza kwamba katika kuliona hilo tupo katika hatua za kuweza kuruhusu utaratibu wa hadhi maalum kwa raia hawa ambao wataweza kufaidika na mambo mbalimbali na wataweza kuchangia vilevile katika maendeleo ya nchi yetu. Miongoni mwa fursa hizo ni fursa tatu tu ambazo zitahitaji baadae marekebisho ya sheria na wakati huo utakapofika tutazileta, lakini fursa zingine zote hazihitaji mabadiliko ya kisheria na zitaweza kuruhusika kwa pale ambapo utaratibu huu utakapokuwa umekamilika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Oran Manase Njeza Mbunge wa Mbeya Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 328

### Hitaji la barabara ya mchepuko – Mlima Nyoka (Uyole – Uwanja wa Ndege wa Songwe)

**MHE. ORAN M. NJEZA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikalii itajenga barabara ya mchepuko ya Mlima Nyoka (Uyole) hadi Uwanja wa Ndege wa Songwe ili kuondoa msongamano na ajali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Mhandisi Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ipo kwenye maandalizi ya kujenga barabara ya Igawa – Songwe – Tunduma yenye urefu wa kilomita 218 pamoja na barabara ya mchepuo ya Mlima wa Nyoka pale Uyole hadi Uwanja wa Ndege wa Songwe (Uyole – Songwe *Bypass*) yenye urefu wa kilomita 48.9 kwa utaratibu wa *EPC+F*. Hadi sasa Mkandarasi amekwishapatikana na mkataba wa ujenzi utakuwa umesainiwa kabla ya mwisho wa mwezi Juni, 2023, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oran Njeza, swali la nyongeza.

**MHE. ORANA M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri haya ya Serikali. Lakini naomba nikupongeze wewe mwenyewe kwa jitihada hizi na sasa kweli maendeleo ya Mbeya na Mbeya imetulia. Swali langu la kwanza je, ni lini sasa wananchi waliyopisha hii barabara wataanza kulipwa fidia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Kuna barabara ya kiungo muhimu cha Mkoa wa Songwe pamoja na nchi jirani ya Malawi. Barabara ya Mbalizi – Shigamba ni lini Barabara ya Mbalizi – Shigamba itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba barabara hii itaanza kujengwa kwa *EPC+F* ili kupunguza msongamano katika Jiji la Mbeya. Hii inaenda sambamba na ujenzi wa barabara ya njia nne kilomita 29 Uyole hadi Ifisi ambayo tayari Mkandarasi yuko *site*. Sasa kuhusu fidia ni kwamba fidia itaanza kulipwa mara tutakapokuwa tumehakiki wale wananchi wote ambao walishaainishwa kwamba watalipwa kwa mpango wa sasa kwamba kabla atujaanza kujenga hiyo barabara tutahakikisha kwamba fidia inalipwa kwenye barabara hiyo ambayo wananchi watapisha ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala lake la pili Barabara ya Mbalizi – Shigamba ambayo inakwenda mpaka Itumba – Isongole mpakani na Malawi. Nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba sasa hivi tunakamilisha na anafahamu Mheshimiwa Mbunge tunakamilisha kufanya usanifu wa kina na tunategemea mwaka huu tutakamilisha na baada ya hapo sasa utaratibu ni kuijenga barabara hiyo yote kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Sillo Baran, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa ahsante, zabuni ya ujenzi wa kilometa nane za awali kwa Barabara ya Dareda – Dongobesh imetangazwa zaidi ya mara mbili. Je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo itaanza kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ni kweli tulishatangaza lakini tumeitangaza tena nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba barabara hii kilomita zote zilizotangazwa kilomita 8 tutaijenga katika kipindi hiki shida ilikuwa tu baada ya kutangaza hatukumpata mkandarasi sahihi. Kwa hiyo, mpango upo na tayari tumeishaitangaza upya na tuko kwenye mazungumzo na mkandarasi ambaye ataijenga. Kwa hiyo, tutakapokuwa tumeikamilisha hayo mazungumzo barabara hiyo itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Samweli Hhayuma Xaday.

Na. 329

**Ujenzi wa soko la samaki Kilwa Kivinje**

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA K.n.y. MHE ALLY M. KASSINGE** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga Soko la Samaki Kilwa Kivinje?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imefanya tathmini ya athari za mazingira na kijamii katika eneo la Kitongoji cha Miramba kilichopo Kilwa Kivinje kwa ajili ya kujenga miundombinu ya kuhifadhia mazao ya uvuvi ya chumba cha ubaridi, vichanja vya kukaushia dagaa na kuweka mtambo wa kuzalisha barafu na wa kukaushia dagaa kwa kutumia umeme.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi inayofadhiliwa na Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo *(IFAD)* itaweka miundombinu hiyo katika eneo hilo. Aidha, Serikali itaendelea na mpango wa kufanya tathmini ya athari ya mazingira na kijamii kwa ajili ya ujenzi wa soko la samaki katika eneo hilo kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Samweli Hhayuma Xaday, swali la nyongeza.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuambatana na Mheshimiwa Ally Kassinge kutembelea eneo la Kilwa Kivinje ili kujiridhisha na mahitaji ya soko hilo na kuharakisha ujenzi wake?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Ziwa Bassotu ukanda upande wa Kata ya Mulbadaw miundombinu ya msingi imeishajengwa ya mwalo. Je, yupo tayari kutoa tamko ili watendaji wake ndani ya Wilaya Hanang' wafungue Mwalo huo mara moja? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, niko tayari kuongozana na Mheshimiwa Mbunge mara baada ya Bunge hili kuhairishwa na ratiba yetu tutapanga kuanzia mwezi ya saba kwa hiyo hilo limekubalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tamko la ziwa niseme tu kwamba, nimelipokea jambo hilo na ninakwenda kulifanyia kazi na baada ya hapo tutatoa tamko rasmi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Katiba na Sheria Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Nyasa, sasa aulize swali lake.

Na. 330

**Ujenzi wa Mahakama ya Wilaya – Nyasa**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA** aliuliza: -

Je, lini Mahakama ya Wilaya ya Nyasa itaanza kujengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Pauline Gekul, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, nikushukuru, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Nyasa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kujenga Mahakama ya Wilaya ya Nyasa katika mwaka huu wa fedha

wa 2022/2023, ambapo taratibu zote za awali za kupitia michoro na makadirio ya gharama zimekamilika, na hatua za kupata mkandarasi wa ujenzi ipo katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Spika, Tunategemea muda wowote jengo hili litaanza kujengwa, na kukamilika katika mwaka ujao wa fedha wa 2023/2024.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Manyanya. Swali la nyongeza.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nashukuru kwa kuianzisha mahakama hiyo. Kwa kuwa Mahakama ya Wilaya ya Nyasa inatumia majengo ya watu binafsi ambao pia wanaweza kuvunja sheria na kutakiwa kushtakiwa katika Mahakama hii;

Je, Serikali haioni kuwa kwa kufanya hivyo inaweza kuwafanya wadau wengine kutokuwa na Imani na Mahakama katika kutoa haki?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Mahakama za mwanzo za Tingi na Litui ni chakavu sana.

Je, ni nini mpango wa Serikali katika kuboresha Mahakama hizi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru naomba sasa nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Stella kama alivyouliza. Swali lake la kwanza, anasema jengo hili la Mahakama ya Wilaya liko katika majengo ya watu binafsi, na anapata wasiwasi kama Mahakama inaweza ikatenda haki pale ambapo mtu huyu ambako tumepanga kwake ana jambo na Mahakama.

Mheshimiwa Spika, nikuhakikishie kwamba muhimili wetu wa Mahakama umeona jambo hili, ndiyo maana tumetenga fedha ili kuhakikisha mwaka huu wa fedha tunajenga Mahakama takribani 24 za Wilaya. Kwa hiyo sisi tutaipa kipaumbele Mahakama hii, na kwa kuwa kazi imeshaanza Mheshimiwa Manyanya awe na imani tu kwamba jengo hili litakamilika ili pasiwepo na wasiwasi wowote, japo Mahakama siku zote inatenda haki.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili amependa kufahamu, kwamba hizi Mahakama za kata ambazo zimetajwa zitajengwa lini na kwamba zimechakaa sana. Naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Mahakama yetu ya Tanzania imeliona jambo hili, na ndiyo maana katika mwaka huu wa fedha tumetenga ujenzi wa Mahakama 60 kote nchini. Mahakama inafanya tathmini kujua kata zipi zipo mbali, na mpango wa Mahakama ni kujenga Mahakama katika maeneo ya tarafa ili kuhakikisha kwamba tunatoa huduma. Na taratibu tutaendelea kufikia kama bajeti utaruhusu kwenye hizo kata ambazo uhitaji umeonekana. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jonas William Mbunda, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Serikali inaendelea kujenga majengo mapya katika maeneo mbalimbali.

Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama katika Wilaya ya Mbinga na Songea?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha nimesema kwamba tuna Mahakama 24 tumeziitenga kuzijenga na Wilaya yake ni miongozni mwa wilaya hizo mabazo tutajengea Mahakama. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Maji, Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, Mbunge wa Mbongwe sasa aulize swali lake.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Nicodemas Maganga

**SPIKA:** Subiri uitwe Mheshimiwa, unasimama kwanza nikikuona ndio nakupa nafasi. Kwa niaba ya Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, Mheshimiwa Zaytun Swai.

Na. 331

**Tatizo la maji – Jimbo la Mbogwe**

**MHE. ZAYTUN S. SWAI K.n.y. MHE. NICODEMAS H. MAGANGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatatua tatizo la ukosefu wa maji katika Jimbo la Mbogwe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nicodemus Henry Maganga Mbunge wa Jimbo la Mbogwe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji Wilayani Mbongwe ni wastani wa asilimia 55. Katika kupunguza kero ya maji kwa wananchi wa Wilaya hiyo, Serikali ina mipango ya muda mfupi na muda mrefu, ambapo Katika mpango wa muda mfupi Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya maji ya Iponya, Kagera, Kanegere na Lugunga-Luhala. Miradi hiyo imeanza kutoa huduma kwa wananchi. Vilevile, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali itachimba visima virefu 28 sambamba na kufanya upanuzi wa miradi ya maji ya Lulembela, Kagera, Kanegere na ujenzi wa miradi mipya ya maji katika vijiji vya Kisumo, Nyang'holongo, Ikobe, Ngemo, Bwendamwizo, Isebya, Ushirika, Mlale, Kadoke, na Mpakali. Kukamilika kwa Miradi hiyo kutaongeza huduma ya maji kufikia wastani wa asilimi 75.

Mheshimiwa Spika, mpango wa muda mrefu ni kutekeleza mradi mkubwa wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Wilaya ya Mbogwe ambapo usanifu wa mradi huo unaendelea na utakamilikaji katika mwaka wa fedha 2023/2024 na ujenzi kuanza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Naomba kuuliza;

Je, Serikali ina mikakati gani mahususi ya kutatua tatizo la maji lililoko sasa hivi katika Wilaya ya Longido?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaytun Swai, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, miradi ambayo iko Longido yote iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji, na lengo ni kuhakikisha tunakamilisha miradi hii kwa wakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shabani Shekilindi, swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, huu ni mwaka wa nane Serikali iliahidi kupeleka maji katika Kata za Makanya, Mlola, Kwai, Kwekanga hadi Kilole.

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake hii ya kupeleka maji katika maeneo hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shabani Shekilindi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwenye kata hizi zote alizozitaja Mheshimiwa Mbunge tuna miradi ambayo tunaielekeza katika mwaka wa fedha ujao. Lakini vilevile maeneo yote ambako miradi tulishaanza kuitekeleza tutakwenda kuikamilisha. Mheshimiwa Mbunge hili tumeshajadiliana muda mrefu na ameshafika ofisini mara nyingi. Naomba nimpe ahadi kwamba baada ya hapa kama tulivyokubaliana tutakwenda na tutahakikisha miradi ile tunaifanya vizuri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Nilete tangazo nililonalo hapa mbele. Kwanza tutaanza na wageni walioko Jukwaa la Spika.

Wapo wageni 11 wa Bunge ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Uchumi wa Taifa, Biashara na masuala ya Kazi kutoka Bunge la Zambia; yupo Mheshimiwa Mutotwe Kafwaya ambaye ni Kiongozi wa Msafara; Mheshimiwa Sefulo Sibeso (Mb), Mheshimiwa Sialubalo Simuunza (Mb), Mheshimiwa Mubika Mubika (Mb), Mheshimiwa Bindwell Mpundu (Mb), Mheshimiwa David Mabumba (Mb), Mheshimiwa Ronald Chitolela (Mb), Mheshimiwa Davies Chisopa (Mb), Mheshimiwa Njavwa Simutowe (Mb), Ndugu Charles Chisimba Afisa, Ndugu Emmanuel Bwalya, Afisa; karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Waziri wa Afya.

Waheshimiwa Wabunge mnaozungumza tafadhali tusikilizane.

Wapo wageni wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Waziri wa Afya; yupo Ndugu Hilda Nkabe, Mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa *Lukiza Autism Foundation* na muandaaji wa mbio ya *Run for Autism Tanzania,* karibu sana. *(Makofi)*

Sasa huyu ameambatana na mtoto wake ambaye ana usonji, *autism* ni usonji; mtoto wake anaitwa Lukiza Mutegeki Lwekama. Yupo pia na kaka wa huyu kijana ambaye ana usonji, yeye anaitwa Kami Lwekamwa, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia Ndugu Godfrey Kimathy, Mwenyekiti wa Chama cha Watoa Tiba kwa Vitendo Tanzania na *Program*

*Manager* wa *Afya Checkers Consultants,* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Christina Mwandamila ambaye ni Mkurugenzi wa Wauguzi kutoka Mloganzila, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Wilson Fungameza, Mshindi wa Tano wa Shindano la Wauguzi Bora kati ya washiriki 52,000 kutoka nchi 202, karibuni sana. *(Makofi)*

Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge, huyu ni muuguzi ambaye ametuwakilisha sisi Tanzania, kwamba amefanya vizuri na washindani walikuwa wengi, 52,000 kutoka nchi 202, Tanzania imekuwa ya tano kupitia yeye Ndugu Wilson Fungameza. Tunakupongeza sana kwa kazi nzuri unayoifanya na tunakutakia kila la kheri katika utendaji wako wa kazi. (*Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama tumeanza kupata tuzo kama hivi inaashiria kwamba Serikali yetu inajitahidi kwenye vifaa, kwa sababu mhudumu hawezi kutoa huduma vizuri kama hakuna vifaa kwa ajili ya kuwahudumia hao wananchi anaowahudumia. Kwa hiyo tunawapongeza sana Serikali, Mheshimiwa Waziri wa Afya lakini pia Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri mnayoifanya kwenye eneo la afya.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na wenye ulemavu amabye ni Katibu wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Kasulu Ndugu Abdallah Kazwika, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 14 wa Mheshimiwa Shabani Shekilindi, hawa ni Wenyeviti wa Chama cha Mapinduzi Wilayani Lushoto, Mkoani Tanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 22 wa Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya amabo ni wahitimu wenzake wa Mwanzi Sekondari iliyopo Manyoni Mkoa wa Singida, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni 11 wa Mheshimiwa Boniventure Kiswaga kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni sita wa Mheshimiwa Jacqueline Kainja ambao ni wanafunzi wa kutoka Chuo cha *St. John,* karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Joseph Mkundi kutoka Ukerewe, Mkoani Mwanza, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tunao wanafunzi 230 na walimu 12 kutoka Shule ya Awali na Msingi Moga ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana watoto wetu. *(Makofi)*

Sasa Waheshimiwa Wabunge nimepata vikaratasi hapa vingi vya Wabunge ambao mna watoto huko. Sasa kwa sababu ni vingi imeniwia kidogo ngumu kuvifanyia kazi vyote; lakini watoto wa Waheshimiwa Wabunge wanaosoma huko tunatambua uwepo wenu, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wanachama 13 wa Taasisi ya Wakulima inayoitwa *Young World Feeder* ya Jijini Dodoma, karibuni sana Bungeni Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hilo ndilo tangazo la wageni tulilo nalo asubuhi hii.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, Hoja ya Dharura.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga.

**HOJA YA DHARURA**

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nimesimama kwa Kanuni ya 54(1). Ninaweza nikasoma. Baada ya muda wa maswali kuisha Mbunge yoyote…

**SPIKA:** Endelea tu na hoja yako Mheshimiwa.

**MHE. FEDTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kuna jambo la dharura ambalo linaendelea Dar es Salaam, kwa maana ya Kariakoo, kwa siku ya leo, ambapo hivi ninavyozungumza hakuna biashara inayoendelea kwenye soko lile. Sisi kama nyumba ya Watanzania, kwa maana ya wawakilishi wa wananchi, Kariakoo imebeba majimbo mengi na Watanzania wengi wako pale wanafanya biashara. Na mimi kama Mbunge wa Jimbo la Makete zaidi ya asilimia 50 ya wafanyabiashara wa Kariakoo pia wanatoka Makete. Ninavyozungumza sasa hivi kuna mgomo ambao unaendela ambao umesababishwa na changamoto mbalimbali, mojawapo ikiwa ni kamata kamata za wafanyabiashara, sheria ya kikodi ya *EFD*, pia kuna changamoto nyingine ya usajili wa *storage*. Kwa hiyo kuna changamoto nyingi ambazo zinaendelea,

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu Kariakoo; nilisimama siku ile pia hapa nikazungumza, kwamba ndiyo Dubai yetu Tanzania. Dakika hizi ambazo zinazidi Kwenda na maduka yamefungwa, ni kwamba Serikali inazidi kukosa mapato. Siku ya leo ambapo tulitegemea mapato mengi yatakusanywa kwa leo Serikali haitaweza kupata mapato Kariakoo. Sasa kwa sababu ya udharura wake na upekee wake, Kariakoo inapotikisika na mikoa nayo inatikisika. Kwa sababu wafanyabiashara wengi wanaenda kuchukua bidhaa pale, na inawezekana kuna wafanyabiashara wengi pia wametoka nje ya nchi na wengine wamesafiri kutoka mikoani kwa siku ya leo kwenda pale Kariakoo kwa ajili ya kuchukua mizigo wanapata usumbufu.

Mheshimiwa Spika, sasa nimeona udharura wa jambo hili na haja ya Bunge kulijadili. Sasa nilikuwa naomba kutoa hoja ili shughuli za Bunge zihairishwe kwa muda ili Waheshimiwa Wabunge tuweze kujadili jambo hili jinsi gani Kariakoo tunaweza tukainusuru na wafanyabiashara wakaweza kuerejea kwenye shughuli zao na Serikali ikatoa kauli yake.

Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge naona mmesimama wakati sijampa nafasi ya yeye kutoa hoja. Waheshimiwa Wabunge ili hoja iweze kutolewa na Mbunge lazima mimi niwe nimejiridhisha halafu namrejeshea nafasi ili sasa atoe hoja. Kwa hiyo hayo aliotoa hapo ni maelezo ya awali ili mimi nijiridhishe je, hoja hiyo ni ya dharuara au Hapana.

Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Festo Sanga akitumia Kanuni ya 54, kwamba tuweze kuahirisha Bunge ili tujadili jambo ambalo ameliita jambo la dharura. Na ameeleza kuhusu Soko letu kubwa kabisa la Kariakoo, na kwamba shughuli za kibiashara hivi anavyozungumza hapo yeye haziendelei. Sasa mimi sijui kama haziendelei ama vipi kwa sababu nimekaa hapa mbele.

Sasa kwa sababu nimeyasikiliza maelezo yake na yeye ndiye aliyesema shughuli haziendelei Kariakoo, ngoja nipate kujua kama kauli kweli haziendelei Kariakoo. Namuona hapa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, ili kama shughuli haziendelei Kariakoo nitamrejeshea Mheshimiwa Sanga nafasi ili atoe hoja Bunge liweze kujadili.

Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii kulisema jambo hili. Kumekuwa na majadiliano ambayo yanaendelea kati ya Serikali na wafanyabiashara wetu ambao wako

Kariakoo kuhusu hoja zao mbalimbali ambazo wanatamani Serikali izifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi tunapoongea Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa pamoja na wataalam wetu kutoka Wizara ya Fedha, Wizara ya Viwanda na Biashara, wapo kwenye kikao na uongozi wa wafanyabiashara wa Kariakoo na yapo baadhi ya maeneo ndani ya Kariakoo ambayo shughuli zinaendelea na kuna wengine, kama ilivyo uhuru wa kila mtu kufanya kile anachokiona anatakiwa kukifanya, wengine wamefunga maduka yao na wengine maduka yanafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimempa nafasi ya kuzungumza Waziri ili anieleze, maana mimi niko hapa mbele kwa hivyo, sifahamu, lakini Mheshimiwa Waziri anasema Kariakoo si kwamba, shughuli zimesimama, shughuli zinaendelea. Maana yake ni baadhi tu ya watu ndio hawaendeshi shughuli zao ambapo mtu anaweza kuwa haendeshi shughuli yake kwa sababu, anaumwa ama ana jambo lingine.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waluzungumza bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, twende vizuri, tusikilizane. Sasa Kanuni yetu ya 55 inatueleza kwamba, 55(3) inatueleza, lakini pia (4) inasema; "Jambo lolote litahesabiwa kuwa ni lenye maslahi kwa umma iwapo utatuzi wake unategemea hatua zaidi kuliko zile za utekelezaji wa kawaida wa sheria peke yake."

Sasa kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri hapa amesema shuguli zinaendelea, lakini pia amesema kwamba, wapo wanaendelea na kikao, kwa maana ya viongozi,

jambo ambalo linaashiria kuna shida ndio maana mazungumzo yanafanyika kati ya viongozi hawa ambao amewataja kwa maana ya wenzetu wa mapato, lakini pia Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam. Ila kwa sababu, Mheshimiwa Waziri amesema wako kwenye kikao, ambayo inaashiria tayari kuna shida, tuwape nafasi, maadamu wako kwenye kikao muda huu tuwape nafasi halafu na mimi nitajiridhisha sasa kwamba, huko shughuli zinaendelea au hapana. Halafu kwa sababu, Bunge linaendelea tutapata nafasi ya kulitazama jambo hili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, kwenye hoja hii ya Mheshimiwa Sanga itakuwa bado iko hewani ikisubiri hayo ambayo nimeyasema hapa. Ahsante sana.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo tena. Mheshimiwa Musukuma.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Siko mbali sana na majibu ya Mheshimiwa Waziri aliyoyajibu, lakini nina kitu cha tofauti ambacho pia ni taharuki kinaendelea kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikimsikiliza sana Mheshimiwa Jesca akizungumzia suala la afya ya akili na Watanzania tuna utaratibu wa kufanya kazi ikifika *weekend* watu wanapata burudani, lakini tunavyoendelea hivi sasa kuna taharuki kubwa sana kwenye sehemu zetu za burudani, *weekend*. Ukianzia Mwanza, Dar es Salaam, *club* zote nzuri ambazo watu wanaenda ku-*refresh* akili zao, hata hapa Dodoma, zimefungwa.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka utupe Mwongozo wako kwa sababu, hili pia linaendana na Kariakoo ambalo limekaliwa na Mkuu wa Mkoa, lakini hili la sehemu za starehe ambazo zimefungwa kwa kigezo cha kuzidisha kelele, kitu ambacho si sahihi. Nipate Mwongozo wako na wao ni wafanyabiashara wanaingiza mapato makubwa sana kwenye Serikali.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Musukuma hapa kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 76, akiomba Mwongozo kuhusu jambo ambalo amelieleza yeye hapo. Sasa Kanuni yetu ya 76 inataka ueleze jambo ambalo limetokea hapa Bungeni na uwe unataka kujua kama linaruhusiwa ama haliruhusiwi. Kwa hiyo, kwa hoja aliyoileta Mheshimiwa Musukuma, hilo jambo haliko kwenye kanuni hiyo ya Mwongozo, lakini kama anataka kuleta hoja yake kwa kanuni nyingine, hiyo itakuwa sasa ni uchaguzi wake, lakini Kanuni ya 76 hakuna Mwongozo wowote unaoweza kutolewa hapo.

Waheshimiwa Wabunge…

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Huu utakuwa Mwongozo wa mwisho Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Hawa Mwaifunga.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Spika, nimesimama na mimi kwa Kanuni ya 76 ya kuomba Mwongozo wako kuhusiana na majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara juu ya suala zima la Kariakoo.

Mheshimiwa Spika, nimekubaliana na majibu yake, lakini kiufupi ni kwamba, mpaka sasa hayo maongezi anayoyasema baina ya wafanyabiashara na Serikali wamekubaliana mpaka Alhamisi ndio watakapopata majibu

sahihi na wafanyabishara wameamua kutofungua biashara zao mpaka wapate majibu sahihi kutoka Serikalini. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba uhakika zaidi wa Serikali, nini kinachoendelea?

Mheshimiwa Spika, Waziri anaposema kwamba, maduka yamefunguliwa Kariakoo, hakuna duka lolote lililofunguliwa Kariakoo, ukifungua duka Kariakoo wewe wamesema ni halali yao. Nazungumza hili kwa uhakika kwa sababu, kuna watu ambao wananihusu wako hapo Kariakoo na wananipa taarifa ya kinachoendelea Kariakoo. Kwa hiyo, tunaomba Serikali itoe kauli ili wafanyabiashara waendelee kufanya shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, hebu nisaidie kwa sababu, hapa tutakapokuwa tunajadili mwishoni maana yake Bunge litafanya maamuzi yatakayoelekezwa Serikalini. Ndio maana naiuliza Serikali, Soko la karaiakoo wafanyabiashara wako sokoni ama hawapo?

**WABUNGE FULANI:** Hawapo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Spika, hapana, naiuliza Serikali. Sasa mkijibu kwa namna hiyo, siwezi kuwasikiliza upande mmoja, lazima tunapofanya maamuzi kama Bunge tuwe na taarifa, Mheshimiwa Waziri, biashara Kariakoo inaendelea au haiendelei ama inasubiri mazungumzo ya leo?

**WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa fursa hii tena. Kama nilivyosema awali, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa akiongoza timu ya Serikali wako kwenye kikao na wafanyabiashara kwa ajili ya mgogoro huu unaoendelea ndani ya Kariakoo. Kama nilivyosema, wapo wafanyabiashara waliotumia uhuru wao kufungua maduka na wapo waliotumia uhuru wao kufunga

maduka, ni demokrasia, hakuna mtu anayelazimishwa kufanya jambo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali tunachokijua tuko kwenye majadiliano na wafanyabiashara na ndio jambo tulilonalo kwa sasa. Kama tuna taarifa nyingine tutaileta ndani ya Bunge lako tukufu.

**SPIKA:** Naona mwenye hoja amesimama. Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, juzi tulikuwa Ukumbi wa Mwalimu Nyerere kuzindua Tanzania ya Kidigitali. Sisi Wabunge tuko hapa tuna simu, tuna kila kitu, tuna *access* ya taarifa. Hatuwezi watu kama Bunge tukajidai hatuoni kinachoendelea Kariakoo na hatuna taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uhalisia *RC* wa Dar es Salaam ameenda Kariakoo, majadiliano yameshindikana. Alienda na lugha ya kwamba, wafanyabiashara waje Dar es Salaam wamuone Waziri Mkuu na wafanyabiashara wamekataa, kwa hiyo, hakuna duka lililofunguliwa Kariakoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi ni wawakilishi wa wananchi tusiishi hapa ndani kama tumejifungia, hatuoni kinachoendelea nje. Naomba ku… *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa. Waheshimiwa Wabunge kama nilivyokuwa nimesema mwanzo, ninyi ni kweli mnazo simu hapo, mimi sina. Ili niweze kuliongoza Bunge vizuri kwenye kufanya maamuzi lazima niwe na taarifa. Kwa sababu hiyo, nipeni muda wa kupata hizo taarifa, halafu nitamrejeshea Mheshimiwa Sanga, kama nilivyosema mwanzo.

Siwezi kuitoa hoja kwenu wakati mimi sina taarifa, kwa hiyo, nikishakuwa na hizo taarifa, watu wangu wanafuatilia kama Kariakoo biashara zinaendelea au hapana, lakini

jambo la dhahiri ni kwamba, kuna changamoto. Waziri amesema kuna kikao kuashiria kwamba, ipo changamoto na pia amesema kuhusu mgogoro maana yake kuna changamoto hapo; lakini sasa ili nijue, tunahitaji hatua za ziada au hizi za kawaida za Serikali zitasaidia basi lazima nipate taarifa. Kwa hiyo, nipeni muda nikishapata taarifa kama nilivyosema tangu mwanzo jambo hili nitalileta kwenu ili tuweze kulijadili kwa mujibu wa kanuni zetu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo kwa sababu, nilisema Mheshimiwa Hawa atakuwa wa mwisho kwa maana ya Miongozo, sasa tunaweza kuendelea.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea. Tunaanza na Mheshimiwa Profesa Patrick Aloyce Ndakidemi, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Paulina Daniel Nahato. Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea ajiandae.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na nianze moja kwamoja kwa kumpongeza sana Waziri wetu wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu kwa ripoti nzuri aliyowasilishwa. Ile ripoti ilikuwa imejaa kila kitu nami nimepata uelewa mkubwa sana wa vitu ambavyo Wizara ya Afya inafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudie kumpongeza Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Naibu wake Dkt. Godwin Mollel, Katibu Mkuu Dkt. Shekalaghe, Mganga Mkuu wa Serikali Dkt. Tumaini Nagu, Taasisi zote zilizopo chini ya Wizara ya Afya, Madaktari wote nchini na manesi na wafamasia kwa kazi nzuri wanayofanya. Kusema ukweli Udaktari ni kazi ya wito na hawa watu wanatutendea haki sana. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisitoke hapa bila kumpongeza Rais wetu, Rais wetu ameona umuhimu wa hii Sekta ya Afya na ametoa pesa za kutosha kabisa kusaidia Watanzania ili wapate huduma. Nampongeza Rais kwa sababu kwenye bajeti hii ambayo wanatuomba tuwapitishie, Mheshimiwa Rais ametenga shilingi 1,235,000,000,000 ikiwa ni nyongeza. Mwaka jana hii bajeti ilikuwa ni trilioni…

*(Hapa umeme ulikatika)*

*(Saa 4.40 asubuhi Bunge Lilisitishwa hadi Saa 10.00 Alasiri)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**15 MEI, 2023**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya Mwaka wa Fedha 2023/2024**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Kabla hatujaenda kwenye majadiliano, asubuhi kuna jambo ambalo lilijitokeza na lingine lilijitokeza wiki iliyopita. Sasa kwa namna Kanuni zetu zilivyo, ukisoma Kanuni ya 36 inayohusu mpangilio wa Shughuli za Bunge, ukisoma hapo Fasili ya Nne utagundua Shughuli za Serikali, ambayo ndiyo tunayo hapa mbele, lakini kuna mambo yanazitangulia, kwa hiyo yakiwepo hayo maana yake yanatangulia kabla shughuli hizo hazijaanza.

Waheshimiwa Wabunge, hapa tunalo jambo kwenye (h) na (i). Kwenye (h), hoja ya kuairisha shughuli ili kujadili mambo muhimu ya dharura, kuna hoja hapa ilijitokeza asubuhi kwa hivyo nitatoa maelezo. Pia kwenye Kauli za Mawaziri, kuna Kauli ya Waziri ambayo nimeletewa hapa, halafu ndiyo tuendelee na hii shughuli iliyo mbele yetu.

Waheshimiwa Wabunge, hii sasa ngoja nisimame kabisa.

Waheshimiwa Wabunge, asubuhi alisimama Mheshimiwa Festo Sanga kwa hoja ya dharura kupitia Kanuni ya 54 kuhusu jambo ambalo alilieleza la mgomo wa wafanyabiashara kule Kariakoo. Waziri akapewa nafasi ya kutoa maelezo kuhusu jambo hilo akatoa maelezo na sote tulimsikia, sina haja ya kuyarejea hayo. Sasa kwa sababu wakati tukiahirisha Bunge niliahirisha kwa ajili ya sababu nyingine lakini inabidi tuanze na haya kwa sababu nilisema nikishajiridhisha.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, baada ya kutoka sasa hapa Bungeni nikapata taarifa za ziada kwamba ni kweli Kariakoo kuna changamoto na kuna mgomo wa wafanyabiashara na baada ya kuzipata taarifa hizo za mgomo wa wafanyabiashara, wakati huo huo pia nimeletewa taarifa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba alikutana na viongozi wa wafanyabiashara wa Kariakoo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kukutana na Viongozi majira haya ninayozungumza na ninyi sasa kwa sababu ninyi mna simu mtakuwa mnafuatilia zaidi huko Mheshimiwa Waziri Mkuu anaelekea Kariakoo kwenda kuzungumza na wafanyabiashara. *(Makofi)*

Katika mazingira hayo sitaweza kuitoa hoja ili Waheshimiwa Wabunge tuweze kufuata utaratibu wa Kanuni yetu ya 54 isipokuwa nitatoa nafasi kwa Serikali kwa maana ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu taarifa amenipa, kwamba anaelekea Kariakoo muda huu kuzungumza na wafanyabiashara, basi tutoe fursa kwa Serikali kufanya kazi yake kwa namna ambavyo Kanuni ya 55 inatuongoza. Kwa sasa tutumie njia hizo ambazo Serikali inazichukua, halafu kama hizo hazikuzaa matunda na tunaamini zitazaa matunda, kama hazikuzaa matunda tutajua jambo hilo linahitaji kazi ya ziada na hivyo Bunge tutafanya kazi yetu ya kuishauri Serikali.*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo sasa nitamuita Mheshimiwa Waziri yule ambaye ana kauli ya Serikali baada ya kuketi.

Waheshimiwa Wabunge, wiki iliyopita, Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelekezo hapa kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii ielekee Mbarali kwa hoja iliyokuwa imetolewa na Mheshimiwa Francis Mtega kuhusu madhara

waliyoyapata wananchi kule Mbarali. Sasa nitampa fursa ya kutoa hiyo kauli ya Serikali halafu tutaendelea na ratiba yetu.

Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Waziri wa Maliasili na Utalii.

## KAULI ZA MAWAZIRI

### Kauli ya Serikali kuhusu tukio la wananchi watano kujeruhiwa na Askari wa *TANAPA* katika Hifadhi ya Taifa Ruaha, Wilayani Mbarali, Mkoa wa Mbeya

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 56 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kutumia fursa hii kutoa taarifa fupi ya Serikali kuhusu tukio la wananchi Watano katika Wilaya ya Mbarali, Mkoani Mbeya kujeruhiwa na Askari wa *TANAPA* tarehe 6 Mei, 2023.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa, mnamo tarehe 11 Mei, 2023 baada ya kipindi cha maswali na majibu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu Bungeni, Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, Mbunge wa Mbarali, aliomba Mwongozo kwa Mheshimiwa Spika akiomba Bunge liahirishe mjadala ili kujadili suala la dharura la wananchi watano katika Jimbo lake kujeruhiwa na Askari wa *TANAPA*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge alieleza kuwa Askari wa *TANAPA* walifika na helikopta katika Kijiji cha Mwanavala na kuvamia wananchi, kuwapiga na kupora mifugo 250. Aidha, Mheshimiwa Mbunge alilieleza Bunge kuwa mwananchi ambaye mifugo yake waliporwa ameathirika kisaikolojia na anataka kujinyonga na kwamba ndugu, jamaa na marafiki wanafanya kazi ya kumlinda ili asijinyonge.

Mheshimiwa Spika, kufuatia hali hiyo Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitoa maelekezo kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kwenda Mkoani Mbeya kuonana na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya na Kamati yake ya Ulinzi na Usalama na ile ya Wilaya ya Mbarali ili kupata undani wa suala hilo kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, siku hiyo, tarehe 11 Mei, 2023 niliambatana na Naibu Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori na Kamishna wa Uhifadhi wa *TANAPA* kwenda Mkoani Mbeya. Tarehe 12 Mei, 2023 asubuhi nilikutana na kufanya Kikao na Mheshimiwa Juma Zuberi Homera, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, Kanali Denis Mwila, Mkuu wa Wilaya ya Mbarali na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Mbarali na Viongozi wa Chama cha Mapinduzi (Chama Tawala) Wilaya ya Mbarali wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mbarali, Ndugu Mary Mbwilo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kikao hicho, Wajumbe wote tuliambatana kwenda Wilayani Mbarali ambapo nilianzia katika Ofisi za Chama cha Mapinduzi na nilifanya kikao na viongozi wote niliowakuta ambao ni Mwenyeki wa Wilaya, Katibu wa Wilaya, Makatibu wote wa Kata wa Chama cha Mapinduzi na baadae kuelekea eneo la tukio katika Kijiji cha Mwanavala.

Mheshimiwa Spika, umbali wa kutoka Kijiji cha Mwanavala mpaka eneo tukio lilipotokea ni takribani kilometa 20. Kwa mipaka ya awali na ya sasa, maeneo haya yapo chini ya Hifadhi ya *TANAPA* na katika maeneo yote haya zipo *beacons* (vigingi) kubwa za *TANAPA* zilizowekwa na zinaonekana wazi.

Mheshimiwa Spika, tukiwa eneo la tukio tulifanya mazungumzo na baadhi ya wananchi akiwemo mwananchi

ambaye Mheshimiwa Mbunge alieleza hapa mbele ya Bunge lako tukufu kuwa mifugo wake ng'ombe 250 walikuwa wameporwa na mbuzi wawili wameuwawa. Baada ya hapo tulifanya mkutano wa hadhara na wananchi, kwanza kuwapa pole kwa tukio lililoteka na vilevile kupata uelewa wa pamoja kuhusiana na tukio hilo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kikao tulichofanya na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa pamoja na Wilaya, kutembela eneo la tukio na baadae kufanya mkutano wa hadhara wa wananchi wa eneo husika ambao walishiriki kwa wingi wakiwemo waathirika na baadhi ya ndugu zao, pamoja na Madiwani akiwemo Diwani wa Kata husika, Mheshimiwa Chuki Jeremiah Mbanjine, Mheshimiwa Michael Jeremia Makao, Diwani wa Kata ya Rujewa na Mheshimiwa Udes Nasoro Selemani, Diwani wa Kata ya Igawa, pamoja na viongozi wa Chama Tawala (CCM).

Mheshimiwa Spika, kutokana na vikao, mikutano na ziara hiyo, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa yafuatayo yalibaininika: -

(i) Ni kweli kuwa mnamo Tarehe 06 Mei, 2023 Askari wa *TANAPA* wakiwa katika doria za kawaida walifika katika Kijiji cha Mwanavala na helikopta katika maeneo yaliyopo ndani ya Hifadhi ya Ruaha ambapo ni sawasawa na kilometa 20 ndani ya Hifadhi ya *TANAPA* kutoka ulipo mpaka wa awali. Eneo hilo ni katika maeneo ambayo wananchi hawaruhusiwi kuingia kwa kuwa ni karibu na Mto Ruaha ambao ni sehemu ya chanzo cha kupeleka maji katika Bwawa la Mwalimu Nyerere. Askari husika wakiwa katika doria za kawaida walibaini ujenzi wa maboma mawili mapya ya mifugo ndani ya Hifadhi ya Ruaha kinyume cha sheria;

(ii) Katika harakati za kutaka kuwakamata watuhumiwa, wananchi hawa, waliongia kijinai na kinyume cha sheria katika eneo la Hifadhi walizuia kutiwa nguvuni kwa

kurusha mawe, fimbo, mishale na silaha nyingine za jadi na kusakizia mbwa Askari wa Jeshi la Uhifadhi kwa lengo la kuwadhuru Askari hao. Aidha, miongoni mwa silaha za jadi zilizorushwa zilitishia usalama wa Askari wa Jeshi la Uhifadhi waliokuwa katika kazi yao halali ya uhifadhi na kupelekea kitako cha bunduki aliyokuwa nayo Askari hao kuvunjika. Nguvu waliyotumia Askari kujilinda ilipelekea majeraha kwa wananchi hao na Askari Jeshi kulazimika kuwadhuru mbwa waliowasakizia kwa hofu ya kulinda maisha yao.

(iii) Baada ya mivutano hiyo, wananchi wote waliopata majeraha walipelekwa hospitali na walipatiwa matibabu ambayo yaligharamiwa na *TANAPA* na wanaendelea na shughuli zao kama kawaida. Pamoja na kwamba tukio husika limetokea ndani ya hifadhi, Wizara iliona ni busara kutoa pole ya shilingi milioni moja kwa kila mwananchi aliyeathirika na tukio hilo.

(iv) Mheshimiwa Spika, ikumbukwe mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa eneo lilipotokea tukio hili ni karibu na eneo yalipotokea mauaji ya Askari wa Uhifadhi Ndugu Yusti Matei mwenye umri wa miaka 25, na Askari waWanyamapori wa Vijiji Ndugu Isaya Mwambe, miaka michache iliyopita kwa kushambuliwa na wananchi waliovamia hifadhi kwa silaha za jadi. Takwimu za Wizara zinaonesha kwamba Askari wa Jeshi la Uhifadhi 15 wameuwa na wengine 51 wamejeruhiwa na wananchi wavamizi ndani ya hifadhi mbalimbali nchini wakiwa wanatekeleza majukumu yao.

(v) Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa hakuna uthibitisho wa vitendo vya wanawake kuvuliwa nguo na Askari wa Uhifadhi kama ilivyoelezwa hapa Bungeni na Mheshimiwa Mbunge.

(vi) Mheshimiwa Spika, naomba kulithibitishia Bunge lako tukufu kwamba Hakuna mwananchi yeyote aliyenyanyaswa kijinsia, lakini pia hakuna mifugo yoyote ya

mwananchi yeyote (ng'ombe 250) walioporwa na hakuna mbuzi yeyote aliyeuawa kwa kupigwa risasi. Hakuna taarifa ya mtu yeyote kutaka kujinyonga kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Mbunge katika Bunge lako hili Tukufu; na

(vii) Mheshimiwa spika, askari wote waliohusika na tukio hilo waliandikishwa maelezo Polisi kufuatia maelekezo ya Serikali na maelekezo yangu.

Mheshimiwa Spika, kufuatia tukio liliojitokeza Wilayani Mbarali napenda kusisitiza maelekezo yangu niliyoyatoa Wilayani Mbarali kama ifutavyo: -

(1) Askari wote wa uhifadhi nchini watumie weledi wao katika kudhibiti uvamizi kwenye hifadhi badala ya kutumia nguvu kupita kiasi katika utekelezaji wa himasheria. Hii ni pamoja na kuwakamata na kuwafikisha watuhumiwa kwenye vyombo vya sheria ili sheria ichukue mkondo wake;

(2) Tukio la Mbarali limetokea ndani ya hifadhi, takriban kilometa 10 baada ya mpaka mpya wa hifadhi na kilometa 20 ndani ya mpaka wa zamani karibu kabisa na Mto Ruaha ambao ndiyo mto tegemezi unaozalisha maji yanayotegemewa katika Bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo Serikali, kupitia kodi za wananchi, inatumia zaidi ya trilioni 6.5 kulijenga, lakini pia ndiyo mto tegemezi wa maji ya kunywa na ndiyo chanzo cha maji katika mito mbalimbali nchini. Hii inadhihirisha kwamba wananchi hao waliingia ndani ya hifadhi kimakosa, bila kufuata taratibu za kisheria. Eneo hili halina ruhusa ya kulima wala kufuga, wala mapito ya wananchi na hii ni kwa kuzingatia hali halisi ya uwandani kama nilivyoeleza hapo juu sambamba na kulinda maeneo oevu ili mito iweze kurejesha mikondo yake ya asili ya mitiririko yake ya maji kama nilivyoeleza.

(3) Mheshimiwa Spika, nimewasihi sana wananchi na ninaomba uniruhusu niendelee kuwasihi wananchi kufuata

sheria na taratibu zote za maeneo yaliyohifadhiwa kisheria kwa maslahi mapana ya Watanzania wote kwa ujumla wa vizazi vya leo na vizazi vya kesho. Naomba niendelee kuwasihi Waheshimiwa Wabunge mtusaidie, tusaidiane katika kutoa elimu kuhusu umuhimu wa maeneo haya yaliyohifadhiwa.

(4) Wahifadhi wote nchini wawashirikishe viongozi wa Chama na Serikali katika kutatua migogoro kati ya wananchi na maeneo ya hifadhi ikiwemo kutoa elimu ya uhifadhi kwa wananchi wanaozunguka maeneo hayo, lakini watambue kwamba wananchi ni wahifadhi namba moja hivyo waboreshe mahusiano baina yao na wahifadhi, wananchi na kila kiongozi wa uhifadhi katika eneo lake atapimwa kwa namna anavyoshirikiana na wananchi katika maeneo yao. Hivyo wakaimarishe mahusiano yao na wananchi na vijiji vinavyopakana na hifadhi.

(5) Wahifadhi wote nchini waendelee kuimarisha doria, kuweka alama za mipaka, kuweka mabango na kulima mkuza ili kudhibiti uvamizi katika maeneo ya hifadhi kwa mustakabali wa nchi yetu ikiwemo kuhakikisha upatikanaji wa maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu, mifugo, kufua umeme na kilimo, hususan programu za umwagiliaji.

(6) Mheshimiwa Spika, ninaiagiza *TANAPA* kuanza ujenzi wa *Rangers Post* (Kituo cha Askari wa Uhifadhi) ili kuimarisha ulinzi katika eneo la Hifadhi ya Ruaha.

Mheshimiwa Spika, katika kupata suluhisho la kudumu la migogoro katika hifadhi hii kongwe iliyoanzishwa mwaka 1910 iliyojulikana wakati huo kwa jina la Hifadhi ya Saba, mwaka 1946 ilibadilishwa jina na kuitwa Rungwa na mwaka 1964 Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wetu wa Awamu ya Kwanza aliporidhia Hifadhi hii iitwe Hifadhi ya Ruaha, Serikali inakusudia kumega eneo la hifadhi lenye ukubwa wa takribani hekta 34,000 ili zitumike kwa shughuli za maendeleo

ya wananchi ambapo wananchi wa vijiji husika watajipangia mpango bora wa matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, aidha Serikali itaondoa ekari 900 ili zitumike kwa shughuli za malisho. Wiki hii Serikali itakamilisha uthamini wa mali za wananchi katika baadhi ya maeneo ya Kijiji cha Mwanavala ili taratibu zingine za fidia ziendelee. Vilevile napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa Serikali imekamilisha uwekaji wa vigingi katika mpaka mpya wa Hifadhi ya Ruaha.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakamilisha mchakato wa kuandaa rasimu ya Tangazo la Serikali *(Government Notice)* jipya la Hifadhi ya Taifa Ruaha na mara taratibu husika zitakapokamilika Serikali itawasilisha Azimio Bungeni ili kupata ridhaa ya Bunge lako tukufu kama ilivyo kwa mujibu wa sheria na hatimaye kuwasilishwa *GN* husika kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hatua stahiki.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, hiyo ndiyo kauli ya Serikali. Kwa mujibu wa Kanuni zetu kauli ya Serikali haina mjadala. Pamoja na taarifa hiyo Mheshimiwa Waziri, nitaomba nakala umpatie Mbunge ili aweze kufuatilia kwa karibu yale mambo ambayo yeye akiwa huku Bungeni aliletewa na wananchi wake. Kwa hivyo, ni jambo jema kwamba Serikali imeweza kuchukua hizo hatua mbalimbali na nadhani mnaweza kumpa hiyo taarifa Mbunge ili na yeye ajue namna ya kufuatilia kwa wananchi wake.

Waheshimiwa Wabunge, Katibu alikua ameshatusomea jambo ambalo tunaendelea nalo sasa, asubuhi tulikua tumemtaja Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi na ndiyo inabidi aanze sasa mchango wake, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Paulina Daniel Nahato, Mhe. Dkt. Alfred James Kimea ajiandae.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa, na ninaomba niendelee pale nilipoachia.

Mheshimiwa Spika, kwa pesa ambazo Serikali imetoa katika Wizara hii ya Afya, tumeona Wizara imefanya mambo mengi makubwa ambayo ni faraja kwa Watanzania wote. Kuna huduma za kinga ambapo tunapata chanjo za pepopunda, kifaduro, kupooza, surua mpaka UVIKO. Kuna huduma za lishe, huduma za usafi wa afya na mazingira, huduma za afya mipakani kwa wasafiri wanaoingia Tanzania kuzuia ujio wa magonjwa mapya na huduma za kibingwa ambazo zimefanywa na vijana wetu wa Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri, juzi niliguswa hasa nilipomwona yule mtoto aliyekuwa na Selimundu mkamleta hapa, mkatuambia dada yake, Esther, ndiye aliyetoa uroto akamsaidia kaka yake, na yule mtoto amepona, Waziri na wataalam wetu, tunawapa *big up,* hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, hawa mabingwa wetu wa figo, wa kupasua ubongo bila kupasua fuvu, moyo na Selimundu tuendelee kuwapa nguvu ili waendelee kuwahudumia Watanzania. Chonde chonde, najua mmeshaanza, lakini tuongeze nguvu zaidi, kwa sababu ukienda kwenye Kliniki za Selimundu, utaona ule huruma vile vitoto vinavyoteseka. Kama tiba tayari imeshapatikana, naomba sana tuendelee kuwapa nguvu Wizara ili watekeleze hilo.

Mheshimiwa Spika, niongee kwa kifupi kuhusu Hospitali ya *KCMC,* ni hospitali bingwa inayofanya vitu vingi. Pale kuna uhaba wa madaktari na watumishi wengine. Wana-*operate at fifty percent capacity.* Kwa hiyo, naomba mwaongezee watumishi ili waendelee kutoa huduma kwa Watanzania ambao wanaopelekwa pale kupata tiba.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie masuala machache kwenye jimbo langu kabla sijachangia kitu ambacho nilitaka kusema. Naishukuru Serikali, imetujengea Hospitali ya Wilaya pale Mabogini. Ni eneo ambalo lina watu wengi, karibu *20.3 percent* ya wakazi wa jimbo langu wametoka pale. Kwa hiyo, tunashukuru sana, hospitali ile imekamilika. Naendelea kuomba Wizara itupelekee vifaa, dawa na vitu vingine ili wananchi waanze kupata huduma. Katika Hospitali ya Kibosho, nilikuwa nimemwomba Waziri anipatie *digital x-ray,* bado wanangojea kule *Kibosho Hospital.* Chonde chonde, dada yangu Mheshimiwa Ummy, hii ni ahadi, wananchi wanaingojea, mwendelee kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa leo utajikita kwenye changamoto ya watu wenye ulemavu na wanaohitaji viungo bandia. Hapa Tanzania kuna wenzetu wengi ambao wana ulemavu na wanahitaji viungo bandia kwenye miguu na mikono. Kinachosababisha hao watu wawe na ulemavu ni nyingi. Kwanza, wanaweza wakawa wamezaliwa hivyo; ya pili, wanaweza kuwa wamepata ajali; wengine wameugua saratani na kisukari wakaishia kukatwa mikono na miguu; na sasa hivi hali ilivyo, vijana wetu wa bodaboda wamejiajiri kule, wanaendesha boda boda na bahati mbaya tunawagonga, yeye na abiria wanaishia kukatwa mguu au mkono.

Mheshimiwa Spika, sasa idadi ya hawa wagonjwa imekuwa kubwa na ninaomba Serikali iangalie kwa jicho la pekee kwa sababu hili kundi hatujaliangalia vizuri. Linahitaji viungo bandia na hawa watu wanahitaji warudie maisha yao ya zamani ili waweze kuchangia kwenye uchumi wa Taifa, lakini kwa kuwa hakuna hivi viungo, basi wanakuwa na mateso makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini watu wachache ndio wamepata hii huduma? Ni kwamba, kwanza kabisa hospitali zilizopo zinazotoa huduma ya viungo bandia ni chache hapa

nchini. Kwa haraka haraka ninajua kuna *KCMC,* kuna Bugando *Hospital*, kuna *MOI* na *Dodoma General Hospital.* Hiyo ni sababu ya kwanza. Kwa hiyo, tunaomba huduma hii isambae kwenye hospitali za mikoa ili watu watibiwe kwenye hospitali zao za mikoa huko huko.

Mheshimiwa Spika, sababu ya pili ni gharama za viungo kuwa ni kubwa sana. Viungo bandia, kumwekea mtu mguu, kwa utafiti nilioufanya mimi ni kati ya shilingi milioni 1.5 mpaka shilingi milioni 3.5; na mkono ni kati ya shilingi milioni mbili mpaka shilingi milioni 4.5. Sasa kwa Mtanzania wa kawaida, hao wenye saratani waliokatwa mikono na miguu, ni wazee ambao hawajiwezi kabisa. Kwa Mtanzania wa kawaida, hii gharama ni kubwa sana. Naomba Serikali iwaangalie hawa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kingine kikubwa ni kwamba Mfuko wetu wa Taifa wa Bima ya Afya, mfuko wetu pendwa, hautoi huduma kwa viungo bandia. Yaani wewe ukiugua, kama ukikatwa mguu, unatakiwa ujilipie mwenyewe. Namwomba Waziri atakapo kuja ku-*wind-up* hapa atusaidie kwa sababu kuna watu wanateseka huko, ni wengi kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, sasa nitoe ushauri kwa Serikali kwamba, chonde chonde, ijumuishe viungo bandia kwenye Mfuko wa Taifa wa Bima yetu ya Afya. Watu wanapopata ajali akikatwa mguu, kama anahitaji kiungo bandia, basi iwe kwenye huduma ambazo zinaweza zikatolewa na Mfuko wa Taifa wa Bima yetu ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu cha pili, naishauri Serikali, ikiwezekana tufanye utafiti. Kuna watu wengi sana wako huko ambao, akishaenda hospitali akiambiwa gharama ni kubwa, anarudi nyumbani kwenda kufa peke yake tu. Tufanye utafiti, tupate kanzidata ya wagonjwa ni wangapi ambao wana hili tatizo ili tuweze kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu wa tatu kwa Serikali ni kwamba Vyuo vyetu Vikuu vya Afya ambavyo vipo vingi, vimetapakaa nchi nzima, vifundishe wataalam wa hii fani ili waweze kuwahudumia Watanzania wenzao ambao wana hili tatizo. Kama nilivyosema awali, napendekeza pia hii huduma isiishie kwenye zile hospiatli nne tu ambazo zipo sasa hivi, iende kwenye hospitali zote za mkoa. Kila mkoa uwe na kitengo ambacho kitakuwa kinasaidia hawa wagonjwa ambao wana hili tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu mwingine kwa Serikali, ikiwezekana ihamasishe wadau wa maendeleo au Serikali yenyewe, kila mahali penye hii huduma pawe na *Unit* ya kutengeneza hivi viungo bandia ili watu waweze kupata huduma hapo kwa hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu wa mwisho ni kwamba, wahitimu ambao wameshahitimu hapa nchini, tunao ambao wamesoma *KCMC,* Serikali iwape ajira na iwapeleke huko mikoani ili waweze kutoa huduma kwa watu ambao wana hili tatizo la viungo bandia.

Mheshimiwa Spika, kingine muhimu, elimu itolewe kwa watu ambao wameshapata hili tatizo kwamba ukikatika mkono au mguu siyo mwisho wa maisha. Unaweza ukavaa kiungo bandia ukaendelea na shughuli zako kama ilivyokuwa awali. Ikiwapendeza, mbadilishe sera itakayotoa umuhimu wa kutatua tatizo hili katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa niseme kwamba wagonjwa wengi ambao wana hili tatizo la kukatwa miguu na mikono, hukwazika kwa kiwango kikubwa cha gharama ambazo nimezitaja hapa. Naiomba Serikali, chonde chonde, tuangalie namna ya kuweka kwenye mifumo yetu ili ndugu zetu ambao wamepata haya matatizo waweze kuhudumia na Serikali yao pendwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Paulina Daniel Nahato, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea na Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, ajiandae.

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi nami nichangie katika Wizara hii ya Afya. Awali ya yote, napenda kumshukuru Mungu kwa kunijalia afya na kusimama leo na kuweza kuchangia katika Wizara.

Mheshimiwa Spika, pia naomba kumshukuru Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ya kujali afya ya wananchi wote na hivyo kuipatia Serikali fedha nyingi sana ili huduma ya afya iweze kuboreshwa kuanzia katika ngazi ya vijiji mpaka ngazi ya juu. Napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Waziri na kumshukuru sana Mheshimiwa Ummy Mwalimu kwa kazi nzuri anayoifanya. Kwa kweli ni mchapakazi, pamoja na Naibu wake, timu yote na Madaktari wote Tanzania kwa kazi nzuri wanayoifanya. Nawapongezeni sana, kwani hii kazi ni nzuri, ni kazi ambayo ni ya muhimu kwa sababu bila afya kwa wananchi, maendeleo hayawezi kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeipitia hii bajeti na kwa kweli inatia moyo sana, na kwa kweli tumepiga hatua na tunaenda sehemu nzuri. Naomba nichangie kwanza kwa kuipongeza sana Wizara ya Afya kwa mambo matatu ambayo wameyaleta na wanakwenda kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, nawapongeza kwa kuja na mpango wa uzalishaji, uratibu na kuwatumia wahudumu wa afya katika ngazi ya jamii *(Integrated and Coordinated Community Health Workers Programme)*. Hii ni muhimu sana, na kwa kweli italeta mafanikio makubwa sana

katika Wizara ya Afya na afya kwa ujumla. Kwa sababu katika ngazi ya familia ndipo walipo watu wengi, hawajulikani na hawaendi kupata matibabu wanapoumwa. Kwa hiyo, hii programu italeta mafanikio makubwa kwa sababu hao watakaokuwa *trained* watakuwa kule katika ngazi ya chini katika vijiji, na watakuwa wanawafahamu watu na tamaduni na hata lugha mbalimbali za watu, na hivyo hii programu itasaidia sana kupunguza gharama au mzigo mkubwa kwa Serikali katika kuleta tiba katika hospitali zetu kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa pika, kwa hiyo, kwa hilo naipongeza sana Wizara ya Afya kwa kuja na mpango huu. Nina hakika, hata nchi ya Rwanda ambayo Bunge liliwahi kunituma kuwakilisha, waliona hilo kwamba lilikuwa ni jambo lililokuwa na mafanikio. Naipongeza sana Wizara kwa kuliona hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, naipongeza sana Wizara kwa kuanzisha programu ya kuwa na *Bachelor of Science Psychology* katika Vyuo Vikuu nchini, kwa kuanzia na Chuo Kikuu cha *MUHAS*. Tatizo la afya ya akili limeongelewa mno na hata Mheshimiwa Ummy Mwalimu inaonekana sasa hivi anaijua vizuri hii changamoto ya afya ya akili. Afya ya akili ni chanzo cha matatizo ya magonjwa mengi. Hivyo basi, programu hii inapoanza itaenda kutoa suluhisho la matatizo mengi ya magonjwa ambayo yanaambatana na magonjwa ya akili. Kwa hiyo, naipongeza Serikali.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, naipongeza Serikali kwa kuipandisha hadhi Hospitali ya Mirembe kutoka katika jina hili na kuifanya kuwa Taasisi ya Taifa ya Afya ya Akili. Hili jina "Mirembe" kwa kweli lilikuwa linaleta unyanyapaa *(stigma)*. Neno "Mirembe" hata mtu wa kawaida akiambiwa, anaonekana kama ni kichaa. Kwa hiyo, sasa hivi Wizara kwa kuliona hilo, na kubadilisha hospitali hii na kuipa hadhi, itaonekana ni seheme ya kawaida kabisa kama hospitali nyingine zozote nchini. Kwa hili nawapongeza sana, sana, sana Wizara ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie mambo manne kwa Wizara yetu ya Afya. Jambo la kwanza, niwaombe kama nilivyowahi kuchangia, kuwekeza zaidi kwenye kuzuia magonjwa yasiyo ya kuambukiza *(Non-Communicable Diseases)*. Naomba sana hili suala tuliangalie. Magonjwa mengi ambayo siyo ya kuambukiza, yanaleta changamoto. Gharama za kutibu magonjwa haya ni ghali na kwa kweli yana-*consume* fedha nyingi sana. Kwa hiyo, kama tutawekeza uzito katika kuzuia magonjwa haya yasiyo ya kuambukiza, hakika mambo yatakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, ninaishauri Serikali au Wizara kupanua wigo wa huduma ya vipimo *(Diagnostic Services)* katika jamii zetu. Kwa sababu kuna magonjwa mengi ambapo yanapogunduliwa mapema, kwa mfano kansa, inatibika, lakini mara nyingi wagonjwa wanakuja hospitali wakiwa tayari wako katika *stage* nyingine. Kwa hiyo, tuboreshe pia hizi huduma za kugundua magonjwa yanapokuwa katika *stage* ya awali kabisa.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, naomba kuishauri Serikali, kutokana na mabadiliko ya mara kwa mara ya teknolojia ya afya, Wizara itenge fedha kwa ajili ya elimu endelevu kwa watumishi wa Wizara ya Afya. Mambo yanabadilika kila siku, kwa hiyo, *in service training, workshop* pamoja na kozi fupi fupi kwa wafanyakazi wa afya au watoa huduma wa afya itawasaidia kuwafanya watoe huduma iliyo bora zaidi, inayoendana na teknolojia na mabadiliko yanayotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la nne, naendelea kuishauri Serikali kwa kutoa motisha kwa wafanyakazi wanaofanya kazi vijijini. Watoa huduma wa afya wanapopelekwa vijijini wanaanza kufikiria maisha ya kijijini, kwa hiyo, wanakata tamaa, wanatamani kupangwa mijini. Naiomba Serikali tu iweze kutoa motisha; itoe *incentives* ili daktari au mtoa huduma anapopelekwa kijijini afurahie, ajue kwamba mimi

kumbe kule kijijini nitakuwa aidha tofauti na wa mjini au nitakuwa bora. Kwa hiyo, atafurahia kwenda kufanya kazi vijijini, kuliko hivi sasa ambapo anayekwenda kijijini akifikiria kupata nyumba, akifikiria hali ya kijijini, anaanza kujifikiria mara mbili mbili, anatamani kufanya kila mbinu ili abaki mjini. Watakapopata motisha, labda wao na familia zao, na uhakika pengine wa kupata malipo ya ziada kwa kazi wanayofanya vijijini, kwa sababu tunajua vijijini changamoto ni nyingi. Kwa kweli wafanyakazi wengi watatamani kwenda vijijini hata kuliko kubaki mijini kwa sababu wanajua wataangaliwa kwa jicho tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya muda, naomba kuipongeza tena Serikali kwa kazi nzuri. Naomba kuwashukuru sana Wizara kwa kuiangalia hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea, atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, na Mheshimiwa George Natany Malima, ajiandae.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Afya. Awali ya yote, nitumie fursa hii kuushukuru uongozi wa Wizara; moja, dada yangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu, na kaka yetu Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel. Pia nawapongeza Dkt. Self Shekalaghe pamoja na dada yetu Grace Maghembe kwa kazi kubwa wanayoifanya kuhakikisha sekta ya afya kwenye nchi hii inapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, naishukuru na kuipongeza Serikali yetu ya Awamu ya Sita kwa kazi kubwa ambayo imeifanya hasa kwenye sekta ya afya. Wote tunashuhudia kazi kubwa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia

Suluhu Hassan ameifanya kwenye sekta hii ya afya. Wote tunashuhudia ujenzi wa hospitali za kikanda, hospitali za rufaa za mikoa, hospitali za wilaya na vituo vya afya na zahanati. Kimsingi, Serikali yetu imefanya kazi kubwa sana, hivyo hatuna budi kuipongeza.

Mheshimiwa Spika, hususan kwenye Jimbo langu la Korogwe mjini, kazi kubwa kwenye sekta ya afya imefanyika, hivyo sina budi kuipongeza Serikali yetu. Mfano, kwenye jimbo langu la Korogwe Mjini kwa kipindi hiki, Mheshimiwa Dkt. Samia akiwa Rais, ameshatujengea vituo vya afya viwili. Moja, kwenye Kata inaitwa Mgombezi na kingine kwenye Kata ya Kwamsisi. Pamoja na hilo, tumejengewa *EMD* kwenye hospitali yetu ya Wilaya na zahanati karibu kwenye kila Kijiji. Kwa hiyo, hiyo ni kazi kubwa ambayo Serikali yetu imeifanya kwenye sekta ya afya na hatuna budi ya kuipongeza sisi kama wawakilishi wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada kubwa ambazo Serikali imefanya, bado ziko changamoto chache ambapo leo napenda kuzieleza ili Wizara yetu hii ya Afya ikapate kuzichukua na kuzifanyia kazi, hasa nitajikita moja kwa moja kwenye Jimbo langu la Korogwe Mjini.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tumejengewa vituo vya afya kama nilivyoeleza hapo mwanzo, lakini hadi sasa hivi bado hatujaletewa vifaa tiba. Hivyo naomba Wizara, Mheshimiwa Waziri, basi tupatiwe vifaa tiba ili vituo vile vya afya vizuri kabisa ambavyo Serikali imejenga viende kufanya kazi na wananchi wa Korogwe waweze kunufaika na matunda ya Serikli yao ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Spika, ukiacha vifaa tiba, changamoto nyingine inayotukumba kwenye Halmashauri yetu kwenye sekta ya afya ni upungufu mkubwa wa watumishi kwenye sekta hiyo. Kwenye Halmashauri yetu ya Korogwe Mjini, ili kukidhi mahitaji ya sekta ya afya tunatakiwa kuwa na

wafanyakazi zaidi ya 700, lakini hadi sasa tuna wafanyakazi chini ya 300, hivyo tuna upungufu wa wafanyakazi 400.

Mheshimiwa Spika, upungufu huo hasa kwa wataalam wa maabara, wauguzi pamoja na wafamasia. Hivyo, tunaishauri na tunaiomba Serikali yetu ikapate kuendelea kuajilri watumishi wa afya kama ilivyofanya hapo awali ili wakapate kuweza kuongezeka na vituo vile ambavyo tumejenga vikapate wataalamu ili wananchi wetu waweze kuhudumiwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ambayo napenda kuizungumzia leo, ni changamoto ya usafiri. Kwenye Halmashauri yetu ya Korogwe, kwenye jimbo langu, kwenye hospitali zetu tuna uhaba mkubwa sana wa usafiri hasa *ambulance* lakini pamoja na magari mengine ya *administrative supervision* na kazi nyingine. Hivyo, tunaiomba Serikali ikapate Kwenda kutupatia *ambulance* kwa ajili ya vituo hivi vya afya lakini pamoja na hospitali yetu ya wilaya.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ambayo napenda kuieleza kwenye sekta ya afya kwenye jimbo langu ni uchakavu wa miundombinu. Nilikwisha kueleza hapa Bungeni si mara moja kwamba, Hospitali yetu ya Korogwe, hospitali yetu ya wilaya ni chakavu sana na imechoka ilijengwa tangu mwaka 1952 na haikidhi kabisa matakwa ya kuhudumia watu wetu kwa kipindi hiki. Nimekwisha kuomba mara nyingi lakini nipende kuishukuru Serikali kupitia Wizara ya TAMISEMI, kwenye bajeti hii imetutengea shilingi milioni 900 kwa ajili ya ukarabati wa hospitali ile.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na ushauri kidogo mahali hapa, naomba Waziri wa Afya akae na Waziri wa TAMISEMI, ili wapate kukubaliana jambo hili. Hospitali yetu ya Korogwe ambayo ni chakavu na hospitali nyingine kwenye nchi hii, hospitali zile kongwe na chakavu zimepelekewa fedha kwa ajili ya ukarabati shilingi milioni 900.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, fedha hizi zisiende kufanya ukarabati hatutaona *value for money,* fedha hizi ziende kujenga majengo mapya. Safari hii mmetupatia milioni 900 basi tucahgue majengo gani yatajengwa na milioni 900 safari hii na mwakani mtupatie nyingine zikajenge majengo mengine. Mkisema muende kukarabati hela zitisha na hamna kitu kitakacho onekana pale. Hatutapata *value for money* kwa ajili vijengo ni vidogo *designing* yake ni ya miaka 60 iliyopita, tunakwenda kukarabati kitu gani?

Mheshimiwa Spika, hivyo ninamuomba Waziri wa Afya akae na akabualiane na Waziri wa TAMISEMI, wakubaliane ili hizi hela zisiende kufanya ukarabati. Watu watakwenda kupiga piga rangi, watabadilisha mabati, *tiles* kidogo hamna kitu kitakachoonekana baada ya miaka miwili tutakuwa na uhitaji mwingine. Hivyo, fedha hizi ziende kujenga majengo mapya naamini miaka miwili mpaka mitatu tutapata hospitali mpya kabisa ambazo zitakidhi mahitaji ya karne hii, sio kukarabati hozpitali za miaka 50 iliyopita. Huo ndio ulikuwa ushauri wangu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, Mheshimiwa Waziri, naomba hili ulielewe vizuri dada yangu, najua wewe ni mpambanaji na unaweza. Serikali imefanya pakubwa, imejenga majengo, inaajiri wataalam, vifaa tiba na hadi sasa hivi tuna madawa ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, changamoto tuliyokuwa nayo ni malalamiko ya wagojwa juu ya wauguzi na wataalam kwenye hospitali zetu. Kumekuwa na malalamiko mengi kwenye hospitali zetu za halmashauri wagonjwa wanalalamika hawawi–*treated* vizuri na wauguzi wetu. Hivyo, Mheshimiwa Waziri, ushauri na rai yai yangu kwako, hebu fanya uchunguzi kwenye hospiali za Halmashauri ya Korogwe Mjini lakini na hospitali nyingine kwenye taifa hili uweze kuangalia ni kwa ajili gani wagonjwa wanalalamikia wauguzi.

Mheshimiwa Spika, kama shida ipo, basi mfuatilie mjue ni shida gani inawezekana wauguzi wetu wanakuwa *over worked,* inawezekana watu ni wachache au hawapati stahili zao vizuri. Basi muende kufuatilia changamoto hizi ili muweze kuzitibu ili waweze kuhudumia wananchi wetu vizuri. Mnafanya kazi kubwa lakini wagonjwa wetu wasipohudumiwa vizuri itakuwa ni kazi bure, hivyo Mheshimiwa Waziri nakuomba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo ninatamani pia wawe wanapewa elimu ya mara kwa mara *ethical education* na vitu vingine. Waambiwe ni namna gani wao ni muhimu kwenye afya ya watanzania. Mheshimiwa Waziri, hayo ni machache ya kwangu niliyokuwa nayo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, nilikuwa na hayo machache kwenye bajeti hii ya Wizara ya Afya. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Fatma Hassan Taufiq, atafuatiwa na Mheshimiwa George Natany Malima, Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasam, ajiandae.

**MHE. FATMA H. TAUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Afya kwa Mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, niungane na Waheshimiwa Wabunge wote kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Afya na Taasisi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo naomba pia na mimi nichukue fursa hii kumshukuru sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri sana anayoifanya katika suala zima la

kuleta maendeleo. Pia kuhakikisha kwamba anaiangalia sekta hii ya Afya kwa jicho la kipekee, nampongeza sana Mheshimiwa Rais. Tunajua kabisa azma yake ni kuhakikisha kwamba afya ya watanzania ina imarika ili kusudi waweze kufanya maendeleo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa Saba wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ambapo ameeleza kwamba azma ya Serikali ni kuboresha utoaji huduma pamoja na kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya katika hospitali za rufaa, hospitali za mikoa, hospitali za kanda, maalum na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili naomba nitoe ushauri, natambua kazi nzuri sana ambayo inafanywa na Serikali. Lakini pia napenda kuishauri Serikali hasa kwa Mkoa wangu wa Dodoma, katika Mkoa wa Dodoma, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma, hospitali hii ni tegemeo kubwa sana kwa wananchi wa Dodoma na maeneo mengine ya Jirani.

Mheshimiwa Spika, wananchi wengi wanategemea kupata matibabu katika eneo hili. Naipongeza sana Serikali imejitahidi sana kuwekeza miundombinu mbalimbali ikiwemo ujenzi wa jengo la wagonjwa la *ICU* lakini pia usimikaji wa mashine ya *CT – Scan* ambayo iko katika hospitali ile na inatumika vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hayo ni kwamba hospitali ile ina majengo mengi sana ambayo ni chakavu na ambayo yalikuwepo tangu enzi za mkoloni. Pamoja na kwamba kuna majengo ambayo yamekuwa yakijengwa lakini bado eneo lile ni dogo. Kwa hiyo, nilikuwa naomba nitoe ushauri kwamba, hebu Serikali ione umuhimu basi katika eneo lile dogo iweze kujenga majengo ya ghorofa ili kusudi kuweza kupata majengo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na mpango wa Serikali wa kujenga ghorofa ambalo lingeweza kuhudumia magonjwa ya mifupa. Ushauri ni kwamba Serikali ione uharaka sasa wa kujenga jengo hili la mifupa ili kusudi wananchi waweze kupata tiba vizuri na jengo liwe la kisasa. Naamini kabisa kama likijengwa jengo hili basi huduma zitapatikana kwa uzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba hospitali hii ya mkoa ambayo ni maarufu kwa jina la *General Hospital* inapakana na eneo la jeshi ambalo liko Jeshi la polisi pale. Kwa hiyo, kuna eneo liko pale, Serikali iome umuhimu wa kulitoa lile eneo la Polisi kwa hospitali ili kusudi waweze kujenga miundombinu zaidi katika kuendeleza majengo mapya kwa ajili ya utoaji wa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri mwingine ni kuhusiana na manunuzi ya dawa katika vituo vya kutolea huduma. Kuna fedha kwa ajili ya manunuzi ya bidhaa za dawa moja kwa moja kutoka bohari, hili ni jambo jema sana. Lakini kuna nyakati bidhaa hizi yaani dawa zinakuwa hazipatikani katika bohari ya dawa. Ushauri wangu, je, Serikali haioni umuhimu wa kuwa na asilimia fulani ya fedha zipelekwe kwenye akaunti za vituo husika ili bidhaa zinunuliwe kutumia wazabuni wengine? Hii itachangia upatikanaji wa dawa pale ambapo bohari kuu inakuwa imeishiwa dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niliona kwamba nishauri hili kwa sababu tumekuwa tukipata malalamiko ya mara kwa mara kuhusiana na upungufu wa dawa katika vituo pamoja na hospitali. Kwa hiyo basi, ushauri wangu kama Serikali itaona hii inafaa basi hebu ichukue ushauri huo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilitamani kuzungumzia nilitaka kuzungumzia kuhusiana na suala zima la mwitikio wa UKIMWI. Natambua juhudi kubwa sana ambazo Serikali imekuwa ikizifanya kwa ajili ya kupambana na

UKIMWI, naipongeza sana Serikali. Hata hivyo, pamoja na pongezi hizo bado maambukizi mapya yanaendelea na takwimu za hivi karibuni zinaonesha kwamba walau karibu wananchi 54000 wamepata maambukizi mapya. Hii taarifa nzuri. Basi nilikuwa naomba Serikali iendelee na juhudi za kudhibiti maambukizi ya VVU na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, lakini katika ukurasa wa 40 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, watoto 58760 wapo katika dawa za *ARV*. Hii sio taarifa nzuri kwani inaonekana kwamba watoto hawa walipata maambukizi kutoka kwa mama zao. Kwa hiyo basi, natambua juhudi za Serikali kwa kuona Kwamba maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto yanakuwa yanazuiwa. Kikubwa ni kwamba inabidi elimu itolewe ili kusidi hawa wakina mama waweze kufika katika vituo vya *clinic* mapema waweze kupata huduma mapema ili kusudi wasiweze kuwaambukiza watoto wao.

Mheshimiwa Spika, Tanzania bila maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto inawezekana. Kwa hiyo, nilikuwa naishauri Serikali iendelee kutoa elimu hasa katika maeneo ya pembezoni. Kwa sababu tunaamini kabia mijini wanapata elimu lakini pia maeneo ya pembezoni wanapata elimu lakini wanahitaji elimu zaidi ili kusudi waweze kupata huduma mapema na mwisho wa siku maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto yanaweza kuzuiwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, ambalo nilitaka kuzungumzia kuhusiana na hili suala la UKIMWI ni kuhusu huduma ya *early infant diagnosis* ambapo watoto wachanga waliozaliowa na wakinamama wenye VVU hupimwa kwa kutumia vinasaba. Taarifa imebainishwa ya kwamba vituo viko 130 na vinaendelea kutoa huduma lakini ili kuweza kufikia malengo Serikali inatamani kuwa na vituo 340 na hii itasaidia kupunguza maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto hasa maeneo ya pembezoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, Serikali basi iweze ku–*speed up* kuhakikisha kwamba vituo hivi vinajengwa kwa wakati ili kusudi wakinamama wale ambao wana maambukizi waweze kupimwa na hatimae wakishajua hali zao waweze kupata zile huduma ili kusudi mwisho wa siku watoto wao wasiweze kupata maambukizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba niseme kwamba naunga mkono hoja ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa George Natany Malima, afafuatiwa na Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasam, Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, ajiandae.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango katika hotuba hii ya Wizara ya Afya. Kwanza kabisa naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, kwa ajili ya kazi nyingi nzuri ambazo zinaendelea kufanyika katika nchi yetu. Sisi watu wa Mpwapwa Mheshimiwa Rais, amefanya mambo mengi makubwa na hasa ktika sekta hii ya afya.

Mheshimiwa Spika, tumeopata shilingi milioni 900 katika ukarabati wa hospitali yetu ya wilaya. Mtakumbuka huko nyuma nimezungumza sana habari ya uchakavu wa ile hospitali lakini nashukuru sana Wizara imepata tarifa na imesikia. Sasa hivi ukarabati unaendelea lakini tunajenga jengo jipya la huduma ya mama na mtoto. Kwa hiyo, nina mshukuru sana Rais, kwa ajili ya kutusaidia hilo.

Mheshimiwa Spika, sio hilo tu, tumejenga jengo la *ICU* kwa gharama ya shilingi milioni 250 na pia tumepata vifaa katika jengo hilo tayari vimefungwa vyenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 400 na huduma zinaendelea pale. Pia, kwa muda mrefu hospitali hii ya Mpwapwa haikuwa na *x–ray* lakini leo nina furaha kuwaambia Bunge lako Tukufu kwamba sasa

tuna *digital x–ray* na wananchi wa Mpwapwa wanaendelea kufurahia huduma za Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha pia tumefanikiwa kujenga au kumalizia maboma ya zahanati nane na zingine kazi zinafanyika tayari zinaendelea kumaliziwa na nyingine tayari zinatoa huduma kwa wananchi. Pia, tumeopata vituo vya afya viwili, kituo cha Iwondo na kingine tumejenga Matomondo. Vituo hivi vimejengwa maeneo ya Kimkakati, maeneo ambayo yako mbali sana na mjini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri amesema katika mwaka huu wa fedha wamepanga kununua *ambulance* zaidi ya 700. Niombe Mheshimiwa Waziri, utukumbuke na sisi wa Mpwapwa, tuna vituo vitatu kwa ujumla, kituo cha Mima, Iwondo na Matomondo vituo ambavyo viko kwenye maeneo ya kimkakati. Lakini pia tuna hospitali yetu ya wilaya haina gari ya kubebea wagonjwa, kwa hiyo, tukumbuke kwa ajili ya kupata magari ya kubebea wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Waziri nikushukuru wewe binafasi, umekuwa moja ya Mawaziri wanaofanya kazi zao kwa umakini sana. Nichukue fursa hii kukupongeza, na hata ukisoma ripoti yako unawea kuona umegusa kila eneo hata tunaposimama kuchangia tunasema kusema kweli tunataka kuweka mkazo tu lakini kwa kweli umejaribu kugusa kila eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia katika eneo la matibabu ya wazee, Mheshimiwa Waziri, umezungumza katika ukurasa wa 55 habari ya kuongeza dawa kwa ajili ya wazee. Lakini kuboresha huduma zao, lakini nikwambie kwamba bado hatujawa na mkakati thabiti wa namna ya kuwahudumia wazee kwa sababu wiki mbili zilizopita nilimpeleka mpiga kura wangu mmoja mwenye umri

wa mika zaidi ya 70. Nilipofika pale hospitali nilikuta kuna mabango yameandikwa mpishe mzee asipange foleni, kuna msamaha wa wazee. Mheshimiwa Waziri, lakini kusema kweli hayo mambo yameandikwa lakini *practically* hakuna kitu kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wazee wanateseka sana kwa sababu ya umri na uchumi wao mdogo basi wanateseka na wengi wanafariki kwa sababu ya kuteseka na kuchelewa kupata matibabu. Mheshimiwa Waziri, ningekushauri jambo hili mliangalie upya ikiwezekana mje na mpango mahususi au sera mahususi ya kuwatibu wazee wetu.

Mheshimiwa Spika, wazee wetu ni wengi wamefanya kazi katika Taifa hili kwa uaminifu mkubwa lakini leo inaonekana kama hatuwajali kabisa. Kwa hiyo, mzee yule hata tulipofika *issue* nyingine ikawa ni dawa ile aliyotakiwa kupata hakuna. Nikupongeze nimeona mmeongeza dawa tano kwa ajili ya wazee labda hilo litatusaidia. Pia shida iko pale kwamba dawa hazipo. Mheshimiwa Waziri, uje na sera maalum kwa ajili ya wazee hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, ambalo ningependa kukusisitiza pia ni uhaba wa dawa. Nimeona kwenye ripoti umezungumza mikakati ya kuongeza dawa hospitali lakini kwa kweli hospitalini bado kuna shida ya dawa. Kama nilivyosema watu wengi hawawezi kunua dawa nje ya maduka *private*. Kwa hiyo, mtu anakwenda hospitali na bima yake anaadikiwa dawa inakuwa hamna, akienda nje bima haiwezi kutumika, yako maduka ambayo hayakubali bima. Kwa hiyo, yule mtu anarudi nyumbani hana dawa kwa sababu tu hana hela ya kununua dawa.

Mheshimiwa Spika, ningeomba sana Mheshimiwa Waziri, yale maduka ambayo yako ndani ya hospitali yapate dawa zote ili wananchi wetu wakifika pale waweze kuhudumiwa vizuri. Shida ya dawa bado ni kubwa pamoja na juhudi nyingi

ambazo Serikali inafanya na wewe Mheshimiwa Waziri lakini dawa bado ni chache.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni huduma zisizolirisha katika hospitali zetu. Kuna wafanyakazi wachache ambao bado hawana lugha nzuri kwa wagonjwa. Mfano, hospitali yangu ya Wilaya ya Mpwapwa bado kuna malalamiko mengi kuhusiana na uhafifu wa huduma zinazotolewa pale. Watu wanajibiwa vibaya, watu hawatibiwi kwa wakati, kuna vurugu nyingi. Mheshimiwa Waziri ningeomba jambo hili ikiwezekana watumishi hawa wa afya wapate semina za mara kwa mara ili kuwafundisha maadili ya kazi zao. Kazi ya kuwatibu watu ni kazi ya wito inahitaji upendo, inahitaji mtu anaejitambua vizuri.

Mheshimiwa Spika, pamekuwa na watu ambao ni wajeuri, mtu anakwenda anaumwa anajibiwa vibaya wakati mwingine wanadaiwa rushwa, wanadaiwa fedha kwa mambo ambayo hayatakiwi kulipiwa. Kwa hiyo, kuna fujo nyingi kwenye maeneo haya ya kutolea huduma na kelele hizi zinachafua mahusiano bora au mahusiano mazuri na Serikali na wananchi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nirudie kumshukuru Mheshimiwa Waziri wetu wa Afya kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasam, atafuatiwa na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, Mheshimiwa Esther Lukago Midimu ajiandae.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia katika bajeti hii ya Wizara yetu pendwa ya Afya.

Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza sana Wizara kwa kazi nzuri wanazofanya madaktari wao, madaktari bingwa katika nchi hii, tumeona jitihada zao za dhati kutoka moyoni, kuanzia Jakaya Kikwete Muhimbili hapa Benjamini Mkapa, Bugando Mbeya na *KCMC* inaonyesha ni namna gani madaktari wetu katika nchi hii sasa wanaanza kwenda mbele zaidi ya uzio.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi ushauri wangu kwa Wizara, ni kwamba lazima ifikie sasa Wizara iunde timu ya madaktari bingwa labda, kwa sababu tunazo wilaya 139 na hao madaktari bingwa wawepo madaktari bingwa ambao ni *mobile unit,* wanaotembea.

Mheshimiwa Spika, hawa madaktari bingwa katika nchi hii watapunguza mrundikano kule Muhimbili, kwa sababu sisi tunajua kwa kalenda, kama labda Mkoa wa Mwanza kuna madaktari kumi; wanaingia madaktari bingwa wa macho, viungo, figo na moyo. Wakifika pale tunaambiwa kwamba Sengerema watakuwepo kwa wiki mbili au kwa siku mbili; wale madaktari bingwa watasaidia watu wetu ambao ni maskini ambao hawana uwezo wa kusafiri kuja katika hospitali za rufaa.

Mheshimiwa Spika, katika hili tunamshukuru Mheshimiwa Rais sasa vifaa tiba vimeanza kupelekwa nchi nzima. Tuna kila kitu katika hospitali zetu za wilaya. Mnafeli wapi watu wa Wizara ya Afya katika jambo hili?

Mheshimiwa Spika, Tunaona hospitalli zetu za makanisa Wajerumani wale Waholanzi wana ma-*flying doctors* wale, wanasafiri wanakuja Itigi, Sengerema na kwingine, na wanafanya jambo kubwa sana. Wanakuja na meli, sisi tumewahi kwenda kutibiwa na Wachina kwenye meli bandarini. Hapa tuna madaktari bingwa wamemaliza elimu zao, kwa nini msitengeneze u*nit* hiyo ya madaktari bingwa ambao bado hawajapata ajira lakini wawekwe katika

sehemu hiyo? Wale madaktari watasaidia sana kupunguza magonjwa hayo ambayo wananchi wamekaa nayo kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala jingine ambalo nataka niishauri Wizara hii ni kwamba, tunayo magonjwa haya ya mlipuko ambayo yamezunguka katika ukanda huu wa maziwa makuu haya magonjwa hayajaisha naishukuru sana Wizara kwa kuchukua hatua ya haraka katika hili gonjwa lililojitokeza Bukoba watu wengi waliona kwamba wale Watanzania inakwenda kuangamia lakini jambo hili waliweza kulidhibiti ndani ya siku kumi likaisha tunaipongeza sana Wizara katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule Usukumani wamenituma nije nishukuru wanasema yule Mama wa corona mbona hatumuoni, hali sasa siyo nzuri sasa tunataka huyu Mama wa corona sasa leo aje aseme hapa, je, corona imeisha? Kwenye nchi hii? hawa wanaokufa wanakufa kwa mafua tu? Au wanashindwa kupumua?

Mheshimiwa Spika, sasa haya tunakuomba sana Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yako uje utueleze haya magonjwa ya mlipuko ni namna gani mmejipanga nayo; na kama yamekwisha au kama hayajaisha basi tuendelee kuchukua tahadhari. Unayo nafasi kubwa sana kwa mujibu wa sheria kuwaeleza Watanzania nini kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, nakuja kuzungumzia hospitali zetu za wilaya. Hizi hospitali za wilaya sasa hivi zinapelekewa madaktari zimepewa vifaa tiba nchi nzima, lakini tunavyo vituo vya afya na zahanati. Sasa kule kwa sababu kuna madaktari sasa wanahitajika madaktari bingwa. Leo vituo vyetu vya afya vilikuwa havijapata madaktari vinapelekewa madaktari. Sasa, kama mnapeleka madaktari kule kwenye Hospitali zetu na vituo vya afya basi hizi hospitali za wilaya mziweke katika sehemu ya hospitali za rufaa. Kwa sababu,

kwa mfano kwenye jimbo langu mimi nina hospitali vituo vya afya ninavyo vinane bado nina zahanati karibu zahanati 30.

Mheshimiwa Spika, sasa unategemea kwamba wagonjwa wale tunawapa rufaa kuwapeleka Bugando au Sekou Toure hospitali inakwenda kuelemewa. Ninachoomba mimi katika sera sasa za Wizara mzitambue kuzichukua hizo hospitali za wilaya ziwe zenu, madaktari bingwa wapelekwe kule ili tupunguze msongamano Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri hili wazo Mheshimiwa Waziri alichukue. Katika majumuisho yake aje atuambie; kama wanaweza kuhudumia, kupeleka vifaa tiba na kila kitu kwa nini wasilete madaktari bingwa kule? Vifaa vya maabara na wataalamu wamepeleka, isipokuwa hatuna madaktari bingwa naomba sana Wizara wachukue jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, jingine ambalo ni la muhimu sana ni suala la huduma bora kwa hawa wagonjwa wetu. Tunakwenda kutoa huduma bora lakini muangalie na madaktari katika nchi hii sasa nao wapewe huduma. Madaktari wanakiumbia katika nchi hii, wanaondoka. Wauguzi nao muwajali sasa ifikie hatua…

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. TABASAM H. MWANGAO:** Mheshimiwa Spika, niache basi Mheshimiwa nimalizie.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasamu kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge.

**TAARIFA**

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nilikuwa naomba kumpa taarifa tu Mheshimiwa

tabasamu kwamba, hata vitabu vitakatifu vimeisema vizuri nafasi ya daktari na imeisema; *"Innal Muallima Wa Twabiba Kila Humaa, Laa Yanswahan Idhaa Huma Lam Yukramaa Fakna-A Bijahilika In-Jaufata Muallimu, Fasbir Lidaika In Jaufata Twabiba,"* kwamba; ridhika na ujinga wako ukimuudhi mwalimu, lakini subiri maradhi yako ukimuudhi daktari. Madaktari ni watu muhimu sana, tusiwaache watoke nje. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasamu unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. TABASAM H. MWANGAO:** Mheshimiwa Spika, ameanza kwa Aya kwa hiyo amenipiga kwa Aya, na mimi kama muumini naunga mkono taarifa yake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la utoaji wa huduma zetu za afya. Viongozi wetu wa kitaifa wamekuwa wakipita kule katika wilaya zetu, wanapita katika na mikoa, tarafa na kata, wanatoa ahadi kwamba hapa patajengwa hospitali ya wilaya, patajengwa kituo cha afya, patajengwa zahanati.

Mheshimiwa Spika, sasa tunamuomba sana Waziri wa Afya, hizi ahadi za Marais, ahadi za Waziri Mkuu, ahadi za Mawaziri wao wenyewe mnazozitoa kwa wananchi zinakuja kututesa sisi. Sisi Sengerema tunakushukuru ulitoa ahadi ya kujenga Kituo cha Afya Chifufu, kile kituo cha afya Mheshimiwa Waziri wamenituma nije nikushukuru kimeisha, tunakupongeza sana kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, alipita Hayati John Pombe Magufuli pale Busisi, na pale Busisi ni kwao, akatoa ahadi kwamba kuna kituo cha afya kinajengwa pale akiwa na Naibu Waziri Mollel; hili jambo mpaka sasa hivi mnataka labda mimi nikashindwe uchaguzi, kuna lawama zingine zitakuwa zinanitafuna mimi kwa sababu Mheshimiwa Mollel ulikuwepo. Sasa, naomba leo kwenye majumuisho hapa mkija mseme lini Kituo cha Afya cha Busisi kinakwenda kukamilika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jamani tuziheshimu hizi ahadi za Marais. Marais wanapopita kule kwetu sisi wanatuacha na hali mbali. Mnakuja kwenye bajeti hivi viyu havimo, inakuwa ni hatari. Sasa naomba kwenye majumuisho ya Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri waje waseme lini jambo hili litakuwepo.

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho nina Hospitali ya Wilaya. Wewe mwenyewe Mheshimiwa Ummy ulifika pale na umeiona ile hospitali. Mheshimiwa Jafo alipita pale akaona; na leo wote mmo humu. Mheshimiwa Mollel hii Hospitali ya Wilaya imeshakamilika kila kitu. Ni kwa nini hospitali hii haifunguliwi? Naomba majibu katika hayo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nakupongeza leo umekaa kwa utulivu mkubwa na mimi nakuunga mkono dakika zangu kumi hazijatosha nimeacha dakika mbili kwa wengine.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Mungu akubariki sana, amina. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Tabasamu. Waheshimiwa Wabunge jambo moja, Wabunge mnazungumza na simu sana Bungeni, siyo heshima kwa Bunge, siyo heshima kwa wanaokuja kujifunza Bungeni namna tunavyofanya kazi, haipendezi. Ndiyo maana milango imewekwa mingi kila upande. Ukiwa na dharura toka nje na simu kazungumze rejea.

kama una simu ndefu nenda mbali zaidi kazungumze na wapigakura maliza urejee. Haipendezi kuzungumza na simu Bungeni; na wengine mnaweka na vidude maskioni. Sasa sijui ni kwamba hutaki kumsikia anayechangia unasikiliza mziki unamsikiliza mpiga kura sijui unamsikiliza nani? Na hili liko kwa Wabunge, Mawaziri, kila mtu; watu mnaweka vidude

maskioni. Nenda nje kapokee simu ukimaliza rejea. Haipendezi kuzungumza na simu kwenye kikao kama hiki. Niwaombe sana, niwaombe sana tujizuie kuzungumza na simu Bungeni.

Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Lukago Midimu Mheshimiwa Noah Lemburus Saputu, ajiandae.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia Wizara hii ya Afya.

Mheshimiwa Spika, nianze kukupongeza wewe binafsi kwa kazi kubwa unayoifanya ya kuendesha Bunge lako hili. Nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa aliyoifanya kwenye suala zima la afya. Kabla sijaongea maeno yote nianze kuongea jambo liliotokea juzi na leo Bungeni tumeliona Mheshimiwa Rais ameweza kutafuta vifaa vya *high technology,* leo tunatibu *sickle cell*.

Mheshimiwa Spika, Binafsi sikuwahi kujua kaka *sickle cell* inapona; yaani sikuwahi kujua kabisa kwenye maisha yangu. Lakini kwa juhudi binafsi za Mheshimiwa Rais ameweza kupambana kuhakikisha leo katika nchi 50 za kiafrika nchi yetu ya Tanzania inatibu *sickle cell,* ni sifa kubwa sana na juhudu kubwa sana za Mheshimiwa Rais, tunazidi kumpongeza.

Mheshimiwa Spika, lakini nimpongeze Mheshimiwa Waziri Ummy na Naibu wake Mollel kwa kazi kubwa wanayoisimamia kufikia hatua hii tuayoiongelea sasa hivi. Mheshimiwa Rais yuko na juhudi sasa za kujenga kituo mahiri cha utibabu wa kansa hapa Dodoma katika Hospitali ya Benjamini Mkapa ambacho kitakuwa ni kituo kikubwa cha Afrika. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kutujali

kwa sababu ni magonjwa ambayo hayana tiba na yanaua vizazi na vizazi.

Mheshimiwa Spika, hakika tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais tangu tumepata uhuru wa nchi hii hatujawahi kuwa na mashine kubwa kama za *CT scan* kwenye mikoa yetu, ilikuwa ni lazima ufunge safari uende Muhimbili uende Bugando, na hiyo ni kwa familia tu ambazo zina uwezo familia ambazo hazina uwezo hata kujua mgonjwa wao anaumwa nini inakuwa siyo rahisi na hatimaye mnakutwa na vifo.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa juhudi zote za kazi kubwa anayoifanya kusimamia miradi ya kimkakati ambayo inaenda kumalizika, kupeleka pesa kwenye halmashauri, kufanya kila aina ya kazi. Halmashauri sasa hivi kuna fedha zinazoenda asilimia 100 tofauti na ilivyokuwa hapo kale. Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa sana sana sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais pia amejitoa kusimamia Demokrasia ya nchi hii ni jambo kubwa sana. Sasa hivi hakuna tena mapigano hekaheka za kisiasa, tuko kimya tunatekeleza maendeleo jinsi Mheshimiwa Rais anavyo yataka.

Mheshimiwa Spika, mimi niungane tu na mzee ma-bi, ma-bi na ma-tri ma-tri, kwamba wale wenzetu wa upande wa pili ambao ni marafiki zetu wa kisiasa kwa heshima kubwa na kazi kubwa anayofanya Mheshimiwa Rais waweze kumuachia apite bila kupingwa, kwa sababu ameleta vitu ambavyo tulikuwa hatuvifikirii kabisa. Ameleta demokrasia, amaeleta maridhiano ambayo nchi yetu imekuwa ina sifa kubwa kwa wenzetu. Sasa, kama za jirani wanaona sifa kubwa kwa nini sisi tusimpongeze Mheshimiwa Rais na kumpa heshima ya kupita bila kupingwa?

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile nindelee kuipongeza Serikali ya awamu ya sita kwa kazi kubwa waliyoifanya kwenye Mkoa wetu wa Tabora leo hii Mkoa wa Tabora tumekuwa na jengo la *emergency* ambalo lina vifaa vyote na inafanya kazi, ni kitu ambacho hakijawahi kutokea, kwa kweli. Nimezaliwa pale na nimekulia hatukuwa na jengo la *emergency* na niliwahi kuongea humu Bungeni mara kadhaa. Kwa Mheshimiwa Samia Suluhu imewezekana na jengo hili linafanya kazi. Saa hivi tunamalizia jengo la *ICU* ambapo vifaa vya *ICU* vyote vimefika, ni bado muda mchache tu tutaanza kulitumia, tunatoa pongezi kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, tuna wodi mbili za wazazi za ghorofa, wodi ya kwanza imekwisha bado wodi ya pili ambayo ipo inaendelea, ila fedha zimekwisha. Mheshimiwa Ummy tunakuomba sana utumalizie jengo hili la ghorofa la mama na mtoto ili lianze kutumika. Tunajua unajua umuhimu wa mama na mtoto na tunajua jinsi unavyolisimamia jambo hili tunakuomba sana.

Mheshimiwa Spika, narudia kusema katika mkoa wa tabora tuna *CT scan* ambayo inafanya kazi iliyonunuliwa kwa bilioni moja na milioni mia nane. Hili ni jambo la kumshukuru sana Mwenyezi Mungu. Leo ndugu zetu wamekuwa wanapata kila kitu pale Tabora wanampongeza sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunashukuru sana kwa watumishi 38 mliotupa tumewagawa katika kada mbalimbali; lakini bado tuna upungufu mkubwa wa watumishi hasa madaktari bingwa. Kwenye ikama ya Serikali tunatakiwa tuwe na madaktari bingwa 21 lakini tuna madaktari watano tu, wa akina mama mmoja, wa watoto watatu na wa upasuaji mmoja; katika mkoa mzima wenye wilaya saba. Mkoa huu kwenye Sensa ya mwaka jana imekuwa mkoa wa tatu kwa

kuwa na wananchi wengi. Watanzania wengi wanaishi Mkoa wa Tabora kutoka Dar es salaam, Mwanza kisha Tabora, lakini tuna madaktari bingwa watano tu.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri atuongezee madaktari bingwa. Tofauti na hapo watu wengi sana inabidi waende kwenye hospitali za rufaa wabebwe na *ambulance*. Hospitali yetu ya Mkoa wa Tabora ina *ambulance* moja tu, *ambulance* nyingine zote ziko *TAMESA* zinaumwa, haziponi wanasema vipuli hakuna. Sasa sijui ni vipuli hakuna au ni bajeti ya Serikali haipo; hapa nashindwa kuelewa. Kwa sababu hizi *land cruiser* vipuli vyake vipo. Mkitupatia hata milioni 50 tunaweza tukatoa *ambulance* hata 10 zikafanya kazi kwa sabau mkoa wetu ni mkubwa mahitaji ni makubwa sana. Tunakumba sana Mheshimiwa Waziri tupate *ambulance*. Mkoa wa Tabora ni mkubwa, wewe unaufahamu, na una wakazi wengi wengi kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu suala la dawa limekuwa ni kero kubwa. Mheshimiwa Waziri nikuombe sana muongeze mtaji *MSD* ili watu wakiwa na *cash* sasa wafike walipie na wapate dawa za kwenda kwenye mikoa yao na Watanzania waendelee kuhudumiwa. Tunajua Serikali imetenga pesa nyingi hilo Mheshimiwa Waziri hautalishindwa.

Mheshimiwa Spika, ningee sasa kuhusu Malaria. Mwaka 2017/2018 tulikuwa na wastani wa asilimia 11.7 za wagonjwa wa malaria lakini leo hii mwaka 2022 tuna wastani wa 23.4 na hali ya malaria imekuwa mbaya, tuna wagonjwa wengi kwenye hospitali yetu ya mkoa ambao wanaumwa malaria.

Mheshimiwa Spika, nimuombe Mheshimiwa Waziri wafanye kila aina ya mikakati kuhakikisha tunapata dawa nyingi za malaria. Pia wafanye mkakati wa kuhakikisha wanazuia ugonjwa huu wa malaria kwenye mkoa wetu, ambao umekuwa ni mwingi sana. Tunakuomba sana Waziri.

Ugonjwa huu tunajua unashambulia watoto wadogo pamoja na akina mama wajawazito, tunakuomba sana utusaidie.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri aliwahi kuja Tabora. Tulionge humu Bungeni wakatuambia kwamba hospitali ya kanda inajengwa kwenye Mkoa wa Tabora. Mheshimiwa Ummy alikuja Tabora, tukafanya mkutano tukiwa naye kwenye Hospitali ya Kitete, akasema tafuteni eneo. Tumetafuta eneo ekari 200 kwenye Wilaya ya Uyui. Mheshimiwa Waziri hii Hospitali yetu ya Kanda ya Mkoa wa Tabora vipi? Tunaomba ukija ku-*wind up* utupe majibu. Wananchi wa Tabora wamenituma wanasema tunataka hospitali yetu ya kanda, Mheshimiwa Waziri alituahidi hapa. Kwa hiyo Mheshimiwa Ummy wanakusikiliza na wanategemea majibu yatoke kwako ili waweze kujua kuhusu hospitali yao.

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa kusema, kuna watu waliongea hapa wakasema wauguzi wengi wana majibu mabaya sana. Lakini mimi niwe upande wa wauguzi kwa leo. Niliwahi kwenda kumuangalia ndugu yangu hospitali amelazwa wodi moja ina vitanda 40 wamelala wagonjwa wawili wawili. Huyu nesi yuko na nesi a*ttendant* wake mgonjwa huyu anamaliza *drip,* mgonjwa huyu anatapika, mgonjwa huyu anatakiwa achomwe sindano. Yaani inafika *stage* nilikuwa nawasaidia kuwachukua wagonjwa kuwapeleka kwenda kujisaidia. Wanazidiwa Manesi wetu hata ningekuwa mimi wagonjwa 80 walio mahututi unawahudumia wewe peke yako. Nikumuomba Mheshimiwa Waziri mjitahidi sana kutuongezea wauguzi.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kuwalaumu saa nyingine mtu anachoka anafikia *the maximum,* yaani anajikuta amejibu tu jibu lile. Na sisi kwa kweli tuone kazi kubwa wanayoifanya wauguzi wetu kazi kubwa wanayoifanya madaktari wetu.

Mheshimiwa Spika, kitaalamu wanatuambia sijui daktari mmoja anatakiwa ahudumie watu wangapi, lakini unakuta ni daktari mmoja tu tangu asubuhi amehudumia watu zaidi ya 150, amechoka, yuko hoi. Tuendelee sana kuwasemea ili waweze kupata madaktari wengi na manesi wengi watu wetu waweze kupata huduma nzuri; lakini pia waendane na posho zao stahiki ambazo pia zitazidi kuwatia moyo manesi wetu na Madaktari wetu na…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa wako umekwisha

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Esther Lukago Midimu atafuatiwa na Mheshimiwa Noah Lemburus Saputu Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, ajiandae.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuongea, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anazozifanya anaboresha miundombinu ya afya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amejenga zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya na hospitali za mkoa. Mheshimiwa Rais amefanya kazi nzuri, Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan hayuko tayari watu wake wafe kwa kukosa matibabu. Mama yupo vizuri tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, cha kwanza hapa duniani ni afya, bila afya hata ukiwa na mamilioni ya pesa haisaidii. Tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuboresha afya ndio maana vifo vya mama na watoto vimepungua.

Nampongeza Mheshimiwa Waziri Ummy na Naibu wake kwa nzuri wanazozifanya. Mheshimiwa Waziri anafanya kazi nzuri, hotuba yake ni nzuri, namjua yeye ni mchapakazi, nina imani atasimamia hotuba yake ambayo imesheheni matumaini ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea na pongezi kwa Mheshimiwa Rais kwa kuboresha Hospitali ya Muhimbili. Hospitali ya Muhimbili, sasa hivi inafanya operesheni ya kichwa, inapandikiza figo, inafanya operesheni ya moyo. Hata wagonjwa kutoka nchi za nje wanakuja kutibiwa. Hiyo ni kazi ya Mheshimiwa Samia Suluhu, Mama yetu ametuheshimisha, tuko vizuri Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuboresha huduma ya matibabu ya kansa Bungando. Mwaka juzi tulisimama hapa Wabunge wa Kanda ya Ziwa tukaomba matibabu ya kansa yasogezwe Bugando kwa sababu wagonjwa wengi wa kansa wanatoka Kanda ya Ziwa. Mheshimiwa Rais alisikia kilio chetu sasa hivi matibabu yanatolewa hapo karibu, hawawezi kuhangaika tena kwenda Dar es Salaam kutibiwa. naishukuru Serikali kwa kuanzisha utafiti wa kuweza kujua ugonjwa wa kansa unasababishwa na nini Kanda ya Ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea na pongezi kwa Serikali imetujengea hospitali ya mkoa, lakini pia tuna jengo la mama na mtoto, Mheshimiwa Ummy analifahamu yeye ni mwanzilishi. Bajeti yake ni bilioni 5.7, jengo hilo limefikia asilimia 85. Tunamwomba Mheshimiwa Ummy akija kutoa majibu hapa, atupatie bilioni 1.7 ili tuweze kukamilisha hilo jengo la ghorofa na ni zuri la kisasa. Hiyo ni kazi ya Mama Samia Suluhu, hongera sana Mama yangu kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea na pongezi kwa majengo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imetujengea jengo la kutakasia vifaa, ufuaji wa nguo, nyumba mbili za watumishi, nyingine ni *three in one,* lakini pia katika hospitali yetu hiyo tumeletewa *CT scan*. Tulikuwa tunahangaika na kipimo hicho, watu wa Mkoa wa Simiyu walikuwa wanaenda kupata hicho kipimo Mwanza, lakini sasa hivi wanapata Mkoani Simiyu, hiyo ni kazi ya Mama Samia Suluhu, Mama yuko kazini. Ahsante sana Mama kwa kazi nzuri kwa kujalia afya za watu wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi, hospitali yetu ya mkoa haina uzio kabisa na mwaka jana nilisimama nikasema hospitali haina uzio. Upande wa kushoto tumepakana na mlima, upande wa kulia tumepakana na barabara ya lami. Mlimani kuna vichaka vichaka, hospitali ikikosa uzio, utoroshwaji wa vifaa tiba na madawa ni rahisi sana. Mtu anaweza akasomba akaenda kuficha mlimani, halafu baadaye usiku anavisafirisha. Pia na hospitalini wanaenda wagonjwa wa aina mbalimbali. Kuna mwingine anaweza akaenda amechanganyikiwa wa afya ya akili akakimbilia barabara akagongwa gari. Naomba Serikali itujengee uzio, Mheshimiwa Ummy mtani wangu ameinisikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia hospitali hiyo hiyo haina wodi za kulaza wagonjwa. Hatuna wodi ya wanaume, hatuna wodi ya wanawake na hatuna wodi ya watoto. Naiomba Serikali iweze kutujengea halafu na jengo la bima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la hospitali ya mkoa halijapimwa, halina hati. Naiomba Serikali iweze kupima eneo hilo halafu iweze kutupatia hati miliki. Katika hospitali yetu ya mkoa tuna upungufu wa watumishi. Watumishi walipo ni 231, upungufu wa watumishi 437, *specialist* wa nne, *specialist* wanaohitajika 21, Wauguzi waliopo 102 upungufu 97, upungufu wa Madaktari 27, upungufu wa Wafamasia 12. Tunaomba Serikali ituletee watumishi wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kumpongeza Rais wetu katika hospitali zetu za wilaya ametuletea *X-Ray*. Kama unakumbuka nilisimama hapa mwaka jana nikaomba *X-Ray* kila wilaya. Sasa hivi Serikali yetu ni sikivu imeshaleta *X-Ray,* hata kama mtu akipata ajali sasa hivi hawezi akakimbia kwa waganga wa kienyeji, atatibiwa hapo hapo, matatizo yatagundulika mapema. Ila naomba sasa wataalam wa mionzi hatuna. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tuna Hospitali ya Somanda wakati hospitali ya mkoa hawajaanza kujenga ile hospitali ilipandishwa hadhi ikawa hospitali teule ya mkoa. Hiyo hospitali ni ya muda mrefu, majengo yamechakaa, tunaomba pesa ili yale majengo yaweze kukarabatiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu atafuatiwa na Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi ajiandae.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Afya lakini nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetupa uzima kuwepo katika Bunge hili.

Nikushukuru na wewe kwa jinsi ambavyo unaendelea kuendesha Bunge lako kwa umakini na umahiri mkubwa sana. Niendelee kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo anaongoza Taifa letu, lakini kuhakikisha kwamba wananchi wake wanaendelea kupata afya njema kwa kutoa vifaa tiba, kujenga majengo, zahanati, vituo vya afya na hospitali za wilaya na hata za mikoa na kuleta vifaa tiba mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Mheshimiwa Rais katika kipindi hiki ametuheshimisha sana sisi Wabunge, kwa sababu ametuletea miradi mikubwa mpaka ukiwa jimboni unakosa uelekee upande upi katika kukagua miradi. Kwa kweli tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. Pamoja na pongezi zote nilizozitoa kwa Wizara ya Afya kwa maana ya Waziri wetu Ummy Mwalimu pamoja na Naibu Waziri wake pamoja, Katibu MKuu na Naibu Makatibu Wakuu na Wizara nzima kwa ujumla na Madaktari wote hapa nchini lakini bado tunasema barabara ndefu haikosi kona. Kwa hiyo, katika yale ambayo tunayo kama Wabunge na hasa mimi kama Mbunge wa Jimbo la Arumeru Magharibi, kuna mambo ambayo pia napenda tujaribu kushauri ili basi mwisho wa siku hili gurudumu liweze kusonga mbele sisi kwa pamoja kwa maana ya kuwahudumia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa Serikali katika Jimbo langu la Arumeru Magharibi tumejengewa vituo vya afya karibu vitatu. Tumejengewa zahanati nyingi kumalizia nguvu za wananchi, bado zingine hazijaisha, lakini kwa kweli hizo ni shukrani ambazo naweza kusimama katika Bunge hili na kujivunia kwamba natoa shukurani nyingi sana sana kwa Serikali yetu chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema barabara ndefu haikosi kona. Kwenye Jimbo la Arumeru Magharibi kulikuwa na hospitali ambayo naiongelea kila siku katika Bunge hili ya wilaya. Imepandishwa hadhi toka 2012 na Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Jakaya Kikwete. Hospitali hii ilipandishwa hadhi, Rais aliahidi pia kwamba lami kilometa 2.8 iwekwe lakini pia majengo yaongezwe, hospitali hiyo haina jengo la wagonjwa wa nje kwa maana ya *OPD*, hospitali hiyo haina *X-Ray,* hospitali hiyo haina jengo la mochwari. Hospitali hiyo haina chochote na tangu Serikali ianze kuboresha hospitali za wilaya, kwa kweli sisi hasa katika Jimbo langu la Arumeru Magharibi hatukuweza kubahatika kupata hizo fedha za kwa

ajili ya kuhakikisha hospitali hiyo inakaa katika mkao sasa wa kuitwa hospitali ya wilaya.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala hili liko katika Wizara mbili kwa maana ya TAMISEMI na vile vile katika Wizara ya Afya kwa maana ya upande wa vifaa tiba. Nalizungumzia kwa ujumla wake ili Mheshimiwa Waziri wetu wa Afya aweze kuona namna gani atahakikisha tunapata *x-ray*, lakini pia tunapata na vifaa tiba vingine vyote ambavyo vinatakiwa katika hospitali hiyo. Upande wa majengo, TAMISEMI nao wataona jinsi ambavyo wataboresha hospitali ile kwa sababu sasa umefika wakati muafaka hata katika bajeti nimeona wameiangalia hospitali hiyo na nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la kutoa huduma kwa wazee na watoto; suala hili la kuhudumia wazee wetu halijakaa vizuri kabisa. Kwa bahati nzuri Mheshimiwa Ummy na Dkt. Mollel, ni Wabunge wenzetu, hiki kilio nadhani na wao wanakipata mara kwa mara. Wazee wetu wanakwenda pale hospitalini, wanaandikiwa barua wanakuwa labda na hiyo sijui ndio vitambulisho wanapewa halmashauri, lakini wanapoenda pale wanaambiwa dawa zenu hazipo.

Mheshimiwa Spika, wale wazee wanateseka, kwa kweli wazee wetu wanateseka. Kwa hiyo, naomba kuishauri Serikali kama itawezekana na naomba iwezekane kwa sababu wale wazee wametumika Taifa hili kwa umri wao wote huo ambao mmeuona na sisi sote siku moja tutakuwa wazee na hapa tunaelekea kuwa wazee sasa. Kwa hiyo tunahitajika kuhakikisha kwamba tunaanzisha msingi wa kuendelea kuwatunza wazee wetu.

Mheshimiwa Spika, niombe Wizara iangalie namna ya kuwasaidia wazee. Aidha, wawape kabisa *CHF* moja kwa moja ili ijulikane kwamba wakienda pale, basi Serikali ndio inatoa hiyo ruzuku kwa wazee. Hebu tulione hili kwa kweli kwa sababu linaumiza na linatesa sana wazee wetu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la upungufu wa watumishi. Kuna upungufu wa watumishi katika zahanati zetu, hospitali zetu za wilaya na na kadhalika. Kwa hiyo, naomba waliendelee kuliangalia suala hili pamoja na kuishukuru Serikali kwamba imetangaza ajira hizi za juzi, lakini bado upungufu ni mkubwa sana katika hospitali zetu.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la ununuzi wa madawa na vifaa tiba. Katika sehemu hii inatakiwa sana Mheshimiwa Waziri wakae waangalie namna ya kuhakikisha kwamba watakuja na *strategy* mpya kwa sababu, kwa mfano, juzi katika Jimbo langu la Arumeru Magharibi, Halmashauri ya *Arusha DC*, Serikali imetoa fedha kwa ajili ya kununua vifaa tiba tangu Mwezi wa Tisa mwaka jana. Mshitiri anasema kila siku hakuna vifaa, hakuna vifaa mpaka juzi mwezi Machi ndio vifaa vimekuja kupatikana, *can you imagine*? Ina maana hiyo *variation* lazima bei zinapanda, kuna vitu ambavyo vitakuwa havijanunuliwa na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili eneo la Mshitiri na kuimarisha *MSD,* hebu wakae vizuri waangalie kwa umakini na umahiri zaidi, kwa sababu kwa kweli tutatesa wananchi wetu na hata ukizingatia Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika ukurasa wa 138 imeeleza kinaga ubaga na dhahiri shahiri kwamba, naomba kunukuu; "Kuimarisha Mfumo wa Mshitiri ili kuhakikisha kuwa bidhaa za afya zinapatikana kwa uhakika na kwa gharama nafuu katika ngazi zote za huduma". Hiyo ni Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2020-2025.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika suala la upungufu wa magari katika Halmashauri yetu ya *Arusha DC*, Jimbo la Arumeru Magharibi. Tunaomba Serikali itakapokuwa imekamilisha ugawaji wa *ambulance*, Jimbo la Arumeru Magharibi tuna zahanati nyingi, tuna vituo vya afya vingi, jiografia yake imekaa katika mazingira ambayo kwa kweli ni changamoto sana. Kwa hiyo naomba sana watukumbuke

katika kupata gari la wagonjwa. Hasa gari mbili tukipata angalau itakuwa imetusaidia sana na imetufaa sana kuwaokoa wale wananchi katika kuhakikisha wanapata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho; suala la maadili kwa Madaktari wetu, lakini kabla sijasema maadili, niombe Wizara pia muangalie namna ya kuwawezesha Madaktari na Wauguzi katika mishahara yao, posho zao na mambo yote yanayowahusu. Naomba sana waangalie hili kwa sababu yawezekana pia katika changamoto tunazozisema inawezekana na yenyewe ikawa ni changamoto kubwa. Kwa sababu mtu anapochoka hata hapati *overtime*, hapati chochote anajitoa, ana-*toil* lakini mwisho wa siku hapati stahiki yake ambayo anastahili. Kwa hiyo naomba sana tuangalie Madaktari wetu, wanaoshika roho zetu, wanaoshika afya ya Taifa hili, ili waweze kupata stahiki zao kwa kiwango kinachotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa muda naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi na Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga ajiandae.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mungu kwa kunipa kibali cha kusimama katika Bunge lako tukufu na pia nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuichangia katika Wizara hii ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na kumpongeza Rais wetu kipenzi, Daktari Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea pesa nyingi katika Mkoa wetu wa Kagera na ndoto yake ya kupunguza vifo vya akinamama na watoto Tanzania inawezekana, hongera sana Mama yetu, tunazidi kukuombea afya kila iitwapo leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Waziri wa Afya, dada yangu Ummy pamoja na Naibu wake Dkt. Mollel na Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Afya kwa kazi nzuri wanazozifanya, hakika wanatutendea haki. Sasa naomba nijielekeze kwenye mchango wangu, Mkoa wetu wa Kagera halmashauri sita, zimekamilisha ujenzi wa hospitali, Katoke Biharamulo, Bujinangoma *Bukoba DC*, Bulembo Misenyi, Karagwe, Kyerwa, Ngara Rusumo. Pia kuna vituo vya afya na zahanati zilizokamilika zinahitaji vifaa tiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizi hospitali zimekamilika, lakini vifaa tiba imekuwa ni changamoto kubwa sana, pamoja na wataalam wa afya ili ziweze kuanza kutoa huduma. Kwa hiyo, naomba Serikali yangu Tukufu iweze kuleta vifaa tiba vya kutosha katika hospitali hizi pamoja na wataalam ili kuweza kuwasaidia wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika hospitali na vituo vilivyokamilika, tunahitaji ujenzi wa nyumba za watumishi wa afya ili kuwezesha kutoa huduma Madaktari Bingwa kwa muda wa saa 24. Kwa mfano, mgonjwa pale anaweza akaja mama mjamzito anakuja kujifungua anafika pale kituoni daktari yuko mbali, lakini tukiwa tumejenga pale nyumba ina maana Daktari atakuwa pale masaa 24. Kwa hiyo vifo vitapungua havitakuwepo kabisa kwa mama wajawazito pia na watoto na wazee. Nilikuwa naomba hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wetu wa Kagera katika mipaka yetu kuna mapungufu makubwa ya namna ya kudhibiti magonjwa hatarishi. Tunaomba kujengewa majengo ya *medical department*, *insulation* na kadhalika ili huduma za afya katika mipaka yetu ya Mtukula, Chamchusi, Bugango, Msagamba, Igoma, Rusumo na Kabanga ili kudhibiti magonjwa hatarishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wetu wa Kagera uko katika mlipuko wa majanga mengi. Kwa hiyo tunahitaji kujengewa

kituo cha ufuatiliaji wa matukio ya mlipuko, kwa mfano *ebola, marburg,* surua, polio na *yellow fever* pamoja *Covid*, kwa sababu tumepakana na mipaka na nchi zetu jirani. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali yetu iweze kutuangalia kwa jicho la huruma katika Mkoa wetu wa Kagera.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wetu wa Kagera tuna visiwa 38, visiwa vitano tu ndio vina zahanati. Mama wajawazito visiwani hawana pa kujifungulia ili kunusuru uhai wao, tunaomba Serikali yetu itununulie *ambulance boat* ili kuwezesha dharura za matibabu kutoka kwenda visiwa vingine. Kwa mfano mgonjwa mwingine yuko mahututi ili kumtoa katika visiwa vile aje katika hospitali ya rufaa. Kwa hiyo, naomba sana kwa Waziri, dada yangu Ummy tupate hiyo *ambulance boat* ili kuweza kunusuru uhai wa wananchi wetu wa Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wetu wa Kagera umeanza upanuzi wa hospitali ya rufaa ya mkoa kwa kubomoa majengo chakavu. Sasa hivi tumeanza kujenga maghorofa, tuliahidiwa kuletewa bilioni tatu ili kuweza kumalizia. Kwa hiyo, tunaomba hela ije kipindi hiki ili tuendelee na ujenzi wa *OPD*, wodi za watoto na wodi za wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yangu ni hayo machache, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete ajiandae.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami kwanza nianze kumshukuru Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama kwenye Bunge lako Tukufu hili katika Bunge hili la Bajeti leo ikiwa mara yangu ya kwanza kusimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na kukupongeza sana kwa uendeshaji wako wa Bunge pia napenda nimshukuru Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, pongezi hizi nampa kwa yale yote aliyoyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitembea nchi nzima kuitangaza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025, katika ukurasa wa 124 mpaka 141 wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Rais wetu ameitekeleza kwa vitendo. Ninasema hivyo katika ukurasa wa 31 wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kifungu cha 88 kuanzia kifungu kidogo (a) mpaka (k) ameonesha Ilani ile kwamba kutafanyika ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya, ujenzi wa hospitali za Wilaya, ujenzi wa hospitali za Mikoa, ujenzi wa hospitali za Kanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hayo yote Mheshimiwa Rais wetu ameyaweza. Pia ameeleza upatikanaji wa vifaatiba, kusafisha damu, *dialysis, CT scan, MRI.* Hivyo vyote vitafanyika katika sekta ya afya na hayo Mheshimiwa Rais ameyatekeleza kwa vitendo. Pia ameeleza katika ilani hiyo hiyo kuongeza watumishi katika kada ya afya. Hilo linaendelea kutekelezwa lakini limeanza kutekelezeka kwa hayo yote pia amesema matibabu ya kibingwa yapatikane ya figo, moyo, uzazi (kupandikiza uzazi). Hayo yote ndugu zangu yanatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakina mama tulikuwa na changamoto kubwa ya uzazi kuita ugumba, sasa hivi uzazi unapandikizwa katika hospitali zetu za Dar es Salaam za Tanzania, wanapandikiza uzazi kwa akina mama na tunaweza kupata watoto na jambo la ugumba sasa limeondoka. Hayo yote ni makubwa ambapo ameyafanya Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo anayoyafanya kwa kweli tunastahili tumpongeze na tunampongeza sana sana sana kwa sababu ameweza yale aliyoyataka kuyatekeleza, ameyasimamia na yametekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo napenda sasa nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake Waziri, kwa kazi kubwa anayoifanya. Ni Waziri mahiri na Naibu Waziri mahiri wana ushirikiano mzuri kwa kweli tunashukuru. Pia watenda kazi Waheshimiwa Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa pamoja wanafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nirudi katika mchango wangu. Mchango wangu nitaanza na Hospitali ya Muhimbili. Kwa kweli mambo mazuri yanafanyika katika Hospitali ya Muhimbili na niipongeze sana Serikali. Nilisimama hapa kuomba wodi ya wagonjwa wa akili Muhimbili kwamba imeachwa ikiwa chakavu, chafu haijapata urekebisho. Hivi ninavyokwambia, wodi imekarabatiwa vizuri bado sehemu chache. Kwa maana hiyo Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi ni sikivu, inachukua maoni yetu na inayafanyia kazi. Wodi ile iko vizuri bado asilimia kama 20 tu kukamilika kabisa. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia katika Mfumo mzima wa matibabu. Katika Hospitali ya Muhimbili kumekuwa na mabadiliko na mageuzi makubwa. Mimi nikiwa nje alikuja binti kuniambia amesema mimi nimelazwa pale Muhimbili lakini nilipotoka mama nakwambia angalia baada ya miaka miwili tutazungumza mengine Muhimbili tutakuwa kama India labda. Baada ya miaka miwili mambo niliyoyaona ndani, ananiambia binti tu kama wa miaka 28 umeona nini ananiambia mama siyo ile Muhimbili unayoijua wewe. Muhimbili imebadilika, ina mambo mazuri, ina matibabu mazuri. Kwa hiyo, mimi nalipongeza na wananchi wanapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo iko changamoto Muhimbili. Changamoto ni wananchi wanaoenda kuangalia wagonjwa bado hawajapata sehemu sahihi ya utulivu. Kule kunakuwa na wagonjwa wengine mahututi hawajiwezi. Mgonjwa wako akiwa mahututi huwezi kuwa na akili ya kukaa nyumbani, kwa vyovyote utakuwa mazingira yale yale unasubiri. Sasa pale unaposubiri inakuwa tatizo. Niiombe Serikali itenge eneo maalum, wale watu wanaosubiri wagonjwa wao wakae huko, wakisubiri wagonjwa wao baada ya masaa matatu manne kwenda kuwaona. Kwa kawaida sisi Waafrika tunafarijika zaidi unapougua ukimuona ndugu yako wa karibu. Utapewa matibabu ya kila aina, utapewa kila huduma na Nesi lakini ukimuona ndugu yako wa karibu unafarijika zaidi. Hivyo hilo nalo tulizingatie kwa sababu wale wagonjwa wanakuwa wanahitaji *counsel* na kuwa-*counsel* kwa kwanza kumpa mtu ambaye anampenda ili aweze kupata nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naipongeza kuna wodi maalum ya wazazi ambayo imeanza kuzingatia, wao wanakwenda na wenza wao na watu wa kuwahudumia, iko pale Muhimbili hapa jirani na kanisani hapa, kuna wodi nzuri tu ya wazazi lakini bado ni ya kulipia, tumeanza ninayo imani huko tunakoenda tutaangalia mifumo hiyo, kwa sababu hata tunapoenda kwenye nchi za wenzetu mgonjwa amelala pale lakini hapa kunakuwa na kochi la muuguzaji anamuangalia mgonjwa wake. Najua tulikotoka ni mbali na tunakoenda ni mbali. Hapa tulikofika siyo haba, tunamshukuru Mungu kwa yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie Taasisi ya Afya ya *Ocean Road* ya kansa. Taasisi ile imekuwa na ongezeko kubwa la wagonjwa siku hadi siku, imekuwa na changamoto kubwa ya ucheleweshaji wa vifaa vya matibabu kutokana na taratibu za kikodi. Sasa niiombe Serikali kuwa ile taasisi inategemewa na watu wengi na

tunaona wakina mama ndiyo wanaongoza kwenye kuwepo pale wagonjwa wa kansa ya kizazi, lakini pia zaidi siyo kina mama hata akina baba kansa ya tezi dume inazidi kushamiri ukienda unawakuta wengi tu pale wana matatizo hayo. Sasa vifaa vile tunavihitaji kwa afya, inakuwaje tena kunakuwa na tatizo la kikodi?

Mheshimiwa Spika, Serikali iweke mifumo sahihi na iliyo wazi. Leo tunakwenda kununua wenyewe kwa fedha zetu za Tanzania, tunaenda kununua vifaa nje tulete kwenye hospitali yetu ya *Ocean Road* vinakwama, je, Mfadhili akitaka kutuletea vifaa ndiyo vitaingiaje kama sisi wenyewe vina kwama kwa matatizo ya kikodi. Naomba hilo mliangalie Serikali na Wizara ya Fedha tunavihitaji, tatizo la kansa ni kubwa watu wanahitaji huduma hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nije kwenye hospitali ya Mloganzila, kwa kweli tunashukuru sana hospitali ipo nzuri lakini nayo changamoto yake kubwa ni gharama za matibabu. Wagonjwa, mtu anaumwa akiulizwa unanipeleka wapi? Mlaganzila, aah! naenda kufa mama, nini? Watoto wangu wataweza hizo bili? Eeh! Ile hospitali hivi mfumo wake hasa wa *bill* ukoje? Mbona watu wanashindwa kuelewa? Kwa sababu mwisho wa yote mtu yule anaugua, anakufa, maiti inakwama, Mbunge hukai Bungeni, unahangaika, unateseka, unaambiwa ukamkopeshe mtu hela za kwenda maiti, nazipata wapi ghafla shilingi milioni saba, nane? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali siyo Mloganzila tu, Muhimbili, Mloganzila ituwekee mpango sahihi juu ya hizi tiba, watu wanakwama, kila ukienda yaani mpaka tunaogopa, ukifika Muhimbili tu ukienda maeneo ya watu wengi utakumbana na tatizo hilo. Ukiwa Bungeni utakumbana na simu hizo. Kweli tunakwenda pale, wengine tunawaelezea lakini wako watu ambao hamjui hata Mbunge wake, hivi huyu anatokaje?

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali iweke utaratibu mzuri utakaoeleweka, kwamba huyu mtu ana uwezo na ikiwezekana mtu aambiwe mapema, umeingia hapa kwenye wodi hii itakubidi ufanye hivi, uweke *advance* hii ili hapa ukitoka tena isiwe tatizo. Ninaona Mheshimiwa Waziri unatoa taarifa, unajitahidi kutoa taarifa, jamani maiti isizuiwe lakini inafika sehemu hali ni ile ile. Sasa hii kitu sisi kama wananchi tunafanyaje kutoka hapo?

Mheshimiwa Spika, sasa nije kwenye suala zima la afya ya mama na mtoto. Mimi niombe Serikali….

**SPIKA:** Dakika moja malizia kengele imeshagonga ya pili.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, namalizia mchango wangu. Naiomba Serikali iangalie huduma ya afya ya mama na mtoto iwe bure, bure ya kweli. Mama kliniki afanye bure, kwa sababu hata wanaoenda na bima unachajiwa. Sasa kwa nini na sisi tunataka afya ya mama na mtoto iwe bure kwa wote?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga atafuatiwa na Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe ajiandae.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Wizara hii ya Afya. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia afya ya kuweza kusimama tena kwenye Bunge hili nikichangia katika Wizara hii ya Afya.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ushauri kwa Serikali kupitia Wizara hii ya Afya. Kumekuwa na ujenzi wa hospitali za Wilaya, kumekuwa na ujenzi wa vituo vya afya, kumekuwa na ujenzi wa zahanati nyingi sana ambazo ukipita kwenye Halmashauri mbalimbali hospitali hizi za Wilaya hazifanyi kazi, vituo vingi vya afya havifanyi kazi, zahanati nyingi hazifanyi kazi kwa sababu hazina vifaatiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi niombe sana, nafikiri kwamba hii kasi ya Mheshimiwa Rais anayoenda nayo ya kuweka miundombinu ya afya muende nayo na nyinyi sasa Wizara ya Afya kwa kupeleka vifaatiba pamoja na Madaktari na Wauguzi katika hospitali zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ukizunugumza kwamba kuna hospitali za Wilaya, kuna vituo vingi vya afya kama havifanyi kazi, wananchi hawa hawawezi kuona tija ya hivyo vituo vya afya na hizo hospitali za Wilaya ambazo zinajengwa. Kwa hiyo, niombe sana kupitia Bunge lako Tukufu, Wizara hii sasa ijikite zaidi katika kupeleka vifaatiba, kupeleka Madaktari pamoja na Wauguzi ili majengo haya yaweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majengo ni mengi mno tumeyaona na tumeshuhudia lakini hayana vifaatiba wala hayana Madaktari, maeneo mengine yanavyo vifaatiba lakini hayana wataalam. Unafika unakuta mitambo imefungwa hapo, iko vizuri imekaa sawa sawa hakuna wataalam. Unauliza huu mtambo umefungwa lini? Una mwaka mzima hakuna mtaalam, huu mtambo umefungwa lini? Una miezi sita hakuna mtaalam.

Mheshimiwa Spika, tumekwenda Halmashauri ya Sumbawanga Mjini kuna kifaa kipo zaidi ya miaka miwili sasa hakijawahi kufanyakazi wala kufunguliwa kule kwenye makaratasi. Sasa hii ni kitu gani? Mimi naomba tuwe tunaangalia zaidi vipaumbele vyetu hasa kwenye afya ni kitu

gani ili tuweze kusaidia wananchi wetu, tuendane sawa na kasi ambayo anakwenda nayo Mama ya kuhakikisha kwamba watu wanapata huduma za afya, basi huduma za afya zipatikane kwa tija inayohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala zima la dawa. Mheshimiwa Waziri amekuwa mara nyingi sana hapa akizungumzia suala la dawa, kwamba sasa hivi hakuna shida ya dawa. Inawezekana hakuna shida ya dawa lakini dawa zinazotakiwa katika maeneo yale ndiyo zinazokosekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unakuta kuna hospitali haina *panadol,* unashangaa mbona Waziri kasema pale kuna madawa, hata *panadol* kweli hakuna? Lakini utakuta kuna dawa zinawekwa kwenye hospitali husika hazina hata watumiaji mpaka zina *expire*. Kwa nini tusiangalie uhitaji wa dawa zinazohitajika kwenye hospitali zetu na kwenye maeneo yetu ili tupeleke zile dawa zinazohitajika, wananchi waweze kupata huduma ya dawa kuliko ilivyo hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumetembea kwenye hospitali mbalimbali tumekuta dawa zime-*expire* ziko pembeni zinatakiwa zitupwe lakini ukiwauliza naomba *paracetamol* hakuna, naomba *cetirizine* hakuna. Sasa tunaomba sana muangalie ni dawa gani ambazo zinahitajika kuchukuliwa ili wananchi wetu waweze kupata huduma inayostahiki kuliko ilivyo hivi sasa kupeleka tu dawa bora mmepeleka dawa mwisho wa siku dawa zile hazifanyi kazi na matokeo yake zinaharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia kuhusiana na suala zima la maradhi haya ya kansa. Hili jambo limekuwa ni janga tena ni janga kubwa sana hasa kwetu sisi wakina mama. Kansa hasa za shingo ya kizazi zimekuwa ni nyingi mno, kiasi kwamba mwanamke mpaka uje ujigundue

kwamba una kansa ya kizazi hasa wanawake wetu wa maeneo yetu ya vijijini kupima ni kwa nadra. Unakuta imeshafika *stage* ambayo haiwezekani tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi natokea Mkoa wa Tabora. Katika Mkoa wetu wakina mama wengi sana wanapata matatizo hayo, mwisho wa siku anapopata tatizo hili hana pa kwenda kukimbilia, anaambiwa aende Bugando ama aje hapa Benjamini Mkapa. Ni wangapi ambao wanao uwezo wa kufika kwenye maeneo hayo? Kwa hiyo, unakuta mama huyo mpaka tayari *stage* yake imefika mbaya anaelekea kufa unaweza ukamsaidia lakini unamsaidia wakati tayari hali imeshakuwa mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe sana, kwanza elimu inahitajika sana hasa kwa wanawake wetu maeneo ya vijijini kuhusiana na hili janga. Sisi wa mjini angalau tunajua kama nitakwenda hospitalini naomba mni-*check*, mni-*check* matiti, mni-*check* na kizazi nitaangaliwa na nitakutwa labda niko salama ama nina dalili za huo ugonjwa lakini wenzetu kule ni ngumu sana. Kwa hiyo, niombe sana Wizara ya Afya mfanye kazi ya ziada tusaidie wanawake hawa wanakufa sana, pamoja na hizo tezi dume zinazosemwa lakini kwa kweli kansa za wakina mama zimekithiri sana maeneo mbalimbali katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe sana tupelekewe na sisi basi hivi vifaatiba vya kansa pale katika Hospitali yetu ya Kitete katika bajeti hii, tunawaomba jamani mtusaidie. Hawa wanawake tuweze kuwaponya ili angalau na wao sasa waweze kupata nafuu na kujua kwamba wanapata huduma ile maeneo yale.

Mheshimiwa Spika, Tabora imefunguka, barabara sasa hivi zimefunguka, kila sehemu magari yanapita yanaingia. Tusaidieni basi ili angalau watu wa kutoka hata kwenye

Wilaya za karibu waweze kufika pale kwenye hospitali yetu ya Kitete waweze kupata huduma hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nifahamu kuhusiana na suala la Bima ya Afya hasa kwa Watoto, imekuwa kero kubwa sana. Hatuelewi, hatujui tushike wapi. Ukiwauliza wanakwambia, kuna siku nilimuuliza Naibu Waziri akaniambia inabidi mzazi amsajili na mtoto wake kwenye bima yake. Mimi mtoto wangu ameshakuwa mkubwa lakini kuna watu ambao wana watoto wana miaka mitano. Huyu mtoto analipa wapi na bima yake imesha-*expire?* Hebu tunaomba Mheshimiwa Waziri unapokuja hapa, utoe majibu yatakayowaridhisha wananchi huko waweze kujua, mtoto wa kuanzia mwaka mmoja mpaka mitano ambaye bima yake imesha-*expire* anatakiwa afanye nini ili aweze kupata bima ya afya? Kwa sababu ukisema ni shule, shule gani anasoma mtoto huyu, kwamba labda ataenda kusajiliwa shuleni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaomba mtoe maelezo basi yatakayowasaidia huko wazazi wengi, au kama ni kulipa hiyo shilingi 190,000 semeni. Mzazi lipa shilingi 190,000 mtoto wako aweze kupata huduma ya afya vieleweke kuliko kuwa mnafumba fumba na kusema kwamba watu wote wasajilini watoto kwenye mashule yao. Shule gani wengine watoto wadogo bado hawaja anza hata hizo shule? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up* hapa, atupe majibu ya kuhusiana na hili suala la bima ya afya hasa kwa hawa watoto wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na madeni pia makubwa sana katika Wizara hii ambapo hospitali nyingi sana za Kanda na hospitali za Mikoa zina madeni yaliyokithiri. Niombe sana Wizara ya Fedha pelekeni fedha wenzenu waweze kulipa madeni haya. Saa zingine kuna huduma nyingine zinakwama

kwa sababu ya madeni makubwa ambayo wanayo katika hospitali zetu za Kanda na hospitali zetu za Mikoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya *CAG* ya Hesabu za Serikali Kuu ya mwezi Machi, 2023, Wizara ya Afya ina madai ya zaidi ya shilingi bilioni 9.21. Madai hayo yanadaiwa katika hospitali ya Rufaa ya Apollo. Inaonekana kwamba kuna baadhi ya wenzetu Serikalini wanatibiwa huko, kwa hiyo kuna madeni hayo ambayo yanadaiwa kwa mujibu wa Taarifa ya *CAG* ya Machi, 2023 muende mkaipitie muione. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hospitali zetu 33 za Rufaa na za Mikoa kuna madeni ya jumla ya zaidi ya shilingi bilioni 34.02. Hizi fedha ni nyingi sana na hapa hata ukizitoa, haya ni madeni ya muda mrefu zaidi ya miezi 12 madeni haya wala hayana mpango wa kulipika.

Mheshimiwa Spika, nitoe tu mfano wa hospitali chache hata hii hospitali yetu mnasema Mirembe mimi najua bado Mirembe sijajua kama tayari imeshabadilishwa lakini ina deni la zaidi ya shilingi bilioni tatu. Kuna Hospitali ya Kanda ya Mbeya ina zaidi ya deni la shilingi bilioni tatu. Dodoma hapo hospitali ya *General* zaidi ya shilingi bilioni 2.8. Hata hospitali ya Mkoa wa Tabora Kitete ina zaidi ya deni la shilingi milioni 948. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Wizara ya Fedha iweze kusaidia haya madeni kuondoka ili watu waweze kupata huduma zinazostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona umeshika *mic* naona muda wangu umeisha. Nakushukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete atafuatiwa na Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel ajiandae.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu sana katika maisha yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya katika nchi yetu. Pia nampongeza Waziri wa Afya, dada yangu Ummy Mwalimu, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel na wafanyakazi wote wa wizara hii kwa jinsi wanavyoendelea kupambana kumsaidia Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kumpongeza sana Mama Samia Suluhu Hassan kwa juhudi kubwa alizozifanya katika Mkoa wetu wa Mara. Mheshimiwa Rais alikuja mwaka 2022 katika Mkoa wa Mara, tulimwomba *CT-Scan,* akaahidi atatekeleza. Sasa ametekeleza, ametuletea *CT-Scan Machine*. Tunamshukuru sana, sana, sana kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Mara na Watanzania wote wanaoishi Mara. Kwa sababu ile mashine ni muda mrefu haikuwa kuwa katika mkoa wetu na wananchi wa Mkoa wa Mara walikuwa wanatoka Mara kwa gharama kubwa kwenda kutafuta huduma hiyo katika Mkoa wa Mwanza katika Hospitali ya Bugando. Hivyo tunamshukuru sana sana Mheshimiwa Rais kwa juhudi hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto iliyoko tu pale, kuna miundombinu ambayo haijamalizika, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, ile miundombinu imalizike ili kusudi ile mashine iweze kufungwa na wananchi wale waweze kupata huduma hiyo inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, niendelee kumpongeza Rais wetu kwa jinsi alivyoendelea kutujengea vituo vya afya, hospitali, zahanati na hospitali za mkoa. Mkoa wetu wa Mara, vituo

vya kutolea huduma ambavyo vimejengwa, tuna vituo 335. Hivyo ni kwa ujumla wa hospitali na vituo vya afya na zahanati. Katika vituo 335 tuna vituo 35 tu ambavyo ndiyo vinakidhi mahitaji ya Wana-Mara ambavyo vinalaza wagonjwa, vinatoa huduma ya damu na upasuaji.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia uwiano, ni mdogo sana. Huo uwiano kwa Mkoa wa Mara, kwa mwaka mzima wanajifungua akina mama 93,339. Unapojifungua, lazima upate huduma inayostahiki. Vile vituo ambavyo vimejengwa, havina sifa, kwa maana ya kwamba havina vifaa tiba, havina madaktari na havina madawa.

Mheshimiwa Spika, nitatolea mfano, Kituo cha Afya cha Mliba, ambacho kilijengwa mwaka 1985, lakini kinahudumia kata saba; Kata ya Nyanungu, Kata ya Golong'a, Kata ya Kwihancha, Kata ya Nyarukoba, na kata nyingine. Siyo kwamba zile kata ziko karibu, umbali ni mrefu. Mgonjwa anatembea kutoka kilometa 50 kuja tu pale kwenye kituo, na kurudi pia ni kilometa 50.

Mheshimiwa Spika, kwa uwiano, ukilinganisha ni kilometa kama 100 mgonjwa anatembea, lakini anapofika pale kwenye kituo anakosa huduma stahiki. Kituo hakina *x-ray,* hakina *ultra-sound,* hakina maji, hakina Daktari hata wa Kituo pale hayupo. Mheshimiwa Ummy mimi naamini kazi yako ni nzuri sana, hebu tembelea Mkoa wa Mara ujionee adha wanayoipata pale akina mama wale wa Mkoa wa Mara. Ni mbali sana. Siyo hicho tu, ukienda Wilaya ya Bunda, Kituo cha Bunda Mjini pale hakina uzio, hakina *generator,* hakina *ultra-sound,* wala *x-ray* haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, alisimama hapa Mbunge wa Mwibara, akasema kuna fedha zimeletwa shilingi milioni 300 kwa ajili ya kujenga Kituo cha Kasuguti kule Mwibara, lakini zile shilingi milioni 300 hazijafanya ile kazi iliyopelekewa kujenga jengo la mama na mtoto. Kwa hiyo, Mheshimiwa

Waziri aje kutueleza kwamba zile shilingi milioni 300 mama alizozitoa zijenge jengo la mama na mtoto, lakini hazikufanya hivyo, sasa sijui atatuletea nyingine au atafuatilia zile ili tujue hasa nini hatma ya wale akina mama wa Mwibara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunamwomba sana, sana, sana Mheshimiwa Waziri atuletee madaktari, hasa madaktari bingwa, hatuna. Pia tunaomba sana tuletewe vifaa tiba katika vituo vyetu vya afya na hospitali. Tunakuomba pia tuletewe magari kule kwenye Mkoa wetu wa Mara. Wana-Mara wanampenda sana mama, wanapenda sana nchi yao, kwa hiyo, tunaomba huduma zile ambazo zinaweza kupatikana kwa wengine zipatikane pia na Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee jambo lingine ambalo ninaliona kama ni gumu sana. Kwenye wizara hii kuna Sera ya Afya inayosema, matibabu bure kwa watoto chini ya miaka mitano, wazee na wamama wajawazito. Hili jambo halifanyiki hivyo. Mama zetu, watoto wetu na baba zetu wale wazee ambao ni kuanzia miaka 65 na kuendelea wanapoenda kwenye vituo vile vya afya au hospitali hawapewi matibabu bure wanalipa. Sasa naomba hii sera tujue inatekelezwa vipi?

Mheshimiwa Spika, naomba kuishia hapo, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, na mtoa hoja ajiandae.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Afya. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Neema kwa kunijalia afya na kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Nimpongeze sana Waziri wa Afya, dada yangu

Mheshimiwa Ummy, Naibu Wake, watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuhakikisha Watanzania wanapata huduma bora za afya. Nawapongeza sana sana.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais mnyenyekevu, msikivu, Rais mwenye huruma na mapenzi makubwa kwa Watanzania. Hii imejidhihirisha wazi katika bajeti hii, tumeona namna ambavyo ameweza kuongeza fedha ili Watanzania waweze kupata huduma bora za afya. Mheshimiwa Rais tunakupongeza sana.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii, kwa niaba ya wananchi na wanawake wa Mkoa wa Singida kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa miradi mingi ambayo ametupatia katika Mkoa wangu wa Singida; miradi ya afya, vituo vya afya vimejengwa, Hospitali za Wilaya ya Mkalama, Ikungi pamoja na Hospitali ya Wilaya ya Ilongero ninampongeza sana Mheshimiwa Rais, tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, ningependa kugusia kuhusu Hospitali yangu ya Rufaa ya Mkoa wa Singida. Hospitali hii ujenzi wake umekuwa ni wa muda mrefu sana. Mheshimiwa Ummy, dada yangu amewahi kuitembelea hospitali hii pamoja na Mheshimiwa Dkt. Mollel na viongozi mbalimbali, lakini hospitali hii ya rufaa hadi sasa haijakamilika. Namwoamba sana Mheshimiwa Ummy hospitali hii ya rufaa sasa hivi ikamilike ili wananchi wa Mkoa wa Singida nao waweze kupata matibabu ya kibingwa katika Hospitali hii ya Rufaa ya Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Spika, hospitali hii ikikamilika itaweza kuwahudumia hata wananchi wa mkoa Jirani kama Tabora, Simiyu pamoja na Shinyanga. Naomba sana Serikali itenge fedha ili hospitali yetu hii ya rufaa iweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, pia hospitali zangu za Wilaya ya Singida hazina vifaa tiba vya kutosha na wataalamu. Naomba Serikali iweze kuleta wataalam pamoja na vifaa tiba ili sasa matibabu yaweze kutolewa kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Hospitali yangu ya Wilaya ya Mkalama, Ikungi pamoja na Manyoni zina changamoto kubwa ya watumishi. Naomba mtuletee watumishi. Mkalama ina ukosefu wa watumishi 750, Ikungi ina ukosefu wa watumishi 1,022 na Manyoni kuna ukosefu wa watumishi 350.

Mheshimiwa Spika, kama Wabunge wenzangu walivyotangulia kusema, kwamba uwepo wa majengo mazuri, yanatakiwa pia yawe na vifaa tiba pamoja na watumishi. Pia vipo vituo vya afya, ambavyo ni Sepuka, Mgori, pamoja Msange, havina magari ya kubebea wagonjwa na pia havifanyi upasuaji. Naomba sana vituo hivi vya afya viweze kupata vifaa tiba pamoja na magari ya kubebea wagonjwa ili huduma bora za afya kwa mama na mtoto ziweze kutolewa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa haya machache, naunga mkono hoja na ninaendelea kuwapongeza sana madaktari wote na wauguzi wote kwa kazi nzuri ambazo wameendelea kuzifanya, ni kazi ya thawabu, Mwenyezi Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Afya kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Afya kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Serikali katika utekelezaji wa sera ya afya ikienda sambamba na ustawi wa jamii na maendeleo endelevu na hii ni mojawapo ya nguzo kuu katika utayari wetu wa ushindani wa kimataifa *(national competitiveness)*. Bajeti hii inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Awamu ya Sita, Serikali kupitia Wizara ya Afya, imetekeleza miradi mingi ya miundombinu ya afya. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na kwa kushirikiana na TAMISEMI imeendelea kutekeleza kwa ufanisi mkubwa miradi ya Hospitali ya Wilaya na vituo vitano vya afya vya Kata za Ikukwa, Ilembo, Santilya, Ilungu na Swaya. Vituo vyote vitano vinaendelea kutoa huduma kwa ufanisi mkubwa hasa huduma ya watoto na wakina mama. Hospitali ya Wilaya pamoja na vituo vya afya vimekamilika na maandalizi ya vifaa tiba yapo katika hatua za mwisho ili vianze kutoa huduma kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki tunapopambana na majanga magonjwa ya mlipuko ikiwemo la *corona virus (covid-19),* tumejifunza umuhimu wa utayari wa huduma ya afya hasa kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali na

hivyo Serikali iongeze msukumo wa kupeleka vifaa tiba na kumalizia vituo vya afya na zahanati zilizojengwa kwa nguvu za wananchi. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wananchi wa Kata za Igoma, Isuto wamejenga vituo vya afya na kuna maendeleo mazuri ya kukamilisha na pia Mji Mdogo wa Mbalizi wenye wakazi zaidi ya 150,000 ujenzi wa kituo cha afya haujakamilika.

Mheshimiwa Spika, hivyo napendekeza Serikali kutoa kipaumbele katika bajeti hii kwa vituo vya afya hivi ili vianze kutoa huduma. Pamoja na vituo vya afya vya Ilungu, Igoma, Isuto na Mbalizi, napendekeza kukamilisha zahanati zote ambazo zimejengwa kwa nguvu za wananchi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maboresho ya miundombinu ya hospitali na vituo vya afya, Serikali ihakikishe bajeti ya mwaka huu inaendelea kujielekeza zaidi kwenye ajira ya madaktari na watumishi wa afya kwa ujumla. Pamoja na maboresho hayo ya miundombinu, vifaa tiba na ajira kwa watumishi, napendekeza Serikali ikamilishe mpango kabambe na Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote na hasa kwa wazee na wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali iangalie jinsi ya kuboresha Bohari ya Madawa *(MSD)* ikiwa ni pamoja na Serikali kuhakikisha inaongeza mtaji wa *MSD* na kuboresha muundo wa shirika ili uendane na jukumu kubwa kutoa huduma kwa tija na ufanisi. Katika kipindi hiki ambapo Serikali inaangalia kuanzisha Bima ya Afya kwa Wote, kipaumbele kielekezwe kwenye maboresho ya upatikanaji wa madawa pamoja na madawa na kuwezesha huduma ya hospitali zetu kutoa huduma bora zaidi kwa ukanda huu wa Afrika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Afya, Naibu Waziri, Katibu Mkuu,

Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi kwa kazi nzuri inayoendelea kufanywa katika kuboresha afya za Watanzania, mnafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa jinsi alivyoziwezesha hospitali zetu kupata *ICU, Emergency, Ct-Scan, MRI, Angio Suite, Pet Scan* na vifaa tiba vingine vingi. Nchi yetu sasa imeanza kupokea wagonjwa kutoka nchi nyingine sababu huduma za afya nchini kwetu zimeboreshwa sana. Ahsante sana Rais wetu na mama yetu mpendwa.

Mheshimiwa Spika, kilio kikubwa kilichopo kwenye vituo vya afya na zahanati ni upungufu wa watumishi na ukosefu wa dawa. Wananchi watafurahia uwepo wa majengo mazuri katika vituo vya kutolea huduma za afya kama wakienda kutibiwa watapata huduma nzuri ikiwemo kupata madawa stahiki. Kwa sasa upatikanaji wa dawa ni shida. Ili kuimarisha upatikanaji wa dawa katika vituo vya kutolea huduma ya afya, inabidi *MSD* ipewe nguvu na mtaji wake.

Mheshimiwa Spika, *MSD* inahusika na kununua, kuhifadhi na kusambaza dawa. Lakini *MSD* haina mtaji wa kwake wa kiwezesha kuagiza dawa mapema. Inategemea ipate bajeti ya hospitali na vituo vingine vya kutolea huduma ya afya, ndipo waanze kuagiza *data*. Utaratibu huu unafanya upatikanaji wa dawa unachelewa, sababu taratibu za manunuzi zinachukua miezi mitatu hadi sita. Kuna marekebisho makubwa yamefanyika ndani ya *MSD,* ikiwemo hata kurekebisha muundo. Ili kuisaidia *MSD* iweze kuzifikisha dawa mapema kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na ili *MSD* iweze kujiendesha kibiashara, napendekeza *MSD* ipewe mtaji wake yenyewe. Wakiwa na mtaji wataweza kuagiza madawa mapema na hivyo vituo ikiwemo hospitali, vituo vya afya na zahanati wakiagiza dawa, zitakuwa tayari ziko kwenye maghala ya *MSD* na hivyo dawa zitafikia vituo haraka. Mfumo wa sasa mkipeleke maoteo *MSD* ndipo

inaanza mchakato wa kuagiza dawa na hivyo kuchelewa kuzipata. *MSD* wapewe mtaji wao.

Mheshimiwa Spika, pia Tanzania iliteuliwa kuweza kusambaza dawa katika nchi za *SADC*. Hii ni fursa, nchi yetu inabidi ijitahidi kutoikosa hii fursa. Ni hapo *MSD* itakapopewa mtaji wao wa kutosha wataweza kununua na kusambaza dawa Tanzania na katika nchi nyingine *SADC*.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kagera unapakana na nchi nyingine nne, ni rahisi kupata magonjwa ya kuambukiza na ya mlipuko kutoka nchi jirani kama UKIMWI, Ebola, Marbag na kadhalika. Pamoja na hayo Mkoa wa Kagera hakuna *isolation centres.* Napendekeza zijengwe *isolation centres* katika maeneo ya Bukoba - Muleba, Ngara, Kyerwa na Mutukura ambapo kuna mipaka inayopitisha na kuingiza watu wengi na hivyo kuongeza uwezekano wa kuletwa kwa hayo magonjwa ya kuambukiza na ya mlipuko.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kagera pamoja na kuwa pembezoni na kupakana na nchi nyingine kadhaa, bado hakuna hospitali yenye hadhi ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Hili nimekwishaliongelea sana na nimeahidiwa mara kadhaa lakini fedha za kujenga hospitali yenye hadhi ya Rufaa ya Mkoa wa Kagera haipelekwi. Tunaomba tujengewe hospitali hiyo. Ni lini hii ahadi itatekelezwa?

Mheshimiwa Spika, bima ya afya ndiyo itakayokuwa mkombozi wa Watanzania walio wengi. Gharama za afya ni ghali, Watanzania wengi hawawezi kumudu gharama za matibabu. Ni lini sasa Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote utarudishwa Bungeni ili wananchi waweze kupata bima ya afya na waweze kutibiwa bila kikwazo cha kukosa fedha?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Waziri wa Afya Ndugu Ummy Mwalimu na Naibu wake Dkt. Godwin Mollel na wataalam wa Wizara ya Afya kwa kazi nzuri wanazofanya kwenye kutekeleza wa Ilani ya CCM.

Mheshimiwa Spika, mimi nitachangia kuhusu changamoto ya watu wenye ulemavu na kuhitaji viungo bandia.

Mheshimiwa Spika, hapa nchini kuna wenzetu waliopatwa na matatizo yaliyosababisha kukatwa viungo vya mwili kama miguu na mikono. Watu hawa wamekuwa wakipambana kuirudisha furaha ya awali ili angalau waweze kushiriki mambo mbalimbali katika jamii ikiwa ni pamoja na kufanya shughuli zao walizokuwa wakifanya awali.

Mheshimiwa Spika, Mtanzania yeyote anaweza kupatwa na ulemavu wa kiungo kutokana na sababu nyingi ikiwamo kuzaliwa na kilema, ajali na kuugua saratani au kisukari. Kutokana na hilo, idadi ya walemavu wa viungo vya miguu na mikono imekuwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, viungo bandia vina nafasi kubwa katika kutatua tatizo hilo. Hapa Tanzania ni watu wachache wameweza kupata huduma na idadi ya waliopo nyumbani ni kubwa zaidi kuliko wanaopata huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba ieleweke kwamba kukatwa kiungo siyo mwisho wa maisha au kushiriki katika shughuli za kimaendeleo. Elimu ikitolewa, tafsiri inaweza kuwa tofauti kabisa na kuwarudishia matumaini ya kuishi Watanzania wenzetu waliokata tamaa.

Mheshimiwa Spika, uhitaji wa viungo bandia hapa nchini umeongezeka sana kutokana na ajali zitokanazo na matumizi ya vyombo vya usafiri kama pikipiki ambapo kumesababisha

mrundikano wa wahitaji wa viungo bandia vya miguu na mikono.

Mheshimiwa Spika, waathirika wengi hufika hospitali, lakini wagonjwa hao wanapotajiwa kiwango cha fedha zinazohitajika ili wapatiwe huduma, idadi kubwa huondoka na hawarudi tena kutokana na gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, hospitali chache zenye huduma hizi ni pamoja na *KCMC*, Bugando, Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili *(MOI)* na *Dodoma General Hospital.*

Mheshimiwa Spika, gharama za huduma hii huwa ni kubwa kutokana na bei ya malighafi ambazo huagizwa kutoka nje ya nchi. Kwa mfano, utafiti niliofanya nimebaini kuwa gharama za kuweka mguu (kutegemea na hospitali) ni kati ya shilingi milioni 1.5 hadi 3.5. Mkono ni takribani shilingi milioni mbili hadi 4.5. Gharama hizi ni kubwa sana kwa Mtanzania wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, pamoja na bei kuwa juu, Mfuko wa Bima ya Afya *(NHIF)* hautoi malipo kwa watu wenye matatizo ya kuwekewa viungo bandia. Hii imekuwa ni changamoto kubwa hasa kwa watoto wanaokua, kwani huhitaji kabadilishiwa viungo mara kwa mara kila maumbile yao yanapobadilika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naishauri Serikali yafuatayo; kwanza naishauri Serikali kuandaa sera zitakazowezesha upatikanaji wa viungo hivyo kwa urahisi kutokana na hali ya uhitaji kuongezeka.

Pili, naishauri Serikali ijumuishe huduma hizi katika Bima za Afya *(NHIF)* ili watu waweze kupata huduma hiyo kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, tatu, naishauri Serikali ifanye tafiti ili kuwa na kanzidata ya waathirika na wahitaki wa viungo bandia.

Nne, naishauri Serikali kupitia vyuo vyetu hapa nchini izalishe idadi ya wataalamu watakaokidhi hitaji la kutoa huduma kwa wahitaji wa viungo bandia hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, tano, naishauri Serikali ipeleke huduma ya viungo katika hospitali zote za mikoa hapa nchini.

Sita, naishauri Serikali ihamasishe wadau kuanzisha vituo vya kutengeneza viungo bandia katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Saba, naishauri Serikali iwapatie ajira vijana wahitimu wa fani ya viungo katika maeneo mbalimbali hapa nchini; na nane, nishauri Serikali itoe elimu kwa uMma kuhusu uwepo wa viungo bandia ili wanufaike na huduma hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Spika, ninapongeza kwa juhudi zote zinazofanywa na Serikali katika kuimarisha afya nchini. Ombi langu tunaomba wale wataalamu waliohitimu katika Kituo cha Sekomu Lushoto, Tanga, kama *Mental Health and Rehabilitation Officer,* wapo kama 143 nchi nzima, watambuliwe kwenye Muundo wa Kazi au *Work Scheme* ili waweze kuajiriwa kwa utaalamu wao. Kwa sasa wanafanya kazi kwa taaluma au madaraja mengine kama Maafisa Tabibu ngazi za Wilaya ambayo sio yao kwa sababu ya kukosa muundo huu.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba kuwasilisha.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Waziri wa Afya Mheshimiwa Ummy Mwalimu na wote wanaomsaidia wakiwemo madaktari na wauguzi wote wa Wilaya ya Nyasa.

Mheshimiwa Spika, maoni yangu; kwanza fedha inayotengwa itolewe kama ilivyokusudiwa; pili, Serikali iweke jitihada kubwa katika kutoa kinga na pia kutoa mafunzo ya ujuzi kwa mabwana na bibi afya ili kuifikia jamii kubwa zaidi. Lakini kuhusu kuwatumia waliomaliza kidato cha nne ni vema kuwatumia waliopata ujuzi wa vyeti vya fani za utabibu na afya pamoja na kuwaongezea ujuzi huo unaohitajika. Hao wapo wengi huko vijijini.

Tatu, Wilaya ya Nyasa inaomba vifaa tiba muhimu *x-ray, utra sound, ambulance* na fedha za vifaa vya vituo vya afya na zahanati zilizikamilika Vituo vya Afya Kingirikiti na liparamba.

Mheshimiwa Spika, nne, Hospitali ya Wilaya ya Nyasa imeshaanza kutoa huduma za afya ya kinywa. Changamoto ni hakuna vifaa tiba kabisa. Tunaomba ahadi ya kupatiwa shilingi 50,000,000 tuliyoahidiwa; tano, Wilaya ya Nyasa ina upungufu mkubwa wa watumishi wa afya, ni vema Wizara iwaongeze watumishi wa afya.

Mheshimiwa Spika, sita, kwa nini Serikali isifikirie kuwa na mfuko maalum wa tozo angalau shilingi mia moja tu kwa ajili ya kupunguza changamoto ya kifedha hasa katika kuboresha huduma za afya vijijini na kwa magonjwa maalum kama saratani, figo na kadhalika, tukubali kukata kupitia mafuta au mawasiliano. Najua changamoto zake, lakini tukiamua inawezekana. Tusijifungie kwenye bima ya afya tu. Afya ya mtu ni utu na heshima ya uhai. Inaumiza sana kuona mtu anapoteza maisha kwa ajili ya kukosa uwezo wa kifedha. Umuhimu wa uhai hauchagui hali ya kiuwezo wa kifedha.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nachukua nafasi ya kuwasilisha mchango wangu kwa hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Afya. Namshukuru Mungu kwa hatua hii ya kusimama mbele ya chombo chetu muhimu kupaza sauti.

Mheshimiwa Spika, napenda kwa dhati nimpongeze Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitahada zake na umahiri anavyosimamia ustawi wa nchi na wananchi wake kwenye nyanja zote ikiwemo uchumi, mahusiano na mashirikiano.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi anavyosimamia shughuli za Serikali kwa ufanisi mkubwa. Hali kadhalika nafurahia na kujivunia umahiri na usimamizi wa viwango wa Spika wetu katika kusimamia majukumu yake kulipaisha Bunge letu sio ndani ya Tanzania bali kimataifa, nampongeza sana Mheshimiwa Spika, Dkt. Tulia.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu naanza pia kuthamini kazi safi inayopimika na inzayokidhi haja inayosimamiwa na Waziri Ummy na watendaji wote wakiongozwa na madaktari, wauguzi na wadau wote katika sekta hiii ya afya.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunakwenda kupaa katika Bara la Afrika kwa vile huduma zetu za afya zinavyoendelea kuboreka na kuwa za kisasa zaidi tumevunja kioo.

Mheshimiwa Spika, leo Madaktari Bingwa wetu wameweza kufanya *operation* nzito kama ya kupandikiza Uloto. *Operation* za kupandikiza figo na *operation* za moyo na nyingine kwa utaalamu wa hali ya juu bila kupasua sehemu kubwa.

Mheshimiwa Spika, madaktari mabingwa na timu nzima hizi kwa hakika waonwe na watazamwe kimaslahi zaidi. Watu hawa wanafanya kazi sana wanastahili kupata mafungu yaliyoombewa fedha bila kikwazo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono na kupongeza dhamira ya kuifanya Hospitali ya Mirembe kuwa taasisi. Kwa jinsi mahitaji ya huduma yanavyoongezeka na watu wanavyozidi kuwa wengi uwepo wa taasisi unakwenda kuwapunguzia wananchi usumbufu wa kusaka huduma.

Mheshimiwa Spika, tunashaka kwamba matatizo ya afya ya akili yanamea kwa *speed* na hivyo vitendo vinavyofanywa na kuvunjwa kwa maadili na udhalilishaji na hata ubakaji vinaweza kuhusishwa na mtiburiko wa akili.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara ikasomesha wataalamu wengi wa fani hii *Psychologists Counsellor* na kuwapa kazi ya kuwashughulikia waathirika badala ya kuwatumia *social workers.*

Mheshimiwa Spika, wapo wagonjwa wa afya ya akili ambao wamepona walioletwa hapa *Mirembe Hospital* kutoka sehemu mbalimbali za nchi yetu. Fungu la kuwarudisha wagonjwa hawa baada kupona halitoshi hivyo wanabaki muda mrefu kabla ya kurudishwa makwao.

Mheshimiwa Spika, sekta hii ya afya imetendewa haki kabisa hospitali za kisasa zimejengwa na zinaendelea kujengwa karibu Wilaya zote na vifaa vya muhimu vipo; *Ct-Scan*, maabara ya kisasa, *theatre* na wodi za heshima za wajawazito na wagonjwa wengine. Vifaa tiba na dawa zinawafika wananchi.

Mheshimiwa Spika, wananchi wengi hasa wa vijijini bado wanateseka na maradhi kama haya kansa mbalimbali kama haya ya shingo ya kizazi na mengine. Pia watu wengi

hawapati fursa za kupata kuchunguzwa afya zao hivyo hubaki na maradhi kwa muda mrefu na hivyo kuathirika vibaya sana.

Mheshimiwa Spika, wananchi hawa wanashindwa kupata tiba mapema na pia kutomudu gharama. Nataka kushauri Serikali kupitia Wizara ya Afya walazimishe kuchunguza wanawake waliona umri hatarishi wa kupata kansa iwe ni lazima kuchunguzwa hivyo tutaweza kuokoa maisha ya wengi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze mchango wangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti hii mchango wangu utaanza kwa maswali kadhaa kama ifuatayovyo:-

Je, ni lini Serikali itaendelea au kusogeza huduma za kibingwa na kihadhi kimataifa/*accreditation* kwa hospitali kubwa na za kanda? Mfano wa Nyanda za Juu Kusini mojawapo ya hospitali inayosaidia karibu mikoa nane iliyopo ukanda huu ni Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya *(Mbeya Zonal Referral Hospital -MZRH)*.

Pili ni hospitali iliyo katika lango kubwa la nchi nyingi zilizo katika *SADC* kama lango kuu kwa upande wa Kusini; tatu, ipo katika mkoa ambao una barabara kuu ya kufikia nchi nyingine kupitia *border* za Tunduma na Kyela. Hivyo muingiliano wa wageni kutoka nchi jirani ni fursa kubwa ya kuzalisha utalii wa kimatibabu *(Medical Tourism)*.

Mheshimiwa Spika, ikiwa patahitajika hospitali kubwa ya kuanza nayo kihuduma kwa wageni wa nchi jirani basi itakuwa ni hii *MZRH*. Hivyo ni fahari mno ikiwa hospitali hii

itapewa kuwa kitovu cha utalii wa kimatibabu. Utalii wa kimatibabu utawezesha nchi za jirani au wageni kuja kupata huduma mbalimbali za kimatibabu na huduma bingwa kwa wepesi na ubora *(fast & quality services)*.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa utalii wa kimatibabu ni kuwezesha kukua kwa pato la ndani la Taifa kupitia fedha za kigeni ambazo zitaingia nchini kwa wageni wanaokuja kupata matibabu na hata kujifunza baadhi ya huduma za matibabu za kibingwa kutoka kwa wataalamu wageni.

Mheshimiwa Spika, utalii wa matibabu na kujifunza teknolojia za matibabu kupitia hospitali hii kutaleta fursa ya muunganiko wa kujifunza hata wengine nao wanafanyaje na hata kuvutia uanzishwaji wa makambi *(medical camps),* nchi nyingine kwa ajili ya kutanua wigo wa huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, ipo haja kubwa kwa Serikali na wadau kuweza kuhakikisha hospitali zilizo katika lango la nchi jirani kuongezewa uwezo wa kupewa hadhi za kutoa huduma tambuzi kimataifa *(international accredited)* katika kufanya kazi na mashirika makubwa na taasisi kubwa za kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kufanikiwa kwa hili kutasaidia sana kukuza hadhi za huduma, huduma za kibingwa kuvuka mipaka ya nchi na hata iwe zamu yetu sasa watu watoke nchi nyingine kuja kupata huduma kwetu kama ilivyo India ilivyojipa nafasi kimataifa kuwa na uwezo mkubwa wa kupokea wagonjwa na hata kutoa fursa za utalii matibabu.

Mheshimiwa Spika, kufanikiwa kwa *MZRH* kupata hadhi hii kutatanua wigo wa hospitali katika kuwa na uwezo mkubwa zaidi katika idara za maabara na ngazi zote za matibabu.

Mheshimiwa Spika, katika Nyanda za Juu Kusini basi mojawapo ya hospitali inayosaidia karibu mikoa nane iliyopo ukanda huu ni Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba kuwasilisha.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Wizara kwa hotuba ya Bajeti, lakini zaidi kwa ile programu ya *mentorship* ambapo tuliwaona madaktari ambao wataenda kila Wilaya kufanya mafunzo kwa mwezi mmoja.

Pili Mheshimiwa Waziri ameeleza kuhusu wahudumu wa ngazi ya jamii *(CHWs)*, hata hivyo naomba awaondoe shaka wahudumu waliopo, na hii ni kwa kuzingatia *message* hii ambayo nimetumiwa na mmoja wa *CHWs.*

"Habari za kazi! Naomba mnisaidie kwa Wizara ya Afya, Aaziri alitangaza kuwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii watatangaza kwa vijana waliofika kidato cha nne, na watawalipa. Sasa wahudumu waliojitolea tangu mwaka 1986 na wapo je, hawa Wizara inawafanyia nini inapowastaafisha, mimi mwenyewe nimefanya tangu 1992 kwa kujitolea, na Wilaya ya Mufindi wapo kila Kijiji."

Mheshimiwa Spika, nadhani ipo sababu ya kuwaondoa shaka hawa waliopo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Daktari Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini mimi na

Mheshimiwa Ummy Mwalimu kuiongoza Wizara ya Afya. Sisi tunachomhakikishia ni kwamba hatutamwangusha.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Makamu wa Rais na Waziri Mkuu kwa miongozo yao ya wakati wote ambayo imekuwa ikitusaidia mimi na Mheshimiwa Ummy Mwalimu katika kazi zetu.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru wewe kwa usimamizi mzuri na ushauri mzuri kwa wakati wote ambao tunafanya shughuli zetu za kibunge hapa. Wabunge wamesema hapa, wakaniona mimi ni sawa wamemwona Mheshimiwa Ummy Mwalimu, na wakimwona Mheshimiwa Ummy Mwalimu ni sawa wameniona mimi. Maana yake ni kwamba, niwaambie tu ukweli, sisi Wizara ya Afya tunajigamba sana, tunaye Waziri wetu, dada yetu, mshauri wetu, lakini ni mtu ambaye hata kabla wewe hujasema, tusitaje sana majina ya Mawaziri, yeye tayari alishaniambia hakuna sababu ya kulitajataja. Sisi tupige kazi, hudumia Wabunge, twendeni mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo niseme machache na mnisikilize kwa umakini nioneshe tuna Rais wa namna gani, na ni kwa namna gani kwa kipindi kifupi ameweza kufanya kazi kubwa ambapo kwa upande wangu mimi, matatizo yote ambayo mnayaona hapa, yeye Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametupandisha mlima, na sasa tunachokiona mbele yetu ni kichuguu, na kichuguu hatutakipanda, tutaenda kukivuruga.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye hospitali zetu za kanda, ukianza hospitali za kanda na za Taifa, kwa mwaka huu mmoja, zimepelekwa zaidi ya shilingi bilioni 51.4. Ukienda kwenye hospitali zetu za mikoa peke yake, ujenzi tu, zimeenda shilingi bilioni 54.2. Ukirudi kwenye hospitali zetu hizi za mikoa pamoja na za Taifa, fedha zilizokwenda kwa ajili ya vifaa tiba ni shilingi bilioni 290.9, ni fedha nyingi sana. Maana yake ni nini? Hizo fedha zimefanya mapinduzi makubwa sana

ambayo mmeyaona hapa. Waziri wetu ameonesha mtoto ambaye ametibiwa hapa na ni huduma ambayo tulikuwa tunaenda kuipata nje kwa zaidi ya shilingi milioni 250. Leo anatibiwa ndani ya Tanzania kwa shilingi milioni 30 na kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda kwetu pale Muhimbili, Hospitali ya MOI utakuta leo tulikuwa tunaenda kwa zaidi ya shilingi milioni 80, wenzetu wanapokuwa na vivimbe chini ya ubongo, tunawapeleka India kwa ajili ya kuwatibu hivyo vivimbe kwa zaidi ya shilingi milioni 80. Leo wanapona ndani ya Tanzania kwa shilingi milioni saba, bila kufungua kichwa, wanaingiza mashine kwenye pua na wanatoa vivimbe chini ya sakafu ya ubongo na mtu anarudi nyumbani kwake amepona.

Mheshimiwa Spika, maana yake nini? Hizo fedha zimeokolewa, ni fedha ambazo zilikuwa ziende nje, halafu sasa zimebaki ndani ya Tanzania zipo kwenye mzunguko wetu ndani ya Tanzania zinasaidia wananchi. Ndiyo maana umeona leo wamekuja Zambia, Rwanda na Malawi juzi mmeona watu wetu wamekwenda kule. Maana yake Rais wetu amepunguza rufaa kwenda nje kwa asilimia 97. Maana yake sisi na wenzetu waliokuwa wametuzunguka, tulikuwa tunaenda kupanga foleni India kwa pamoja. Rais wetu amefanya kazi kwa asilimia 97, leo tunabaki ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, na wenzetu tuliokuwa pamoja tunapanga foleni nje kule India, leo amewarudisha, wanatibiwa ndani ya Tanzania. Ni kazi kubwa sana imefanywa na Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana yake ni nini? Ndiyo maana nasema, nawaambia tusiwe na wasiwasi kwa sababu bado tuko na Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, tuko naye,

tutakuwa naye mpaka 2025 na tunakuwa naye mpaka 2030 na ataendelea kupiga kazi kubwa ya namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yamezungumziwa masuala ya upatikanaji wa dawa kwenye vituo vyetu na zahanati zetu. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge, hili suala la upatikanaji wa dawa lina sehemu nyingi. Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshafanya kazi yake, ametoa fedha kwa ajili ya dawa kusambazwa kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano wa Ngara. Mbunge wa Ngara hapa alikuja akamlalamikia Mheshimiwa Waziri wa Afya, akamwambia kwamba kuna shida ya wizi wa dawa kule. Mheshimiwa Waziri wa Afya akanituma na Mbunge wa Ngara akatoa *Press* kwenye wilaya yake akilalamika kwamba kuna wizi wa dawa. Mheshimiwa Waziri wa Afya akanituma niende Ngara, nilipofika Ngara, Mheshimiwa Mbunge wa Ngara akanionesha *summons* ya kutoka Mahakamani. Akaniambia; "amenishtaki *DMO,* amenishitaki Mfamasia, wananiambia nimewachafua kwamba wameiba dawa." akaniambia, "wamemwambia nikiongea na wewe usiwaguse, wana-*withdraw* hii *summons* ya shilingi milioni 600 wanayokudai." Nikamwambia, usiogope, sisi tutaenda mbele. Hata kitendo cha kutishia Bunge kwa kutumia mwanasheria, hicho kinatosha kuwaondoa hapa.

Mheshimiwa Spika, tulipoingia kwenye kikao, wataalamu wetu walifanya kazi, tukatoa mikoba kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama, na Ushahidi. Wote pamoja na Kamati ya Ulinzi na Usalama tukakubaliana kwamba *DMO* na Mfamasia watoke kwenye Wilaya ya Ngara. Wametoka, na leo ukimwuliza Mbunge wa Ngara, anakwambia dawa zipo kwenye wilaya yake.

Mheshimiwa Spika, ninachokisema hapa ni nini? Anakwambia dawa zipo kwenye wilaya yake. Ninachosema, suala ni kwamba mafisadi wana ushirikiano. Sisi watu wema

tunakosa kushirikiana. Ninawaomba Wabunge, suala la kupambana na wizi wa dawa tusaidieni. Amesema Waziri wa Afya, ameshatoa maelekezo kwamba kuanzia sasa tukienda kujenga uwezo wa timu zetu za mikoa na wilaya tutajenga uwezo pia wa timu za ulinzi na usalama za wilaya ili waweze kufanya. Hata hivyo, Waheshimiwa Wabunge, tushikane mkono, tushirikiane pamoja tutandike wezi. Wangapi wananikubalia hilo? Piga makofi. Tuko pamoja? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haiwezekani Wilaya ya Siha wezi waibe, haki ya Mungu siji kulalamika Bungeni, namalizana nao huko, kama ni Serikali itanikuta Siha nikishughulikia majambazi. Kwa hiyo, nawaomba leo Wabunge wote tukitoka hapa, sisi ni Madiwani tusikubali dawa yoyote ipotee. Tusingojee kuja kulalamika Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kuna eneo lingine linaloitwa Mshitiri. Hili eneo la Mshitiri ni kijiwe kingine cha kuiba. Nimewaambia Wabunge na kote ninakopita kwa ma-*DMO,* nawaambia mkiona Mshitiri analeta bei kubwa mwondoeni. Nimekwenda Nzega kwa Mheshimiwa Bashe, Mshitiri amehonga watu huko ndani, dawa ndani ya hospitali ni bei ghali kuliko nje kwenye duka la Mshitiri aliyechaguliwa. Tulichokisema, tukamnyoosha Mshitiri, sasa hivi kule kwa Mheshimiwa Bashe mambo yanaenda vizuri. Ninachowaomba Waheshimiwa Wabunge, twendeni tukashirikiane pamoja kwenye eneo hili la kushughulika na wezi.

Mheshimiwa Spika, Ndugu zangu niwaambie kitu kimoja. Wengine mmetaja masuala ya *ambulance* hapa, lakini amesema Waziri wetu, Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametoa fedha, zimenunuliwa *ambulance* 727. Wakati huo, Waziri wetu alipoona kulikuwa na taratibu za kimanunuzi zinazotuletea mambo ya ajabu, akakataa, akasema hatununui kwa kufuata hizi taratibu za kimanunuzi, twendeni tukatafute mtu wa kutuuzia moja kwa moja na matokeo yake

tukaongezewa kutokana na kuokoa zile fedha, zikaongezeka *ambulance 168. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana yake ni nini? Wote pamoja tukiungana kupambana na ufisadi kuanzia kwenye eneo la manunuzi na kuanzia tunapotoka majimboni haki ya mama hizi fedha mama yetu anayopeleka kule zitafanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naulizwa na mtu mmoja ananiambia kwanini fedha za afya zimepelekwa kwenye maji wakati ule wa *corona?* lakini nikamwambia Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan anajua hesabu. Alijua ukipeleka dola moja kwenye maji, unapunguza dola nne upande wa afya na ukipiga mahesabu ya teknolojia aliyoileta hapa Tanzania halafu ukapiga hela zilizotolewa dola zilizookelewa kwenda nje unajua huyu ni Rais anaejua nifanye nini? Niokoe dola, wakati wenzangu nje dola zimewaishia yeye ana dola ndani.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana wenye akili walikaa wakasema huyu astahili tena kuitwa Samia Suluhu Hassan aitwe Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa sababu amepiga mahesabu ikaonekana wenzetu sasa wanapita kwenye ugumu mkubwa sana wa kiuchum, lakini sisi tuna nafuu kwa sababu Rais wetu kila kitendo anachokifanya kinabakiza dola nyingi ndani ya nchi badala ya kutoa dola nyingi nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kimoja, Mheshimiwa pale Mbeya kwako tulikuwepo na Kamati ya Bunge, tukawa tunatembelea na wananchi walikuwepo, tukawa tunatembelea majengo ya hospitali ya mikoa zaidi ya bilioni saba. Tumekwenda lile jengo la mama na mtoto ambalo limegharimu zaidi bilioni 19 pamoja na vifaa kuna *MRI*, kuna *CT – Scan.*

Mheshimiwa Spika, wananchi wakaniambia kabla ya wewe kuwa Mbunge, walikuwa wanaota sugu kutoka huku kuja Muhimbili kutafuta huduma. Lakini baada ya wewe kuwa Mbunge leo wananchi wa Mbeya Mjini wanabaki wanapata huduma za kinamama za kibingwa bobezi ndani ya Mbeya wanapata *MRI* ndani ya Mbeya, wanapata *CT – Scan* ndani ya Mbeya na tunataka kuwataarifu watu wengine wananchi wa Mbeya Mjini hawataota tena sugu kutoka Mbeya kwenda Dar es salaam wanataka kutulia na Dr. Tulia wao, waanataka kutulia na Dr. Tulia wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie la mwisho kwamba leo ndani ya Tanzania Afrika kuna nchi nne tu, ambazo zina kiwanda cha kuzalisha mionzi dawa. Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan amejenga kiwanda *Ocean Road* na sasa tunaenda kuwa nchi ya tano Afrika kwa kuzalisha mionzi dawa na mionzi dawa hiyo kila mwaka ilikuwa inatusababisha tutoe bilioni tano nje ya nchi sasa zinabaki ndani ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Ahsante sana, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kabla sijamuita mtoa hoja, kuna wageni waliyopo Bungeni na hawa ni wanachama 150 wa Umoja wa Vijana wa CCM kutoka Jijini Dodoma, karibu sana, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite Mheshimiwa Waziri wa Afya. Mheshimiwa Ummy Mwalimu aje ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, …

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, samahani utatusaidia pia sijui kama ni upotoshaji ama watu wamenakili vibaya ile hoja ya

matibabu ya selimundu nadhani kuna bilioni 58 na kuna milioni 58 ili utusaidie kurebisha hiyo ikae vizuri. Ahsante sana.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha siku ya leo lakini kipekee nimshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuwekeza katika sekta ya afya. Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wote ni mashahidi Bajeti ya Wizara ya Afya mwaka jana Fungu 52 ilikuwa shilingi trilioni 1.1 mwaka huu tunaomba mtupitishie shilingi trilioni 1.2 kuna ongezeko la shilingi bilioni 100.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Sekta ya Afya, ukiangalia fedha zilizotengwa kwenye Wizara ya Afya na fedha za TAMISEMI, bajeti ya Sekta ya Afya imeongezeka kutoka shilingi trilioni 2.1 mwaka jana hadi shilingi trilioni 2.4. Hii inaonyesha dhamira ya dhati kabisa ya Rais Samia ya kuboresha huduma za afya nchini.

Mheshimiwa Spika, natambua kamati imezungumzia maazimio ya viongozi wakuu wa nchi waliyokutana Abuja ya kwamba nchi zinapaswa kutenga asilimia 15 ya fedha zao za bajeti kwa ajili ya afya. Lakini Wabunge naomba tushukuru angalau tunaona ongezeko la fedha za afya kila mwaka. Kwenye hili tutaendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia. Amezungumza Naibu Waziri wangu mafanikio ambayo tumeyapata, majengo yapo kila sehemu, zahanati, vituo vya afya, hospitali za halmashauri tunazungumzia vifaa tiba vya kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miaka miwili iliyopita tulikuwa na *CT–Scan* 13 tu. Leo tuna *CT–Scan* 45 ndani ya Rais Samia Suluhu Hassan. Ndugu zangu wa Kigoma leo wana huduma ya *CT-Scan*, Katavi wana huduma ya *CT–Scan*, Manyara, Simanjiro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwako Mbeya ninahaidi itakapofika tarehe 30, Juni tutakuwa tumekamilisha *MRI* na *CT–Scan* lakini kwenye suala la *MRI* hajapata tokea. Tulikuwa tuna *MRI* moja tu Hospitali ya Taifa Muhimbili leo chini ya Rais Dkt. Samia miaka miwili tumefunga *MRI* Chato, tumefunga *MRI* Mtwara na tutakamilisha ufungaji wa *MRI* Mbeya, huyu ndiyo Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, maneno machache vitendo vingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu hii miaka miwili iliyopita tukipata wagonjwa mahututi tutawalaza wagonjwa 258 tu. Leo watokee wagonjwa mahututi tuna uwezo wa kulaza wagonjwa 1000 kwa wakati mmoja, huyu ndiye Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumetambua huduma za magonjwa ya dharula *(Emergency Medical Department)*. Mwaka jana 2022 tulikuwa na majengo nane, miaka miwili ya Rais Samia Suluhu Hassan tuna majengo ya *EMD* 118, tena yameshuka mpaka katika ngazi za halmashauri. Zamani *EMD* unaiona Muhimbili, unaiona *KCMC* unaiona Bugando leo mpaka kijijini kule hospitali ya halmashauri unakuta huduma ya *EMD*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma za kina mama wajawazito tumeweza kuboresha huduma sasa hivi asilimia 98 ya kinamama wajawazito wana imani na huduma zinazotolewa na wanaudhuria kliniki. Hii imetuwezesha kupunguza vifo vya watoto wenye umri wa chini ya mwaka mmoja kutoka vifo 43 hadi vifo 33 katika kila vizazi hai 100. Lakini vifo vya watoto watano chini ya miaka mitano tumevipunguza kutoka vifo 67 hadi vifo 43. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali ya sekta ya afya duniani inapimwa kwa viashiria hivi. Ikiwemo vifo vya watoto lakini kubwa Tanzania na Dunia ya Kimataifa tulijiwekea malengo,

inapofika 2025 watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI wajue hali zao. Leo Tanzania tumefikia asilimia 94.4 kabla ya 2025.

Mheshimiwa Spika, tulipaswa kuweka asilimia 95 ya wenye UKIMWI wanaotumia dawa, wawe wapo kwenye dawa tumeishafika asilimia 95 kabla ya 2025. Lakini habari njema, wanaotumia dawa za kufubaza virusi za UKIMWI asilimia 96 maambukizi ya UKIMWI yamegandamizwa au virusi vya UKIMWI vimepunguzwa nguvu, haya ni mafanikio makubwa chini ya Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nikushukuru sana kwa jinsi unavyoongoza Bunge letu Tukufu pamoja na kusimamia mijadala ndani ya Bunge. Wewe ni *icon,* wewe ni *inspiration* kwa wasichana na vijana Tanzania kwamba tunaweza kuwa na wanawake wakafanya kazi kubwa na nzuri kama Dkt. Tulia Ackson hongera sana Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee niwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia hoja yetu pamoja na kamati. Kamati yetu madhubuti inayoongozwa na Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo Mbunge wa Maswa Mashariki ambaye imesomwa na Mheshimiwa Cecil Mwambe, tumepokea maoni na ushauri wa kamati. Tunawaponeza sana kamati kwa ushauri wenu mzuri lakini kipekee tunawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa maoni na ushauri kubwa. Kubwa, tutatekeleza maoni naushauri ambao mmetupatia kwa sababu una lengo la kuboresha huduma za afya kwa watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tumefarijika sana kupokea pongezi kutoka kwenu Waheshimiwa Wabunge, pongezi hizi tunazichukulia kama deni letu na watendaji wangu kwenu Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wa kufanya kazi

zaidi usiku na mchana ili tuweze kuimarisha na kuboresha huduma za afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge, napenda nitambue Waheshimiwa Wabunge waliyochangia hoja yangu. Wapo Wabunge 47 akiwemo na Naibu Waziri, Wabunge 44 wamechangia kwa kuongea na Wabunge watatu wamechangia kwa maandishi. Kwa sababu ya muda naomba nisiwataje.

Mheshimiwa Spika, hoja kubwa ambazo zimetolewa ziko kama hoja tisa nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kutoa ufafanuzi. Nitajikita katika hoja nane na kama muda utatosha nitazungumzia hoja ndogo ndogo, moja moja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge hoja kubwa ambayo wameileta pamoja na kamati ni Serikali kuwekeza nguvu zaidi katika huduma za kinga badala ya huduma za tiba. Waheshimiwa Wabunge hoja hii tumeipokea na ndiyo maana katika bajeti yangu kipaumbele cha kwanza maana ya huduma za kinga, huduma ya kwanza ya kinga ni chanjo za watoto zinazoweza kuzuia magonjwa. Tumetenga bilioni 114.3 kwa ajii ya kuhakikisha tunatoa chanjo zote za Watoto. Tutanunua pia ma–*fridge*, majokofu kama 1,600 na tutatumiwa magari ya chanjo 102 na kuyasambaza katika halmashauri zenu ili yaweze kuhudumia suala la chanjo.

Mheshimiwa Spika, chanjo ya pili ambayo tutaipa kipaumbele ni chanjo ya kuwakinga wasichana dhidi ya saratini ya mlango wa kizazi. Waheshimiwa Wabunge, naomba mkawe mabalozi, chanjo hii ni salama, chanjo hii haimzuii msichana kuja kupata mtoto, kuja kupata ujauzito sana sana inamzuia kutokuja kupata maambukizi ya ugonjwa wa saratani.

Mheshimiwa Spika, turuhusu tuje tufanye semina Bunge lako tuonyeshe aina za saratani zinazoongoza kwa watanzania ya kwanza ni sarati ya mlango wa kizazi. Kwa teknolojia hii haikubaliki kuendelea kuwa na kizazi cha wasichana wenye saratani ya mlango wa kikazi. Niwaombe sana wazazi na walezi wenzangu wenye watoto wa umri wa chini ya miaka 14 tuwapatie chanjo ya saratani ya mlango wa kikazi chanjo hii inatolewa bure bila malipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia eneo la pili la kinga ni suala la lishe, tutaendelea kuwasaidia wazalishaji wadogo wa chakula, tutawapatia vinu 300 vya kuongeza virutubisho na kutoa matone ya vitamini A kwa watoto wenye umri ya chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, tumeona pia kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi, viwanda vinavyozalisha unga wa ngano, viwanda vinavyozalisha unga wa mahindi, viwanda vinavyotengeneza mafuta ya kula wanapaswa kuongeza virutubisho katika *product* zao. Kwa hiyo, tutashirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kuhakikisha viwanda vyote Tanzania vinafanya *food fortifications* ili tuweze kuimarisha kiwango cha lishe kwa watanzania.

Mheshimiwa Spika, eneo jipya ambalo tunakuja nalo katika suala hili la kinga ni kuimarisha kada ya wahudumu wa afya ngazi ya jamii *(Community Healthy Workers)*. Wamekuwepo hawa watu, mradi wa UKIMWI ana–*train* wahudumu wa afya ngazi ya jamii siku mbili, watu wa malaria ana–*train* wahudumu wake wa afya siku tatu, mtu wa kifua kikuu kila mtu anawahudumu wa afya ngazi ya jamii.

Mheshimiwa Spika, tumeona ipo haja ya kuja na mfumo mmoja wa wahudumu wa afya ngazi ya jamii *integrated and coordinated community health workers program* hawa wahudumu wa afya ngazi ya jamii tutaanza nao elfu tano na Waheshimiwa Wabunge watachaguliwa katika vijiji vyenu na

mitaa yenu. Tutazielekeza Serikali za vijiji ndiyo wawachague, tutawapa mafunzo ya miezi sita na tumeamua tujikite katika maeneo makubwa sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ya kwanza ni afya ya uzazi mama na mtoto, eneo la pili litakuwa lishe, eneo la tatu afya na usafi wa mazingira, eneo la nne magonjwa ya kuambukiza hususani malaria, kifua kikuu na ukimwi na eneo la tano magonjwa yasiyo ya kuambukiza hususani ni kisukari, shinikizo la juu la damu na magonjwa ya moyo na eneo la sita ni magonjwa haya ya mlipuko kama *Ebola* na *Marburg*.

Mheshimiwa Spika, tunaamini kabisa ameongea Mheshimiwa Oliver pale, tulipata mlipuko wa Marburg kule Goziba kuna watumishi wa afya wawili tu. Ukiweka wahudumu wa afya kila kijiji wawili, watatu wale ndiyo watakuwa jeshi la kwanza la afya la kuwafikia wananchi kutoa huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, nimepokea *concern* kuna wahudumu wa afya ngazi ya jamii waliyopo, waliosoma siku mbili, wiki moja, wiki tatu hatutawaondoa tutawa–*phase out* kidogo kidogo. Kwa hiyo, hii niwatoe wasiwasi kwa hawa tuna–*train*, tutawalipia lakini hawa wataendelea lakini baada ya muda tutawaondoa kidogo kidogo.

Mheshimiwa Spika, eneo la nne kwa upande wa kinga ni suala ya afya mazingira. Tutaanzisha kampeni ya usafi wangu mita tano, mita tano usafi wangu lakini pia tunafikisha miaka 50 ya kampeni ya mtu ni afya iliyoanzishwa na Rais wetu Julius Kambarge Nyerere. Katika kufanikisha huduma za afya, mazingira tutawabana sana Serikali za mitaa watekeleze sheria ndogo zinazosimamia usafi na afya mazingira.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni ubora wa huduma, Wabunge wengi hapa wamesema mmejenga majengo, mmeleta vifaa tiba lakini huduma siyo nzuri. Tunakubaliana

na Waheshimiwa Wabunge, kwamba uwekezaji mkubwa uliyofanywa na Serikali katika eneo la miundombinu, vifaa vya uchunguzi na vifaa tiba pamoja na kuajiri watumishi lakini bado kuna baadhi ya hospitali zetu hazitoi huduma bora.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge tumebaini kuwa changamoto kubwa ni uongozi. Jana nilitoa mfano wa Hospitali ya Muhimbili chini ya Profesa Janabi, ni uongozi. Kwa hiyo tunakuja na programu ya mabadiliko ya kiutendaji kwa wasimamizi wa utoaji wa huduma za afya *(Leadership for Health Transaformation Program)* ili kuwaongezea uwajibikaji, ufanisi na tija katika utoaji wa huduma za afya. Lakini tutaimarisha utawala bora, uongozi na menejimenti za usimamizi za hospitali, kwa kushirikisha kamati za ulinzi na usalama za wilaya na mikoa. Lakini tutafanya kaguzi za mara kwa mara na za kushtukiza ili kuimarisha usimamizi shirikishi katika vituo vya kutoa huduma za afya. Vile vile tutaendelea kushirikiana na mabaraza ya kitaaluma kuhakikisha wanataaluma wao wanatoa huduma bora za afya.

Mheshimiwa Spika, tumeanzisha pia kwenye mitaala ya vyuo vya afya somo la *customer care*. Kwa hiyo shule na vyuo vyetu vya afya pia vitafundisha masuala ya *good customer care*, matumizi ya lugha ya staha na faraja kwa magonjwa, ili wanaomaliza pia wasiwe tu wanatibu lakini pia wafanye huduma kwa kutumia lugha nzuri.

Mheshimiwa Spika, suala la rasilimali watu katika sekta ya afya, uhaba wa watumishi limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge zaidi ya kumi. Sisi tumeendelea kuajiri watumishi takribani 100,000. Sekta ya afya inahitaji watumishi takribani 219,000 na waliopo ni kama 109,616. Sambamba na kuomba vibali utumishi sisi wenyewe kama sekta ya afya tumejiongeza kwa hospitali zetu kupitia mapato yao ya ndani kuajiri wataalamu wa afya takribani 4,189 ambao wameajiriwa kwa mikataba. Lakini pia kuanzia mwaka jana nimewataka wadau wote wa maendeleo wanaotekeleza miradi ya afya

nchini, kutumia angalau asilimia 10 ya fedha zao kuajiri watumishi wa afya. Badala ya mradi malaria sijui malaria kila baada ya dakika moja kwenye redio na *Tv,* tunakata asilimia 10 ya fedha za miradi zinakwenda kuajiri watumishi wa afya na tutawapeleka katika maeneo ambayo yana uhaba. Lakini pia tutatoa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ya wataalamu wa afya, hususani madaktari bingwa na bobezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumetangaza juzi ajira za madaktari bingwa 30. Mpaka tunafunga muda tumepokea maombi ya madaktari bingwa 12 tu. Kwa hiyo madaktari bingwa wengi wanapenda kufanya kazi katika sekta binafsi. Tulichokiona, sera inataka tusomeshe madaktari bingwa walioajiriwa na Serikali, inatutaka tusomeshe watumishi walioajiriwa na Serikali; lakini tumeangalia katika hospitali zetu kuna watumishi wanaojitolea zaidi ya miaka miwili hadi miaka mitatu. Kwa hiyo hao tutawapeleka kusomea udaktari bingwa na tutawapa mikataba ya kufanya kazi katika hospitali husika angalau kwa muda wa miaka minne ndipo wanaweza Kwenda kwenye hospitali binafsi. Suala hili pia nadhani uliligusia wakati wa maswali na majibu.

Mheshimiwa Spika, eneo jingine ni kuhusu magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Tutaendelea kutoa elimu kwa jamiii kuhusu magonjwa yasiyo ya kuambukiza, tutafanya utafiti. Mwaka huu tunafanya utafiti wa kitaifa; na kwa upande wa elimu ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge naomba niwahamasishe, mambo manne tu ukiyazingatia. Ya kwanza, mazoezi angalau zisipungue dakika 30 kwa siku, moyo uende mbio na utoke jasho. Pili, punguzeni matumizi ya chumvi kupita kiasi. Tatu, punguzeni matumizi ya sukari na unaweza kuishi bila kula sukari; kama ulikuwa unatumia vijiko vitatu tumia kijiko kimoja. Vilevile eneo la nne ni kupunguza mafuta na sisi Wizara ya afya tumepeleka maombi kwa Wizara ya fedha kuangalia jinsi gani wanaweza kuongeza ushuru kwenye bidhaa hizi ili tupunguze matumizi ya bidhaa

zinazosababisha magonjwa haya yasiyo ya kuambukiza. Tutajikita kwenye magonjwa matatu; kisukari, shinikizo la damu pamoja na magonjwa ya moyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa magonjwa yasiyo ya kuambukiza pia tumeshusha huduma hizi tumeanzisha kliniki katika ngazi za msingi, lakini pia tutaanzisha vituo 100 vya uchunguzi wa saratani katika ngazi ya msingi.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la huduma za utengamao *(rehabilitative services)*. Asubuhi hapa nimemtambulisha mwanangu Lukiza. Lukiza sijui kama unanisikia Lukiza. Nadhani mnamuona ndivyo yuko hivyo. Lukiza amezaliwa na tatizo la *autism*, usonji. Lukiza alikuwa hawezi kuvaa nguo, hawezi kula, hawezi kupiga mswaki, hawezi kufanya chochote. Mama yake Hilda amehangaika na mtoto. Lakini kwa sababau ya huduma za utengamao ikiwemo huduma za mazoezi tiba, huduma za kazi *(occupational therapy)*, huduma za *speech*, Lukiza anaweza kujivalisha nguo zake mwenyewe leo, Lukiza anaweza kula leo, Lukiza ametulia pale ameingia saa kumi, Lukiza hajafanya fujo yoyote kwa sababu amefundishwa jinsi ya kufanya utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala hili limenigusa kama mama. Ukienda kwenye vituo vya watoto wenye ulemavu asilimia 99.5 wanapelekwa na akina mama wenzangu. Sisi kama Serikali tumeamua kuimarisha huduma za utengamao kwa watoto lakini pia tunaboresha huduma hizi kwa sababu umri wa kuishi pia unaongezeka wazee nao wanakua. Lakini pia ajali zimeongezeka, Profesa Ndakidemi umesema hapa mtu amekatwa mguu, amekatwa mkono, huduma za utengamao ndio zinamsaidia mtu tuishi maisha bora *(quality life)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile pia tutaangalia watoto wenye *autism*, tutaangalia watoto wenye mtindio wa

ubongo, watoto wenye udumavu wa akili, watoto wenye *mongolia*, watoto wenye ukosefu wa utulivu. Waheshimiwa wabunge anaweza akazaliwa mtoto ana ukosefu wa utulivu akapewa masaa mawili atunge ushanga, miaka miwili mtoto yule anabadilika anakuwa na utulivu. Kwa hiyo eneo hili ni eneo ambalo tutalipa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, na kipekee nimpongeze sana Hilda Nkabe kama mama, akaanzisha taasisi ya Lukiza *Autism Foundation* ili kuongeza elimu na hamasa ya watoto wenye usonji. Lengo la Hilda ametaka wanawake wenzake wasiwafiche watoto wenye usonji na watoto wenye ulemavu. Ndiyo maana kila mwaka tunafanya mbio *(Run for Autism)* ili kuongeza hamasa kuwaonesha kwamba watoto hawa wanawezekana.

Mheshimiwa Spika, nipongeze wataalamu wetu. Tunaye *Doctor* ambaye amekuja hapa mtaalamu wa *Physiotherapy,* Godfrey Kibati, ambaye anafanya masuala la *Occupational Therapy.* Tutashirikiana naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona mpaka twende Muhimbili hawa madaktari wakasome miaka mitano hatutafika. Kwa hiyo tutaanzisha kozi za miezi sita mpaka tisa za muda mfupi. Tuchukue wauguzi labda wawili kutoka kila hospitali au kila halmashauri, madaktari wawili kutoka kila hospitali kila halmashauri tuwapeleke wasome angalau kozi hizi tatu za masuala la tiba utengamao.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumesema, kwamba lazima tufanye *assessment*. Tiba hizi za utengamao zinapatikana wapi? Kwa hiyo tutafanya *assessment* kujua vituo vyote ambavyo vinafanya huduma hii, ikiwemo kuimarisha huduma za matibabu. Lakini pia kuna suala la afya ya akili na namna ya kukabiliana nalo. Tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuona umuhimu wa Serikali kuwekeza kwa kuibeba ajenda hii ya afya ya akili. Afya ya akili ndio msingi

wa afya ya binadamu. Hakuna afya bila afya ya akili, na ndio uchumi wa mtu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwenye hili, kama ilivyo kwenye huduma za utengamao, hatuna wataalamu wa kutosha. Tunafurahi wenzetu wa Chuo Kikuu cha Muhimbili *(MUHAS)* mwaka huu wataanzisha kozi ya *Clinical Psychology,* angalau, na mimi nimewaambia, sisi Serikali tuko tayari kugharamia wanafunzi 10 watakaofanya *degree* ya kwanza ya *Clinical Psychology* ili tuweze kuwapata na kuwasajili katika maeneo mbalimbali. Lakini tunatoa elimu kwa umma kuhusu vihatarishi vya afya ya akili na namna ya kukabiliana nayo. Tutahakikisha pia kwamba tunakuwa na wataalamu wa muda mfupi, maana tukisubiri wamalize miaka mitano tutakuwa tumechelewa sana. Kwa hiyo hii pia tutaifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini tumeamua kuipandisha hadhi Hospitali ya Taifa ya Akili Mirembe, itakuwa ni Taasisi ya Taifa ya Afya ya Akili. Tunawataka Mirembe wafanye *promotional activities*, wafanye tiba, wafanye mafunzo na wafanye tafiti. Kwa hiyo tutawapa maeneo makuu manne. Vilevile pia tumesema tutaanza na huduma za afya ya akili katika hospitali kumi za rufaa za mikoa na hospitali za halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umuhimu wa kuanzisha huduma ya kisaikolojia Balozi dada yangu Jesca Msambatavangu ameiongea vizuri. Tunawaaalika sekta binafsi; Ulaya, Marekani, India hii ni biashara kubwa. *Yoga* masuala ya *rehabilitation*, masuala ya *breathing technique*, kama kuna mtu kuna msitu mzuri akaanzishe watu waende siku mbili wakaondoe ma-*stress* ya Bungeni, muondoe ma-stress ya familia nyumbani, baba amekuchukiza, jamani Watanzania tengeni muda wa ku-*refresh*, *otherwise* mtapata changamoto nyingi. Kwa hiyo suala hili tutaendelea kuliboresha.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto, kwa kweli tunakwenda vizuri. Lakini jambo moja ambalo limezungumzwa na Wabunge wenzangu wananwake, wameniuliza, Mheshimiwa Waziri, hebu tuambieni sasa sera ya huduma hizi ni bure au siyo bure? Nimefanya uchambuzi na timu yangu, tukaangalia, Mheshimiwa Waziri wa fedha yupo. Tukaangalia mama anatakiwa kwenda kliniki angalau mara tano wakati wa ujauzito. Hudhurio la kwanza ni shilingi 2,397. Hudhurio la pili shilingi 15,187. Hudhurio la tatu 2,397. Hudhurio la nne 1,727. Hudhurio la tano ni 2,397. Kwa hiyo kwa mahudhurio matano mwanamke mjamzito gharama ni shilingi 24,103. Tumeondoa umeme, tumeondoa mzani, tumeondoa dawa ambazo zinanuliwa na Serikali, hizi ni zile *re-agent* kufanya nini kwa mfano, *Hb*, kupima wingi wa damu, protini, kupima mkojo pamoja na kupima *blood glucose*. Tuna wanawake takribani milioni mbili kila mwaka, kwa hiyo ni 48,000,000,000.

Mheshimiwa Spika, tukienda kwenye huduma za kujifungua kawaida, tumefuta vitu vidogo vidogo vingine vyote, tumepata ni 32,952. Wanawake 1,600,000 ndio wanajifungua kawaida, kwa hiyo inakuwa kama 52,000,000. Wanaojifungua kwa upasuaji gharama ni 63,000; kwa hiyo hapa inakuja bilioni 119. Hivyo, kama tunataka kutoa huduma bora kwa wanawake wajawazito Waheshimiwa Wabunge ni bilioni 119, hatujaweka umeme, hatujaweka maji, hatujaweka vifaa, hatujaweka *CT-scan*, hatujaweka *X-Ray* mashine, hatujaweka *ultrasound*. Kwa hiyo tunaongea na wenzetu wa Wizara ya fedha, kwamba hebu watuangalie huko mbeleni kama kuna elimu bure basi na hili sasa liende badala likabaki kwenye makaratasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hiyo ndiyo gharama ambayo tumeipata. Lakini niendelee kusisitiza kwa watoa huduma za afya. Kuna dawa tunazinunua bure, nataka wajawazito wapewe bure. Kuna vitu tunavinunulia bure, tunataka wajawazito wapewe bure.

Mheshimiwa Spika kuna suala la Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Kabla sijazungumza hili niende kwenye kuimarisha huduma za ubingwa bobezi. Kwenye hili kwa kweli tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kutambua mchango wa wataalamu wetu. Lakini kipekee tunamshukuru Rais Samia, tumetenga safari hii bilioni 23, amesema Naibu Waziri. Kupeleka mgonjwa wa figo nje ya nchi ilikuwa milioni 120 lakini ndani ya nchi milioni 30. Uroto nje ya nchi milioni 250 na ndani ya nchi ni milioni 58 mpaka 70. Kwa hio ilikuwa ni kukosea niliposema bilioni kwa hiyo ni milioni 58.

Mheshimiwa Spika, tulikaa na wenzetu wa Wizara ya Fedha, tukampelea Mheshimiwa Rais maombi yetu. Kama mgonjwa huyu mtoto wa *sickle cell* anaweza kupona kwa milioni 58 kama tulikuwa tunapeleka wagonjwa hawa nje ya nchi kwa nini tiusitenge fedha ya ndani ya kuwasaidia wasio na uwezo kupata huduma hizo. Tunamshukuru Rais Samia, na ndiyo maana bajeti yetu ina *addendum*. Tumepata bilioni tano za kugharamia kupandikiza uroto kwa watoto wenye *sickle cell,* lakini pia tutapandikiza figo kwa watu wenye matatizo ya figo, na eneo la tatu tutapandikiza watoto vifaa vya kusaidia kusikia *cochlear implants*. Tutaweka vigezo, tangu jana tulivyosema nimepata maombi mengi, kwa hiyo tutaweka vigezo yupi atastahili, yupi hatastahili. Lakini kubwa Waheshimiwa Wabunge wataalamu wetu wanafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa tiba utalii, hapa ninaposema wataalamu wetu saba wameitwa Malawi ili kutoa huduma za uchunguzi wa moyo kutoka Jakaya Kikwete na wameshawachunguza wagonjwa 720, na kati yao 537 wamegundulika kuwa na matatizo ya moyo, wanakuja Tanzania kupata huduma hii. Kwa hiyo tiba utalii itakuwa inawezekana chini ya Rais Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalize hili la bima ya afya. Bima ya afya ndiyo roho ya huduma za afya nchini. Asilimia 70 ya fedha za hospitali zetu za umma na binafsi zinategemea bima ya afya. Tumefanya *actuarial studies* na kuona kwamba baadhi ya vifurushi vinahatarisha uhai na uendelevu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Ndugu yangu Hawa ameliongea. Hawa *Toto Afya Card* anachangia 50,400. Katika kila shilingi 100 wanatumia shilingi 667. Lakini la pili tumefanya uchambuzi zaidi, katika mwaka 2021 watoto waliosajiliwa *Toto Afya Card* walikuwa 157,920 wakachangia bilioni 5.9 wakatumia bilioni 40.5; jamani kuna bima ya afya hapo? Unachangia bilioni tano unatumia bilioni 40.

Mheshimiwa Spika, fedha zinaenda wapi? Asilimia 53 kumuona daktari. Watanzania tuna utamaduni fulani hivi. Nikishakuwa na bima ya afya kitu cha kwanza naenda kwenye *polyclinic* ya kumuona *specialist*; tukaangalia magonjwa gani haya. Ugonjwa wa kwanza ni malaria, malaria unatibiwa katika zahanati. Ugonjwa wa pili mfumo wa hewa, unatibiwa katika ngazi ya zahanati, ugonjwa wa tatu *UTI*. *UTI* inatibiwa katika ngazi ya chini. Kwa hiyo tumeangalia hela asilimia 58 za hela ya *Toto Afya Card* zimeenda kwenye vituo binafsi vya kutoa huduma za afya, asilimia 20 imekwenda hospitali za Serikali, asilimia 22 imekwenda katika vituo vya taasisi za dini. Kwa hiyo mtaona wenyewe hakuna uendelevu wa bima ya afya ya *Toto Afya Card*.

Mhesimiwa Spika, sasa, *the way forward* mtu-*challenge, the way forward,* ndiyo maana tunasema kuna vifurushi, kwamba watoto wasajiliwe Pamoja na wazazi wao. Lakini la pili watoto wasajiliwe wakiwa shuleni. Kama kuna watoto 100, kwa sababu kama shule ina watoto 100 watakaoumwa watakuwa labda 10 watasaidia 90 watalipia wenzao 10 watakaoumwa, lakini hili suala *the way forward* yake ni bima ya afya kwa wote. Bima ya afya ndiyo itakayotutoa.

Mheshimiwa Spika, tumefanya uwekezaji mkubwa katika huduma za afya, tumejenga ili wananchi wapate huduma bora za afya, inabidi waweze kulipia kabla ya kugua. Suala hili tunaendelea na majadiliano ndani ya Kamati, tunaamini tutaweza kufikia muafaka.

Mheshimiwa Spika, maswali mengine mojamoja ambayo ni suala la dada yangu Mheshimiwa Fatma Toufiq kuhusu *Health Basket Fund* ipelekwe kwenye dawa. Asilimia 33 ya hela ya *Health Basket Fund* inapaswa kutumika kwa ajili ya dawa, lakini tunazungumza kuijengea mtaji *MSD*. Hapa tunalalamika *MSD* haipeleki dawa, tutabadilisha watu kama hatutaipa mtaji *MSD* ikawa ni duka, ukishakuwa na vifaa vyako una-*order* unapewa. *MSD* sasa hivi anasubiri hela za vituo zije ndio akanunue dawa.

Mheshimiwa Spika, la pili, suala la dada yangu Mheshimiwa Munde, tumewanyang'a, kwa nini Hospitali ya Kanda imetoka Tabora imepelekwa kwingine. Hatujawanyang'anya tuliangalia vipaumbele. Tuliona Kigoma tutavutia DRC, wagonjwa wa Burundi na wagonjwa wa Rwanda, ndio maana tukaenda Kigoma, lakini nataka kuwapoza, tutajenga Hospitali ya Taifa ya Huduma za Watu Wenye Ulemavu Tabora kwa sababu, walishatenga eneo. Hilo jambo tunataka kuwaahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalize kuhusu majengo yote ambayo hayajakamilika. Tumetenga fedha na tumekubaliana ndani ya Wizara, badala ya kuanza ujenzi mpya ni vizuri tukakamilisha ujenzi wa majengo ambayo tumeyaanza.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni huduma kwa wazee. Huduma kwa wazee tumelipokea na tumeanza. Dawa za kisukari aina mbili za wazee sasahivi zitapatikana katika ngazi ya zahanati. Dawa aina tano za kisukari kwa ajili ya wazee na magonjwa yasiyo ya kuambukiza, tumezishusha kutoka

Hospitali ya Wilaya, sasa zitapatikana katika kituo cha afya, lakini pia tutaendelea kuimarisha.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, tumepokea hoja za Wabunge zote na nyingine tutazijibu kwa maandishi ikiwemo upatikanaji wa *ambulance,* amesema vizuri Naibu Waziri wangu. Tulipokwenda Toyota *basic ambulance* walitupa bei ya milioni 144, tukaenda *UNICEF* tukapata kwa milioni 83.9, *advanced ambulance,* Toyota, sijui kama naharibu biashara ya mtu sijui lakini, tukapewa bei ya shilingi milioni 162, tukatumia *UNICEF* tumepata kwa shilingi milioni 93. Kwa hiyo, tume-*save* bilioni 17.8, amesema hapa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kila halmashari itapata *ambulance* mbili na sisi Wizara ya Afya tutaongeza *ambulance* moja kwa baadhi ya majimbo ambayo yana idadi kubwa ya vifo vya akinamama wajawazito na watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalize tu kwa kusema, hospitali zetu hizi…

**SPIKA:** Dakika moja, malizia Mheshimiwa.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kusema, niwaombe sana tuilinde *NHIF*. Muhimbili *JKCI* ya Jakaya Kikwete, hela anazokusanya *cash* ni bilioni 5.0, *NHIF* analipa bilioni 22 kwa mwaka. Muhimbili, hela anayokusanya *cash* bilioni 12, *NHIF* bilioni 50; hela hizi ndivyo wanavyotupa maombi, nina mgonjwa amekwama Muhimbili, nina mgonjwa amekwama *JKCI,* nadaiwa maiti, ndio zinatumika kulipia wagonjwa wetu.

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kukushukuru wewe, lakini pia kwa kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ushirikiano mkubwa anaonipatia. Katibu Mkuu Dkt. Seif Shekalaghe, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Grace Magembe, Wakurugenzi wote wa hospitali, lakini kipekee nimshukuru

Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini kuwa Waziri wa Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge, hii ni bajeti yangu ya saba kusoma kama Waziri wa Afya. Mwaka huu tutaleta mabadiliko makubwa zaidi ili tuweze kuboresha huduma za afya. Sio kwamba, najua sana au nina akili sana, lakini naamini ni kwa sababu ya kudura na kadari za Mwenyezi Mungu. Ndio maana nasimama hapa kwa mara ya saba kusoma bajeti ya Wizara ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishukuru familia yangu, ndugu zangu na watu wangu wa Tanga Mjini, nawapenda sana. Watu wa Tanga waangalie kazi zangu za Tanga Mjini, tumejenga barabara, tumejenga shule, tumeboresha Bandari ya Tanga, tumefanya mikopo. Naamini 2025 Tanga Mjini wanarudi na Odo Ummy Mwalimu na sio mtu mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamulie)*

**WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Matumizi.

**SPIKA:** Kamati ya Matumizi.

## KAMATI YA MATUMIZI

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi. Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza na Kitabu cha Pili. Fungu 42 – Wizara ya Afya, Ukurasa wa 468, katika kishkwambi ni Ukurasa 468.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya wameleta *Addendum*. Fungu 52 – Wizara ya Afya, Ukurasa wa 468.

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 52 – Wizara ya Afya

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…........................…Sh. 7,602,257,864

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mambo mawili; kwanza tumeletewa hapa marekebisho ya fedha ambazo zimeongezeka na Kamati yetu ilipata nafasi ya kuzipitia hizi fedha zilizoongezeka kwenye Fungu hili na kwenye Taarifa ya Kamati inaonesha hizi pesa wao wamezikubali kwa maana ya kwamba, wameafikiana na hayo mabadiliko ambayo Serikali imeyaleta.

Sasa kabla ya kuwahoji kuhusu kifungu hiki chenye mshahara wa Mheshimiwa Waziri, wako Wabunge ambao wanataka ufafanuzi kutoka hapa kwenye kifungu hiki. Kila Mbunge ana jambo lake mahususi la kisera analotaka Mheshimiwa Waziri afafanue.

Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa. Siku ya Ijumaa nilipochangia niliomba ufafanuzi wa Wizara ya Afya kuhusiana na lengo la

Serikali kuhamisha masuala ya usalama wa chakula kwa maana ya *food safety* kutoka *TBS* kwa maana ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara na kurudisha Wizara ya Afya. Kwa bahati mbaya wakati anahitimisha Mheshimiwa Waziri hajagusia suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kusema kwamba, natambua wakati Serikali inafanya uamuzi huo ilikuwa ni katika kuangalia namna ya kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya biashara, kulingana na *blue print,* lakini kiuhalisia yako mambo ambayo huwezi ukayafanyia, yaani ni *no go zone area* kwa sababu, suala hili la usalama wa chakula linahusu afya za Watanzania. Kuendelea kwa afya za Watanzania katika *food safety* kuangaliwa na Wizara ya Viwanda na Biashara ni *conflict of interest.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kupata kauli ya Serikali kutoka kwa dada yangu Mheshimiwa Waziri Ummy Mwalimu, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha suala la usalama wa chakula kwa maana ya *food safety* linarudi kwenye Wizara ya Afya kama ilivyokuwa hapo awali na sio kuipeleka hapa ilipo kwa sababu, kumekuwa na matukio mengi ya vyakula kuingia nchini ambavyo haviko sawa, lakini pia kumekuwa na changamoto kubwa sana siku hizi ya usugu wa dawa, kwa maana ya *antibiotics* ambazo zinatumika kwenye mifugo. Kwa hiyo, nadhani Serikali ilichukue suala hili kwa uzito, hivyo, ningependa tu kupata ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri kuhusiana na suala hili. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Neema Lugangira kwa sababu kwa mujibu wa hitaji la Shirika la Afya Duniani, masuala ya dawa, vipodozi na chakula yanaendana pamoja, lakini Serikali katika kuweka mazingira wezeshi ya biashara, hoja ilikuwa kwamba, *TBS* ana-*charge, TFDA* ana-*charge*. Kwa hiyo,

ilienda kwa mlengo huo ili tupunguze ule mlolongo wa kuwa-*charge* wawekezaji na wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeliona tayari jambo hili ndani ya Serikali, tumeliongea katika ngazi ya wataalam, tukaliongea katika ngazi ya Makatibu Wakuu, ngazi ya Waziri Mheshimiwa Jenista alituongoza. Kwa hiyo, tuko katika hatua ya mwisho ili kuweza kupata *position* ya mwisho ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana naye pia. Kwa mfano sasa hivi, Wabunge wengi mnatumia *vitamin supplements,* sasa *supplement* hatu-*regulate* sisi kwa sababu sio dawa, ni chakula, lakini pia kuna usugu wa dawa. Kwa hiyo, jambo hili naomba tu Mheshimiwa Neema atupe nafasi tuendelee kulijadili na kulikamilisha ndani ya Serikali, halafu tutakuwa tumelipatia majibu. Nakubaliana naye pia, hata unapokwenda duka la dawa, liko duka la dawa na vipodozi kwa hiyo, ni vitu vinavyoendana na ndio *WHO practice* kwa hiyo, tumelipokea.

**MWENYEKITI:** Naona Mheshimiwa Neema bado umesimama.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Hapana. Nataka tu kusema naridhika na majibu ya Serikali na naamini mchakato huo hautachukua muda mrefu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Festo Richard Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. suala langu lilikuwa ni kufahamu msimamo wa Mheshimiwa Waziri kutokana na lile nililokuwa nimechangia kuhusu wanafunzi ambao wanakwama kwenye *Post Internship Exam* kwa sababu, utaratibu wa rufaa umekuwa uko gizani sana. Vijana wengi wa Kitanzania Madaktari wamekuwa

wakikwambia hapo na uhitaji wa Madaktari nchini ni mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni ipi kauli ya Serikali; najua kabisa suala la afya halina mzaha na hatuwezi kupeleka watu ambao ni *unqualified,* lakini nataka kufahamu mtu amesoma miaka mitano, anakwama kwenye mtihani wa mwisho ambao unafanywa na Baraza la Madaktari. Ipi ni kauli ya Serikali Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Hebu ngoja nielewe vizuri, anakwama kufanyaje? Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *registration* kwa sababu, ule mtihani akishaufanya anakuwa *registered,* lakini…

**MWENYEKITI:** Ana nafasi ya kufanya tena au hana? Ndio anakuwa amefutwa?

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa changamoto inapokuja ni kwenye ku-*reseat* mtihani na kukata rufaa, mchakato umekuwa uko gizani sana kiasi kwamba, wanafunzi wengi wanakwama kwa muda mrefu, hakuna utaratibu rasmi ambao unawekwa.

**MWENYEKITI:** Hakuna utaratibu rasmi? Nataka nielewe hoja yako ili iwe rahisi na mimi nikisikia ufafanuzi.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni hii, wanafunzi hawa wamesoma kwa muda wa miaka mitano na wameenda kwenye *field,* baadaye wanafanya mtihani unaitwa *Post Internship Exam*. Wakishafanya kuna wale ambao wanakwama kama ambavyo iko kwenye …

**MWENYEKITI:** Sawa, hapo nimeshakuelewa. Nataka kujua akishakwama pale, enhee?

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaokata rufaa, kwa mfano saa hizi tuna matabibu 200 walikata rufaa hadi saa hizi rufaa zao hazijajibiwa ni takribani karibu miezi sita imeshapita. Kwa hiyo, …

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, hawapewi nafasi ya kurudia mtihani?

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapewa nafasi, lakini, *I mean* rufaa ndio inayoleta shida.

**MWENYEKITI:** Rufaa kuhusu nini?

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mitihani ambayo wameifanya.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, yaani mitihani imesahihishwa, hakubaliani na yale matokeo?

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio, anakata rufaa sasa.

**MWENYEKITI:** Ila nafasi ya kurudia mtihani ipo?

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anaipata. Ndio, ipo Mheshimiwa.

**MWENYEKITI:** Haya. Rufaa?

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme Bunge hili hili tulipitisha Sheria ya Madaktari na Wataalam wa Afya Shirikishi, 2017. Moja ya jambo ambalo tulilisema ni kwa ajili ya kuhakikisha tunalinda weledi, *competence* ya watoa huduma za afya. Kwa hiyo, moja ya

sharti, umemaliza miaka yako mitano *University of Dar-es-Salaam, MUHAS, KCMC,* Bugando, popote, tukaona ili tuwe na *uniformity* kuwe na mtihani kabla ya kufanya *internship*. Kwa hiyo, kukawa na *pre-entry examination,* umemaliza miaka yako mitano ya Udaktari unafanya *pre-entry*. Niliporudi Wizarani 2022 wakalalamika, mbona mnaanza kutu-*judge* mapema?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi tukasema ile *pre-entry examination* atafanya, lakini *marks* zake tutazihesabu. Akimaliza *internship* atafanya *post internship examination*. Tutajumlisha *marks* zake, akifaulu atasajiliwa na Baraza la Madaktari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni Mwalimu, kwa kweli kuna watoto wetu wanasoma miaka mitano, lakini hamna kitu, tusidanganyane. Kwa hiyo, kama hatutakuwa wakali taaluma ya udaktari unategemea ni maisha ya watu, tusipokuwa makini kubanana, tunaweza tukawa na Madaktari jina. Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla juzi pia alinisaidia kulisema vizuri sana, lakini muhimu tunawapa fursa ya kurudia mitihani. Mpaka utakapofanya, ukifaulu utasajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la rufaa nalichukua, kwamba, yule mimi nadhani mtihani wangu haujasahihishwa vizuri, hilo tunalichukua, tutaenda kuliboresha. Naomba tumefanya *favor* kubwa sana, hatuwahukumu kwenye *pre-entry,* tunachukua matokeo ya *pre-entry* na matokeo ya *final internship and then* anasajiliwa na Baraza la Madaktari.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Sanga, naona umesimama.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru tu kwamba, nakubali na nimemwelewa

Mheshimiwa Waziri na naridhia alichokisema. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, ukisharidhika unakaa, ukisimama maana yake unataka tena maelezo ya ziada. Ukikaa tu mimi naelewa.

Mheshimiwa Eric James Shigongo.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshtushwa kidogo na takwimu ya homa ya ini kwamba, sasa hivi ni asilimia 4.1. Hiyo bado iko juu sana na ugonjwa huu upo na unaendelea kuenea kwa kasi.

**MWENYEKITI:** Asilimia ya nini? Samahani.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 4.1.

**MWENYEKITI:** Ya?

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, homa ya ini, *Hepatitis Tanzania.*

**MWENYEKITI:** Homa ya ini.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *yes.* Sasa hii bado iko juu sana. Watu wengi wanaambukizwa na ugonjwa huu upo na watu wengi wanakufa kwa ugonjwa huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo chanjo, chanjo ya homa ya ini ambayo mwaka 2000 nchi yangu iliamua kuwachanja watoto wote. Tafsiri yake ni kwamba, mpaka leo 2023 watoto wote wenye miaka 23, vijana wote, wamechanjwa. Hiyo ina maana kwamba, sensa ya mwaka 22 imeonesha kwamba, vijana wenye umri wa miaka 18 ni

asilimia 50 ya Watanzania wote. Kwa hiyo, inaonesha kwamba, nusu ya Watanzania wamechanjwa tayari kwa hiyo, asilimia iliyobaki ambao hatujachanjwa ni wale ambao ni mwaka 2000 kurudi nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachokiona, ile asilimia 4.1 inatoka kwetu sisi tuliozaliwa kabla ya mwaka 2000. Sijamsikia Mheshimiwa Waziri akizungumzia chanjo hii na kama tatizo ni *issue* ya fedha za kuwachanja Watanzania wote bure, Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba, iko *Global Alliance for Vaccination Initiative* na bado ipo *Centre for Disease Analysis Foundation* ambao wanatoa fedha kwa ajili ya nchi maskini kuchanja watu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nahitaji *commitment* ya Serikali. Serikali iko tayari kuwachanja Watanzania hawa waliobaki, milioni 26 tu, ili tuweze kuwa na *heavy immunity* katika nchi yetu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Erick Shigongo, mwaka jana alipoongea tulifanya maamuzi. Tumeunganisha au tumeuongezea majukumu mpango wa Taifa wa kudhibiti UKIMWI sasa ni Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI, Homa ya Ini na Magonjwa ya Ngono, la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, hawa wadau wetu hawagharamii chanjo ya homa ya ini kwa watu wazima. Inatolewa kwa watoto ambayo ipo ndani ya chanjo ya *Penta.* Kwa hiyo tutakachofanya na nimeelekeza kwenye hotuba yangu, ni kuhakikisha watu wanaoweza wajigharamie wenyewe kununua chanjo hizi. Tutatafuta kwa bei rahisi, zipatikane kwenye hospitali za wilaya, hospitali za mikoa na vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Shigongo, kwa hiyo tutakachofanya na nimeelekeza kwenye hotuba yangu ni kuhakikisha watu wanaoweza wajigharamie wenyewe kununua chanjo hizi, tutatafuta kwa bei rahisi zipatikane kwenye hospitali za Wilaya, hospitali za Mikoa na Vituo vya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni kwa nini nimetumia ujanja wa kutumia kwenye UKIMWI? Humo kwenye wadau wa UKIMWI tutawabana kwa sababu kwenye *general population* maambukizi ya homa ya Ini, kama alivyosema Mheshimiwa Shigongo ni asilimia nne, kwa wanaojidunga sindano, wanaotumia dawa za kulevya kwa kujidunga sindano, yako asilimia mpaka ishirini na kitu. Maambukizi ya homa ya Ini hata tukipeana mkono jasho tu nakupa maambukizi ya homa ya Ini. Kwa hiyo, nasi tumeanza kwanza kuingiza kwenye mpango wa UKIMWI halafu tutawaambia wadau wetu kidogokidogo kwamba tununue dozi fulani kwa ajili ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tutaangalia kwenye bajeti ya ndani ya Serikali. Kwa kweli anachoongea Mheshimiwa Shigongo, kinga ni bora kuliko tiba. Kutibu mgonjwa mwenye magonjwa ya Ini ni hela nyingi sana kuliko chanjo, na ninadhani haifiki hata shilingi 30,000 kwa dozi moja, kwa hiyo dozi tatu itakuwa ni 90,000. Mimi naamini wako Watanzania wanaweza waka-*afford* kuchanja chanjo hii kama tutawaelimisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shigongo, naona umesimama.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama. Bei ya chanjo ya homa ya Ini leo…

**MWENYEKITI:** Ukisimama kwenye ngazi hii unasema tu hujaridhika na majibu unataka watu wakuunge mkono. Ukishasema yale ya kwanza akitoa ufafanuzi na hujaridhika

na ule ufafanuzi, kwa sababu yeye sitampa tena nafasi, wewe ukishasimama hapo maana yake hujaridhika, kwa hivyo unatoa hoja ili Wabunge wakuunge mkono.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijafikia hatua hiyo, kama hivyo ndivyo…

**MWENYEKITI:** Huwezi kutoa maelezo mara mbili, ndiyo Kanuni zetu zinavyosema. Ama umeridhika au kama hukuridhika.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi nimeridhika.

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante sana.

Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kushauri, kwa kuwa lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba wananchi wa Tanzania wanapata huduma zinazopelekea kuongeza uhai wao. Hakuna jambo linaloumiza kama mgonjwa mwenyewe kuona kwamba anashuhudia kifo chake kwa sababu hana uwezo, au ndugu yake anashuhudia kifo au Daktari anayetibu anashuhudia kwamba anashindwa kumtibu mgonjwa kwa sababu hajaweza kutimiza masharti ya malipo yanayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu au wazo langu kwa Mheshimiwa Waziri. Kwa nini kama nchi hii tumeweza kuthubutu mambo makubwa, pamoja na shukrani nyingi ambazo Mheshimiwa Rais amethubutu katika kuisaidia afya ya mwananchi wake. Kwa nini sasa tusichukue mfano mzuri tulioufanya katika maeneo mengine kama barabara na sehemu nyingine kwa ajili ya kuhakikisha kwamba sisi wenyewe wananchi tuchangie japo kidogo tena, hata kama

ni shilingi 100 ili kuhakikisha kwamba mwananchi yeyote, hata yule maskini, awe mzee, angalau anaweza kupata huduma zile ambazo zinamhitaji kulipia wakati hana uwezo, kwa kutoa japo shilingi 100, kwa nini Wizara isifikirie kuja na mpango kama huo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Eng.* Manyanya, umesema unatoa ushauri, lakini niwe wazi, sijauelewa huo ushauri wako. Tuchange yaani kama humu Bungeni hiyo 100 ama? Sijaielewa hoja yako.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Maana yangu ni hii, kwa mfano *TARURA* - barabara vijijini, tuliamua kuweka tozo kwenye mafuta angalau ya shilingi 100 na mambo ya aina hiyo kwa kutumia tozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kwa mfano juzi tumeshuhudia kwamba minara ya mawasiliano 754 inakwenda kujengwa ambayo itaongeza wadau wengi katika matumizi ya mawasiliano. Kwa hiyo, kupitia hivi vyanzo vyetu tunaweza tukatoza senti kidogokidogo, nimechukulia mfano shilingi 100 ili kutunisha Mfuko wa Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo siizungumzii Bima ya Afya kwa sababu Bima ya Afya inayo masharti pia ya kila mtu kuchangia, *let's say* kima cha chini kama itakuwa shilingi 100,000 au 300,000, jambo ambalo siyo rahisi kwa mwananchi wa kawaida ambaye hana uwezo.

**MWENYEKITI:** Sawa. Kwa hiyo hoja yako ni kwamba Wizara ya Afya ije na tozo, ipendekeze tozo fulani ya shilingi 100.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sahihi kabisa, na sisi Wabunge tutajadili.

**MWENYEKITI:** Basi sawa, wamekusikia. Sasa hatuwezi kujadili ngazi hii kwa sababu umesema unatoa ushauri. Amesema anatoa ushauri kwa hiyo ninyi pokeeni ushauri wake.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeupokea ushauri wake kwa mikono miwili na tutaufanyia kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya. Wakati wa kupiga haya makofi tuwe na utayari na pale baadaye, tusianze alileta alipita huku, hapana. Makofi yamepigwa hapa ndani, Waziri atakapolileta tusianze kupita kushoto, kulia, kila mtu aliyepiga makofi hapa awe anahusika.

Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami sijaridhika katika jambo ambalo ni mahsusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna majengo yanajengwa ya hospitali za Wilaya na vituo vya afya, yanakaa muda mrefu kabla hayatumiki kwa sababu yamekosa vifaatiba. Nataka *commitment* ya Serikali, je, majengo haya yaliyomaliza kujengwa kwa mabilioni ya shilingi yanakaa mwaka mmoja, miaka miwili bila kufanya kazi, lini yatafanya kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kama tunaweza kupeleka, nimeona mfano Wizara ya Elimu, tulikwenda kujenga majengo ya madarasa na hawa wenzetu wa TAMISEMI, wamekwenda kujenga madarasa, tunajengewa darasa, wakati huohuo na madawati yamo na ubao umo, Mwanafunzi ameingia darasani kusoma, iweje tunajenga hospitali na vituo vya afya vya thamani kubwa halafu tunashindwa kupeleka vifaatiba watu wakaanza kutibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namshukuru Mheshimiwa Rais kwa hili lakini nataka *commitment* ya Wizara lini hospitali hizi za Wilaya na Vituo vya Afya vilivyojengwa nchi nzima vitaanza kufanya kazi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimemwelewa vizuri sana Kaka yangu kwa jambo alilolisema, yeye mwenyewe anajua na amesema kwamba Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwenye eneo hilo tu la vifaatiba kwa maana ya hela zilizokuwepo TAMISEMI mwaka huu ni bilioni 108. Lakini kwa nini sasa tumepata fedha nyingi lakini tumechelewa kufikisha vifaa kwa wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnakumbuka kuna kipindi hapa 2001 dunia nzima imefunga, ninamwomba Mheshimiwa Tabasam atuachie shilingi kwa sababu baada ya muda mfupi vifaa vitatembea. Mpaka sasa tunavyoongea kuna vituo zaidi ya 394 ambavyo vinasambaziwa vifaa mbalimbali vikiwemo vifaa vya watoto njiti kwenye vituo 120. Mkurugenzi wetu wa Tiba wamepanga kwenda kwenye kile kituo chako tukimaliza tu Bunge hili kwa ajili ya kuangalia mambo yanayotakiwa kwenda.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri uliposema 2001 ulimaanisha 2021, siyo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimaanisha 2021 wakati wa *corona*, viwanda vilifungwa na mambo mengi ya vifaatiba tunatoa kule nje.

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Tabasam ameridhika na majibu ya Serikali. Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Tumeshuhudia Watanzania wengi ambao unakuta wamepatwa na magonjwa yanayohitaji gharama nyingi kujitibia na wanashindwa kujitibia kwa kweli, wengine wanaishia kupata ulemavu na wengine kupoteza maisha. Pia kuna wengine ambao wana uwezo unakuta wanakata bima ya afya lakini haina *coverage* ya magonjwa mengine, wanaishia hapohapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mifano kadhaa tumeiona na hili namshukuru Mheshimiwa Rais, alifanya ziara kule Kagera akakutana na mtoto mmoja anaitwa Hamimu Baranyikwa, ambaye alikuwa ameshajikatia tamaa kabisa, akamsaidia na yule mtoto sasa hivi amehuisha matumaini, niliona hata anahojiwa anasema walau sasa hivi anaweza kwenda hata shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna Watanzania wengi sana ambao wanapatwa na hayo matatizo ambao hawafikiki, wanafariki dunia au wanakuwa walemavu. Wengine pia unakuta wanachangisha kwa Mkuu wa Wilaya wanapewa fomu, ile fomu hata asilimia mbili ya matibabu ambayo anatakiwa kutibiwa haifiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja yangu ni ipi, wakati Waziri ana-*wind up* hapa ameonesha kabisa kwamba, kwa mfano kwenye huu Ugonjwa wa Selimundu wametenga bilioni tano kuweza kuhakikisha kwamba watu wenye matatizo haya wanatibiwa. Sasa ninataka kupata *commitment* ya Serikali ya kuweza kuanzisha mfuko maalum ambao utasaidia hawa Watanzania ambao wanakutwa na matatizo haya hawawezi kujitibia, gharama ni kubwa sana wanaishia kupoteza maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine tuliona, alikuja hapa mtoto Esther, Madaktari Bingwa ndiyo walijichangisha eti ili mtoto aweze kufanyiwa *operation*. Sasa kama hao

Madaktari kwanza wanaamua kufanya hivyo kwa sababu wanaona kabisa mtoto hawezi kupoteza uhai chini yetu tunaweza tukamtibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali ibebe hii *burden* ianzishe huu mfuko maalum ambao unaweza ukatoka kwenye *sources* mbalimbali, siyo lazima tozo, Pato la Taifa na kwingineko, kuweza kuhakikisha mfuko unakua pale kuweza kuwasaidia Watanzania ambao wanapata hii shida. Kwa hiyo, ninataka hiyo *commitment* ya Serikali na nisiporidhika nitashika shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Huwezi kushika shilingi hii hoja si ni ya Mheshimiwa *Eng.* Stella Manyanya?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Ngoja, muwe mnasikiliza vizuri. Ndiyo maana mimi nikiwaambia msiongee wakati mwenzenu anasema muwe mnasikiliza. Hoja ya Mheshimiwa *Eng.* Manyanya ni hiyo, yaani wewe umeita mfuko, yeye kaita mfuko akaongeza na neno tozo kwa ajili ya huo mfuko. Hakuishia hapo tu kwenye kuanzisha mfuko, ndiyo maana baada ya Serikali kusema hivyo na yeye akawa ameridhika. Lakini hiyo hoja ndiyo hiyo hiyo, yaani kwamba kuna watu ambao hawana uwezo wanashindwa kutibiwa, Serikali itengeneze utaratibu wa kuwapa matibabu na ndiyo hoja yako. Sasa nipe utofauti wa hoja yako na ya Mheshimiwa Stella Manyanya.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tofauti mbili. Tofauti ya kwanza ni kwamba Mheshimiwa Manyanya ame-*narrow* kwenye tozo, mimi nime-*widen* na kwenye *sources*…

**MWENYEKITI:** Hujamsikiliza. Tozo amekuja kusema baadae, ameanza kwa kueleza Daktari anavyopata taabu

kwa kumuangalia mgonjwa ambaye hana uwezo wa kuhudumiwa kwa sababu hana pesa. Umemsikiliza sehemu hiyo ya mchango wake? Akaenda akaelezea huyu mwananchi ambae anaumwa ugonjwa ambao hawezi kupata matibabu kwa hiyo anasubiria kama anasubiria kifo chake. Umesikiliza akizungumza? Baadaye ndiyo akasema kwa nini Serikali, tena ametumia neno kwanini, kwanini Serikali isianzishe mfuko halafu akaendelea.

Sasa hizo sehemu zake mbili ulizoeleza sana sana wewe ni kwamba umeongea tu kwa nguvu lakini ndicho alichokisema. Sasa wewe unasema tofauti yake ni tozo, hoja yake haiko kwenye tozo, hoja yake iko kwenye kuanzisha mfuko kwa ajili ya Watanzania maskini wanaoshindwa kumudu gharama. *(Makofi)*

Sasa niambie tofauti ya pili labda nitaiona hiyo ya kwanza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti ya pili ni kwamba Mheshimiwa Manyanya ametoa ushauri, mimi nataka *commitment,* yeye ametoa tu ushauri, ushauri *may be taken or not be taken, commitment* siyo hivyo.

**MWENYEKITI:** *Commitment* Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameshasema, ama hujamsikia? Haya, Mheshimiwa Waziri wa Fedha rudia *commitment* yako kwa hoja ya Mheshimiwa *Eng.* Stella Manyanya.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa *Eng.* Manyanya amependekeza tuangalie uwezekano wa kuanzisha tozo kwa ajili ya kunusuru maisha ya Watanzania maskini na Serikali tumepokea kwa mikono miwili ushauri huo na tutaufanyia kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuongeza pia wakati mwenzangu Waziri wa Fedha ana-*make commitment* ya kuanzisha mfuko huo, lakini na hospitali zetu zinahudumia wagonjwa wasio na uwezo kwa msamaha. Ninazo takwimu kuanzia Julai, 2022 hadi Machi, Hospitali ya Taifa Muhimbili, *JKCI, MOI, Ocean Road,* Benjamin Mkapa, Mbeya, *KCMC,* Bugando na Hospitali za Rufaa za Mkoa zimetoa misamaha yenye thamani ya shilingi bilioni 88.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilitoka hoja ndani ya Bunge lako Tukufu nimeipenda, tukafanye tathmini ya misamaha hii, Je, ni kweli au ni misamaha ya kuandikwa. Kwa hiyo, hili pia tunakwenda kulifanyia kazi, watuambie ni misamaha ya *consultation fee,* ni msamaha wa dawa, ni msamaha wa upasuaji au msamaha wa kulazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri wa Fedha ana-*make commitment,* Serikali ya Rais Samia bado ni Sikivu, Mheshimiwa Mbunge wa Songea Mjini, Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro, kulikuwa na mtoto wa saratani, tukamtoa kwa *ambulance* yetu tumempeleka Muhimbili kahudumiwa. Mheshimiwa Mchungahela ni shahidi, kulikuwa na mtoto Mtwara - Lulindi mgonjwa, tumetumia gharama zetu. Kwa hiyo, bado Serikali ya Rais Samia inajali wananchi wanyonge wasio na uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwa na *sustainability* na kutowavunja moyo Madaktari wetu, nafurahi kumsikia Waziri wa Fedha akipokea hoja ya kuwa na fungu la kuhudumia hao. Ndiyo maana Rais Samia kaanza na bilioni tano, Ndugu zangu tushukuru, haikuwepo hata juzi, hiyo bilioni tano tu tunamshukuru kwamba imeanza, mimi naamini tutaenda vizuri zaidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri umetoa maelezo ya ziada hapo ni kwamba huo msamaha hauwafikii watu wote, ndiyo maana wako wanaofariki kwa kukosa huduma. Kwa

hiyo hii ngazi ya msamaha ni moja lakini wako hawa wanaokosa huduma pamoja na msamaha kuwepo. Kwa hiyo, nafikiri ile *commitment* mliyoifanya ni kwa ajili ya hili kundi ambalo hautamsikia Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro, sijui Mbunge wa wapi, yule mwananchi tu huku ambaye hata hafahamu. Kwa hiyo, nadhani hilo ndilo la msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri kwenye hoja hii nimeyasikia makofi kwa hiyo naamini watakuunga mkono kwenye kulianzisha hili ili Wabunge wasianze kumtafuta Waziri kwa ajili ya hiki na kile. Wajue tu kwamba utaratibu upo halafu mambo yanakwenda vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, Wabunge waliokuwa wanataka ufafanuzi hapa majina yao yamekwisha lakini pia muda wetu uliobaki ni wa kupitisha mafungu.

Katibu.

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 52 – Wizara ya Afya**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management* … … … … … … Sh. 7,602,257,864
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit* … Sh. 1,478,221,282
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit* … … Sh. 1,728,399,073
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*… … … … … Sh. 587,491,264
Kifungu 1005 – *Government Communication Unit*… … … … … … … … … … … Sh. 318,836,386
Kifungu 1006 – *Procurement Mgt Unit*… … … Sh. 1,375,458,660
Kifungu 1007 – *Legal Services Unit*… … … … … Sh. 450,349,148
Kifungu 1008 – *Information and Communication Technology Unit*… … … … … … ...Sh. 642,172,006
Kifungu 2001 – *Curative Services*… … … … Sh. 401,085,763,654

Kifungu 2003 – *Chief Medical Officer… … …* Sh. 22,270,949,395
Kifungu 2004 – *Nursing & Midwifery Services Division… … … … … … ... ... ... ...* Sh. 868,296,047
Kifungu 2005 – *Pharmaceutical Services Unit…* Sh. 883,587,831
Kifungu 2006 – *Diagnostic & Health Care Tech. Services Unit… … … ... ... ... ... .*Sh. 15,283,890,000
Kifungu 3001 – *Preventive Services… … … …*Sh. 26,526,863,260
Kifungu 3002 – *Health Quality Assurance Division… … … … … … ... ... ... ...*Sh. 798,962,340
Kifungu 3003 – *Health Emergency Preparedness Response Unit… … … … ... ... ... ..*Sh. 325,669,999
Kifungu 3004 – *Reproductive, Maternal & Child Health Division… ... ... ... .... … …* Sh. 306,790,000
Kifungu 4002 – *Social Welfare… … … … … … …* Sh. 62,000,000
Kifungu 5001 – *Human Resource Development… … … … … …*Sh. 20,355,950,791
Kifungu 6002 – *Bombo Regional Ref. Hospital – Tanga.….* Sh. 0
Kifungu 6003 – *Dodoma Regional Ref. Hospital … … … …* Sh. 0
Kifungu 6004 – *Geita Regional Ref. Hospital … … … … …* Sh. 0
Kifungu 6006 – *Kagera Regional Ref. Hospital … ..…. … …* Sh. 0
Kifungu 6007 – *Katavi Regional Ref. Hospital… … … … …* Sh. 0
Kifungu 6008 – *Ligula Regional Ref. Hospital – Mtwara … ..*Sh. 0
Kifungu 6010 – *Mara Regional Ref. Hospital … … … … … ..*Sh. 0
Kifungu 6011 – *Maweni Regional Ref. Hospital – Kigoma…*Sh. 0
Kifungu 6012 – *Mawenzi Regional Ref. Hospital – Kilimanjaro… … … … … … ... ... ...*Sh. 0
Kifungu 6013 – *Mbeya Regional Ref. Hospital .. … … … …* Sh. 0
Kifungu 6014 – *Morogoro Regional Ref. Hospital … … … …*Sh. 0
Kifungu 6015 – *Mt. Meru Regional Ref. Hospital – Arusha…*Sh. 0
Kifungu 6016 – *Mwananyamala Regional Ref. Hospital – DSM… … … … ... ... ... ... ... ... ... ..*Sh. 0
Kifungu 6017 – *Njombe Regional Ref. Hospital… … … … ...*Sh. 0
Kifungu 6018 – *Sekou Toure Regional Ref. Hospital – Mwanza… … … … … … ... ... ... ..*Sh. 0
Kifungu 6019 – *Shinyanga Regional Ref. Hospital … … … ..*Sh. 0
Kifungu 6021 – *Singida Regional Ref. Hospital … … … … ...*Sh. 0
Kifungu 6022 – *Sokoine Regional Ref. Hospital – Lindi … …* Sh. 0

Kifungu 6023 – *Songea Regional Ref. Hospital – Ruvuma*…Sh. 0
Kifungu 6024 – *Songwe Regional Ref. Hospital* … … … … ..Sh. 0
Kifungu 6025 – *Sumbawanga Regional Ref.*
*Hospital – Rukwa*… … … … … … … ... ... ... .Sh. 0
Kifungu 6026 – *Tabora Regional Ref. Hospital* … … … … …Sh. 0
Kifungu 6027 – *Temeke Regional Ref. Hospital – DSM*… … Sh. 0
Kifungu 6028 – *Tumbi Kibaha Regional Ref.*
*Hospital – Pwani*… … … … … … ... ... ... ... .Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## KITABU CHA NNE

## MIPANGO YA MAENDELEO

### Fungu 52 – Wizara ya Afya

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*… … Sh. 45,958,394,090
Kifungu 2001 – *Curative Services* … … … … Sh. 117,398,000,000
Kifungu 2003 – *Chief Medical Officer*… … … Sh. 58,300,000,000
Kifungu 2004 – *Nursing & Midwifery Services*
*Division*… … … … … … … … … …Sh. 44,950,000
Kifungu 2005 – *Pharmaceutical Services*
*Unit*… … … … … … … … … …Sh. 205,063,250,000
Kifungu 2006 – *Diagnostic & Health Care Tech.*
*Services Unit*… … … ... ... ... ... ..Sh. 1,449,902,378
Kifungu 3001 – *Preventive Services* … … … Sh. 121,419,898,904
Kifungu 3003 – *Health Emergency Preparedness*
*Response Unit*… … … … ... ... ... Sh. 181,000,000
Kifungu 5001 – *Human Resource*
*Development*… … … … … ... Sh. 27,142,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mtoa Hoja, taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati ya Matumizi kumaliza kazi yake, kwa mujibu wa Kanuni ya 123 (3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, ninaomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi yake, naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kutangaza rasmi kwamba Makadirio ya Mapato na Matumizi

ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 yamepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hivyo nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu na Watendaji wote chini ya Wizara hii kwa kupitishiwa bajeti yenu na Bunge. Tunawatakia kila la heri kwenye utekelezaji wa yale ambayo mmeyaahidi kwa Wabunge kupitia taarifa mliyoileta mbele ya Bunge, pia kupitia yale ambayo Wabunge wameyachangia na mmesema mnayachukua, mnaenda kuyafanyia kazi. Tunawatakia kila la heri katika utekelezaji wa hayo yote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati yetu ya Afya na Masuala ya UKIMWI; Mheshimiwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote tunawashukuru sana kwa kazi nzuri ya kuisimamia Wizara hii na pia kuendelea kufanya nao kazi kwa karibu kuhakikisha mambo yanaenda vizuri. Wabunge wengine ambao mmepata nafasi ya kuchangia kwenye bajeti hii, tunawashukuru sana kwa mawazo yenu ambayo bila shaka yataboresha utendaji wa Serikali kuhakikisha wananchi wetu wanakuwa na afya bora.

Waheshimiwa Wabunge, jambo moja kabla Mheshimiwa aliyeomba mwongozo hajapewa nafasi, Mheshimiwa Waziri kuna taarifa zinapitapita huko, huwa tunatamani sana tuwe na taarifa zenye uhakika hasa sisi wawakilishi wa wananchi ili tuwe tunawaambia wananchi. Upimaji wa homa ya tumbo, ni ile nikienda hospitali nikipima naweza kupewa majibu pale, ama ni jambo ambalo linachukua muda mrefu? Maana kila mtu anaambiwa na tunaambiwa kuna usugu wa dawa, na matumizi ya dawa yale yanakuwa ni makubwa sana. Sasa hizi hospitali zetu, vituo vinafuata ule utaratibu wa kutupima kama kweli nina homa ya tumbo ama wakishaniona nina homa, wakipima Malaria haipo, basi nina homa ya tumbo?

Nadhani pia na upimaji wa *UTI,* na yenyewe huwa inaleta hayo kwa maana ya maambukizi kwenye njia ya haja ndogo, na yenyewe ukienda tu hospitali wanakupima wanakwambia unaumwa hiki. Sasa kuna uhalisia hapo au hakuna? Nafikiri ni muhimu, kama yale mengine uliyosema mtakuja mwaeleze Wabunge namna mambo yanavyofanyika, na hili pia ni la muhimu ili tusiwe tunalishwa tu zile dawa halafu tunakuja kuumwa magonjwa ambayo yanasababishwa na hizi dawa na baadaye kuwa sugu katika yale magonjwa ambayo tungeweza kutibiwa na hizo dawa.

Kwa hiyo, haya mawili ndiyo nimewahi kuyasikiasikia. Kwa hiyo, ni muhimu pengine Wabunge tupate taarifa kuhusu jambo hili mtakapokuwa mmejiandaa upande wenu Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, nimpe nafasi Mheshimiwa Patrobass Katambi, inaonekana mwongozo wake hauwezi kabisa kusubiri. Mheshimiwa Patrobass Katambi.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kwa jambo ambalo lilitokea mapema leo asubuhi, lakini pia lilifuatia Mwongozo ulioombwa tarehe 11 Mei, 2023 wa Mheshimiwa Francis Mtega ambapo mbali na mambo mengine alieleza Mkoani Mbeya katika Kijiji cha Mwanavala katika Jimbo la Mbarali, Askari wa *TANAPA* walioenda na helikopta walifika pale na kuvamia wananchi lakini pia kuwapiga, na zaidi ng'ombe 250 waliporwa na askari hao na kwamba mbuzi wawili walikufa katika hiyo prukushani. Zaidi, wapo wanawake waliodharilishwa kwa kuvuliwa nguo na mambo mengine ambayo aliyaeleza na kwamba hata yule

aliyeporwa zile ng'ombe 250 alipata matatizo ya kisaikolojia na ikapelekea kutaka kujinyonga na hivyo ikalazimika ndugu jamaa na marafiki waendelee kuwa wanamlinda ili asije akafanya tukio hilo la kujitoa uhai *unnaturally*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufuatilia hilo, ilikuwa ni baada ya maswali ya papo kwa papo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, na baada ya hapo kiti chako kiliamuru aweze kupewa nafasi tena Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambaye mbali na mambo mengine alielekeza Waziri wa Maliasili na Utalii aende moja kwa moja kufanya ufuatiliaji wa jambo hilo, jambo ambalo alilifanya na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, pamoja na Kamati ya Usalama ya Mkoa wa Mbeya, sambamba na Kamati ya Usalama ya Wilaya Mbarali na Mkuu wa Wilaya pamoja na viongozi wa chama.

Mheshimiwa Spika, leo tumepata taarifa hiyo katika Bunge lako Tukufu ikifuatia tukio hilo la tarehe 6 Mei, 2023. Taarifa ambayo imetolewa na Waziri wa Maliasili na Utalii inakinzana kabisa na maelezo yaliyotolewa na Mbunge Mheshimiwa Francis Mtega ndani ya Bunge lako hili tukufu. Kwa msingi wa *good governance* na *rule of law,* kwa maana ya utawala wa sheria na utawala bora, na misingi ambayo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amejiwekea katika kuhakikisha anaendesha Serikali yake kwa kufuata misingi ya utawala bora na utawala wa sheria katika *4Rs,* kwa maana ya *Resilience*, *Reformation, Reconciliation* pamoja na *Rebuilding,* na sura yetu kama Taifa na muktadha wa kimataifa, jambo hili naliona kama linaleta ukakasi kwa maana ya taarifa zile ambazo zimekuwa zikiripotiwa vibaya sana kuhusu mbuga zetu na pengine inaweza ikapelekea shida aidha za kimasuala ya haki za binadamu na utawala, na zaidi linaweza likasababisha nchi kutafsiriwa tofauti.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kwa kanuni hiyo ya 76 ambayo imenisimamisha, niombe Mwongozo wako kama jambo hili linaruhusiwa ama haliruhusiwi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa jambo lipi sasa? Maana unaomba mwongozo kwa jambo lililotokea mapema leo. Jambo lipi unataka kujua kama linaruhusiwa ama haliruhusiwi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASACAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, jambo mahsusi hili ambalo lilipelekea Serikali kwenda kufanya kazi ya ziada kwa taarifa ambazo zilitolewa tarehe 11 Mei, 2023, na kwa mujibu wa kanuni kwamba zinaeleza mambo ambayo yatazungumzwa Bungeni yawe na ukweli kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge za mwezi Februari, 2023. Kwa hiyo, nilitaka kujua hapo, ukweli wake ukoje? Kama siyo ya kweli, basi yatoke kwenye taarifa za Bunge ili tusichelewe.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Patrobass Katambi, akiomba Mwongozo wa Spika kwa kutumia kanuni yetu ya 76 akitaka kujua jambo lililotokea mapema leo hapa Bungeni kama linaruhusiwa ama haliruhusiwi. Ametoa maelezo kwa kirefu ambayo sina haja ya kuyarejea. Kanuni aliyoitumia, leo tulichosikia hapa ndani ni taarifa ya Mheshimiwa Waziri kwa maana ya Kauli ya Serikali, ambapo ile kauli imeeleza baada ya kwenda kule, nini walichokikuta.

Sasa Mheshimiwa Patrobass kwenye ile taarifa ya Waziri, yeye kayachagua machache; yale ambayo Mheshimiwa Mbunge aliyasema kwamba ni uhalisia, hayo yeye kayaacha pembeni. Hata hivyo, kwa kanuni yetu hii ya 76, jambo lililotokea leo hapa Bungeni linahusu Kauli ya Serikali. Haliruhusu kauli aliyokuwa ameisema Mheshimiwa Mbunge wa Mbarali. Kwa hiyo, kama unataka kwenda kwenye njia hiyo ya kwamba kauli aliyokuwa ameitoa Mheshimiwa Mbunge na kwa maelezo haya yaliyotolewa na Waziri, kuna jambo hapo la kufanya, sasa hapo unaweza kutumia kanuni

nyingine ambazo zinakupa fursa hiyo. Wala usiwe na wasiwasi na utasikilizwa na maamuzi yatatolewa wakati huo. Kwa kutumia kanuni hii ya 76, jambo lililotokea hapa leo ni Waziri kutoa taarifa na hiyo taarifa inaruhusiwa kutolewa kikanuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, taarifa aliyoitoa Mheshimiwa Waziri inaruhusiwa na Kanuni yetu ya 36, inayoeleza kuhusu Kauli za Mawaziri na ndiyo maana mimi nimempa nafasi ya kutoa hiyo taarifa. Kwa hiyo, taarifa ile inaruhusiwa kutolewa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimepewa taarifa pia kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama nilivyokuwa nimewaeleza tulipokuwa tukianza Bunge letu mchana huu, alishaenda Kariakoo, amezungumza na wafanyabiashara na Kariakoo sasa ni shwari na biashara zinaendelea. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, hoja hiyo iliyokuwa imetolewa hapa Bungeni na Mheshimiwa Festo Sanga, kwa sababu nilisema naiacha mpaka tutakapopata taarifa, sasa tumeshapata taarifa, maana yake, hoja yake imefungwa rasmi. Serikali imechukua hatua kadhaa kwa maana ya utaratibu wake wa kawaida, imezifanyia kazi changamoto zilizokuwepo, na sasa soko linaendelea kufanya kazi.

Kwa hiyo, nitumie fursa hii kuipongeza Serikali kwa kuchukua hatua baada ya hiyo changamoto iliyojitokeza Kariakoo, na tunamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hatua alizozichukua.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club,* anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa matokeo ya mechi iliyofanyika tarehe 13 Mei, 2023 kati ya *Bunge Sports Club* na *Kaliua Veteran* kutoka Mkoani Tabora, ni kama ifuatavyo:-

Timu ya *Bunge Sports Club* ilipata magoli mawili na timu ya Kaliua *Veteran* ilipata goli moja. Mfungaji wa magoli kwa upande wa *Bunge Sports Club* alikuwa Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki. *(Makofi)*

Ahsante sana Mheshimiwa. Nadhani kwa muktadha wa hitimisho alilolitoa Mheshimiwa Waziri hapa, wewe utakuwa haumo kwenye zile changamoto alizozitaja Mheshimiwa Waziri. *(Kicheko)*

Haya, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.51 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 14 Mei, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*